JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam.Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi: 255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. FA.27/249/01/2014/2015/42/01 28 Machi 2016

Mh. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
Barabara ya Barack Obama, Na.1
11400, DAR ES SALAAM.

YAH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na mabadiliko na kama ilivyoainishwa katika Sehemu ya 11(4) ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, nawasilisha kwako ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa mwaka wa fedha 2014/15 kwa ajili ya kuiwasilisha Bungeni kulingana na matakwa ya sheria.

Wako Mwaminifu,

Prof. Mussa Juma Assad
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
(Kama ilivyoanzishwa chini ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
Majukumu ya kisheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) na kufafanuliwa na Sheria ya Ukaguzi ya Umma, Na. 11 ya mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa) na kufafanuliwa na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009.

Dira ya Ofsi
Kuwa kituo bora kwenye ukaguzi wa hesabu katika sekta ya ukaguzi wa umma.
Lengo la Ofisi
Kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji unaozingatia thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Misingi Yetu

Kutopendelea:	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki bila upendeleo.
Ubora:	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya ukaguzi.
Uadilifu:	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha maadili ya kazi ya kiwango cha juu na kuheshimu sheria.
Kujali Watu:	Tunajali mahitaji ya wadau kwa kujenga utamaduni mzuri wa kujali wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na kuongeza tija.
Ubunifu:	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya taasisi.
Matumizi bora ya Rasilimali za Umma:	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi inayozingatia matumizi bora ya rasilimali zilizokabidhiwa kwake.

YALIYOMO

YALIYOMO iv
ORODHA YA MAJEDWALI vi
ORODHA YA VIFUPISHO vii
SHUKRANI xiv
MUHTASARI KWA WAANDAMIZI xviii
SURA YA KWANZA 1
UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA 1
SURA YA PILI 6
AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA 6
SURA YA TATU 10
UKAGUZI WA MIAKA ILIYOPITA 10
SURA YA NNE 18
MASUALA YALIYOPEWA UZITO KATIKA UKAGUZI 18
SURA YA TANO 62
MAPITIO YA MIKAKATI NA UENDESHAJI WA KIUFANISI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA 62

SURA YA SITA 133
UFUATILIAJI NA UTATHIMINISHAJI WA UBINAFSISHAJI 133
SURA YA SABA 143
MASUALA MENGINEYO MUHIMU 143
HITIMISHO 171
VIAMBATISHO 173

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Hati zilizotolewa kwa kipindi cha miaka minne mfululizo kutoka 2011/2012 hadi 2014/2015.....8
Jedwali 2: Mikopo Iliyotolewa zaidi ya Asilimia 50 ya Thamani ya Mali za SACCOS..... 35
Jedwali 3: Utofauti wa kumbukumbu kati ya bidhaa zilizo katika mfumo wa Mamlaka ya bandari na mfumo wa Mamlaka ya Mapato 40
Jedwali 4: Wakopaji Waliotumia Fedha kwa Malengo Yasiyokusudiwa 48
Jedwali 5: Madeni yaliyokaa muda mrefu 52
Jedwali 6: Ucheleweshaji wa Kukamilika kwa Ujenzi wa Miradi 56
Jedwali 7: Ufanisi katika Ukusanyaji wa Kodi ya Pango 57
Jedwali 8: Mapato yaliyopotea Kutokana na Upotevu wa Maji 58
Jedwali 9: Ucheleweshaji na kutopelekwa kwa makato ya kisheria 59
Jedwali 10: Mwenendo wa hali ya kifedha wa Shirika la Ndege Tanzania 71
Jedwali 11: Ulinganifu wa bajeti na mapokeo halisi ya fedha kwa kipindi cha miaka minne iliyopita..... 87

ORODHA YA VIFUPISHO

ADB	Benki ya Maendeleo ya Afrika
ADS-B	Mfumo wa Moja kwa Moja wa Kutangaza Matokeo ya Uchunguzi
AFROSAI-E	Umoja wa Ofisi za Taifa za Ukaguzi za Nchi za Kiafrika Zinazozungumza Lugha ya Kiingereza
AHEL	Kampuni ya Azimio
AIDS	Upungufu wa Kinga Mwilini
AMHS	Mfumo wa Utunzaji wa Mawasiliano ya Ndege
AOC	Cheti cha Mwendeshaji wa Huduma za Ndege
APFW	Dirisha la Mikopo ya Miradi ya Kilimo
ARMS	Mfumo wa Ufuatiliaji wa Muda wa Hewani wa Simu
ATC	Shirika la Ndege Tanzania
ATCL	Kampuni ya Ndege Tanzania
ATM	Mfumo wa Usimamizi wa Safari za Ndege
AUWSA	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa MazingiraArusha
BAUWASA	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa MazingiraBabati
BMAF	Taasisi ya Ukimwi ya Benjamin Mkapa
BoQ	Orodha ya Mahitaji na gharama za Ujenzi
BoT	Benki Kuu ya Tanzania
CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali
CAPEX	Matumizi Katika Vitu Vinavyodumu Muda Mrefu
CBE	Chuo cha Elimu ya Biashara
CDA	Mamlaka ya Uendelezaji wa Makao Makuu
CEIR	Kifaa cha Kuwandikisha Utambuzi
CFSs	Kituo cha Kusafirisha Mizigo
CHC	Shirika Hodhi ya Mali za Serikali

CIDA	Wakala wa Maendeleo wa Kimataifa wa Watu wa Canada
CMS	Mfumo wa Usimami wa Forodha
CMSA	Mamlaka ya Masoko ya Mitaji
CNC	Mfumo wa Kompyuta wa Usimamizi wa Namba
COSTECH	Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania
DANIDA	Wakala wa Maendeleo wa Kimataifa wa Watu wa Denmark
DAWASCO	Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam
DBOT	Mfumo wa Kubuni Kujenga Kuendesha na Kuhamisha
DFID	Shirika la Maendeleo na Ufadhili la Uingereza
DIT	Chuo cha Teknolojia Cha Dar es Salaam
DMGP	Mradi wa Mlango Bahari wa Dar es Salaam
DMI	Chuo cha Mabaharia Dar es Salaam
DTT	Mfumo wa Matangazo ya Luninga wa Kidijitali
DUCE	Chuo Kikuu Kishiriki Cha Elimu Dar es Salaam
EADB	Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki
EFD	Kifaa cha Ukusanyaji Fedha cha Kielektroniki
ERP	Mfumo wa Upangaji na Matumizi ya Rasilimali za Biashara
EWURA	Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Nishati na Maji
GIZ	Shirika la Maendeleo la Serikali ya Watu wa Ujerumani
GoT	Serikali ya Tanzania
GVG	Kundi la Sauti za Dunia
HESLB	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu
HIV	Virus vya Ukimwi
HQ	Makao Makuu
IAS	Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu
IATA	Jumuiya ya Usafirishaji wa Anga ya Kimataifa
ICAO	Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga

ICD	Bandari Kavu
IFAC	Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu
IFM	Chuo cha Usimamizi wa Fedha
IFRS	Mfumo wa Kimataifa wa Kutoataarifa na Uandaaji wa Hesabu
IMO	Jumuiya ya Mabaharia Duniani
IMTU	Chuo cha Kimataifa cha Tiba na Teknolojia
INTOSAI	Jumuiya ya Ofisi za Taifa za Ukaguzi ya Kimataifa
IOSA	Ukaguzi wa Usalama Viwanjani wa Kimataifa
IPSASs	Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Taasisi za Umma
ISA	Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu
ISSAIs	Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu wa Taasisi za Umma
JV	Umiliki wa Kampuni kwa Ubia
KM	Kilometa
KMTC	Kampuni ya Kutengeneza Vipuri vya Mashine Kilimanjaro
KOJ	Gati ya Kupakulia Mafuta ya Kurasini
KPI	Kiashiria cha Utendaji
KUWASA	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kigoma
LAPF	Mfuko wa Pensheni wa LAPF
LART	Mfuko wa Mikopo na Karadha
LCMS	Mfumo wa Kusimamia na Kudhibiti Mawasiliano ya Ndani
LUWASA	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi
MCST	Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia
MNH	Hospitali ya Taifa ya Muhimbili
MOF	Wizara ya Fedha
MOI	Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili
MoU	Randama za Makubaliano

MSD	Bohari Kuu ya Dawa
MUCCOBs	Chuo cha Ushirika na Biashara Moshi
MUST	Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya
MWAUWASA	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza
MZARTC	Kampuni ya Biashara ya Mkoa wa Mwanza
NACTE	Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi
NAOT	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
NAPOCO	Kampuni ya Taifa ya Taifa ya Ufugaji wa Kuku
NARCO	Kampuni ya Ranchi za Taifa
NBC	Benki ya Taifa ya Biashara
NCAA	Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro
NDC	Shirika la Maendeleo la Taifa
NECTA	Baraza la Mitihani la Taifa
NHC	Shirika la Nyumba la Taifa
NHIF	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya
NIMR	Taasisi ya Taifa ya Uchunguzi wa Malaria
NIP	Taasisi ya Tija ya Taifa
NIT	Taasisi ya Taifa ya Usafirishaji
NSSF	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii
OUT	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
PA &oBs	Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma
PAA	Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008
PAC	Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali
PAYE	Lipa Kodi Kadri ya Pato Lako
PC	Kompyuta ya Mezani
PFMRP	Mpango wa Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma
PMG	Mlipaji Mkuu wa Serikali
PPF	Mfuko wa Pensheni wa PPF

PPL	Kampuni ya Kusimamia Mali za Mifuko ya Pensheni
PPP	Ushirikiano wa Taasisi za Umma na Binafsi
PPRA	Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma
PRIDE	Taasisi ya Kukuza Maendeleo Vijijini
PSPF	Mfuko wa Pensheni wa Sekta ya Umma
PSRC	Tume ya Rais ya Kurekebisha na Kubinafsisha Mashirika ya Umma
QoS	Ubora wa Huduma
RAHCO	Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli Tanzania
RFP	Maombi ya Kuwasilisha Zabuni
RIF	Mfuko wa Miundombinu ya Reli
RMS	Mkakati wa Uhamasishaji Rasilimali
SAA	Shirika la Ndege la Afrika Kusini
SACCOS	Chama cha Ushirika cha Kuweka na Kukopa
SAI	Taasisi ya Ukaguzi ya Taifa
SAT	Kampuni ya Matengenezo na Ukarabati wa Ndege ya Afrika Kusini
SGS	Kampuni ya Usimamizi wa Viwango ya Kimataifa
SHUWASA	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga
SIDA	Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Watu wa Sweden
SNAO	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden
SPM	Kiwanda cha Karatasi Kusini
SSRA	Mamlaka ya Udhibiti ya Hifadhi za Jamii
SUMATRA	Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi kavu na Majini
TAFIRI	Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania
TANAPA	Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa
TANESCO	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania
TBC	Shirika la Utangazaji Tanzania
TBS	Shirika la Viwango Tanzania

TBT	Bodi ya Chai Tanzania
TCAA	Mamlaka ya anga Tanzania
TCB	Bodi ya Kahawa Tanzania
TCRA	Mamlaka ya Udhibiti Mawasiliano Tanzania
TEU	Kipimo cah Kontena cha Futi Ishirini
TFDA	Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania
TIC	Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania
TICTS	Kituo cha Huduma za Makontena ya Kimataifa
TLTC	Kiwanda cha Uchakataji wa Tumbaku
TMB	Bodi ya Nyama Tanzania
TNBC	Baraza la Taifa la Biashara Tanzania
TPA	Mamlaka ya Bandari Tanzania
TPDC	Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania
TPRI	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa
TR	Msajili wa Hazina
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania
TRL	Shirika la Reli Tanzania
TSN	Kampuni ya Magazeti Tanzania
TTCL	Kampuni ya Simu Tanzania
TTMS	mradi wa mfumo wa usimamizi wa nyendo za mawasiliano ya simu
TZS	Shilingi ya Tanzania
UCSAF	Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote
UDA	Shirika La Usafiri Dar es Salaam
UDOM	Chuo Kikuu Cha Dodoma
UNICEF	Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani
URT	Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
USAID	Shirika la Msaada la Marekani
USD	Dola ya Marekani

UTT-AMIS	Mfuko wa Uwekezaji Tanzania wa kusimamia Mali na Uwekezaji
UTT-PID	Mfuko wa Uwekezaji Tanzania wa Kusimamia Miradi na Maendeleo ya Ujenzi
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani
WB	Benki ya Dunia
WHC	Kampuni ya Nyumba za Watumishi
WHO	Shirika la Afya Duniani
WHT	Kodi ya Zuio
WMA	Wakili wa Vipimo

SHUKRANI

Ninapenda kuchukuwa nafasi hii adhimu kwa niaba ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kumpa pongezi za dhati Mheshimiwa, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia kumtakia kila mafanikio katika kipindi hiki ambacho Watanzania wana matarajio makubwa kutoka kwake. Ninaomba nikuthibitishie kuwa ofisi yetu itakupa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yako kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pongezi zangu za dhati kwa pia ziende Spika na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge; pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kuchaguliwa katika Bunge hili tukufu. Ofisi yangu inaahidi kuwapa kila ushirikiano katika kuyafikia malengo ya kujenga taifa letu.

Pia ninampongeza Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msaada mkubwa aliotupatia katika kipindi chake cha Urais ambao umesaidia katika mafanikio ya ofisi yangu.

Ninapenda kuwashukuru Wabia wa Maendeleo ambao wamekuwa wakiisaidia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, hususani Mpango wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP), chini ya usimamizi wa Benki ya Dunia; Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden ; Serikali ya Sweden kupitia shirika la Kimataifa wa Maendeleo wa Watu wa Sweden; Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza ; Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Watu wa Ujerumani Benki ya Maendeleo ya Afrika ; shirika la Maendeleo la Kimataifa la Watu wa Marekani ; Taasisi ya Ukaguzi ya Taifa la India ; Taasisi ya Ukaguzi ya Taifa la China ; Taasisi ya Ukaguzi ya Taifa la Norway ; Taasisi ya Ukaguzi ya Taifa la Uholanzi ; Umoja wa Ofisi za Taifa za Ukaguzi za Nchi za Kiafrika zinazozungumza lugha ya Kiingereza; shirika la Maendeleo la Kimataifa la Canada ;na wadau wote wanaoitakia mema Ofisi yangu na waliochangia kwa sehemu kubwa kuifanya kuwa ya kisasa katika kutekeleza majukumu yake ya kikaguzi kwa kufadhili mafunzo ya wafanyakazi na kutupatia vitendea kazi mbalimbali pamoja na msaada wa kiutaalamu.

Aidha, ninapenda kuyashukuru makampuni binafsi ya ukaguzi ambayo yamekuwa yakifanya ukaguzi wa hesabu za mashirika ya umma. Mchango wao katika kukamilisha repoti hii unathaminiwa sana. Pia, Ofisi yangu inashukuru kwa ushirikiano unaoendelea kuonyeshwa na Bodi za Wakurugenzi, Maofisa Masuuli, Wasimamizi, Waandamizi na wafanyakazi wa Mashirika ya Umma tunayoyakagua kwa ushirikiano waliotupatia wakati wa kufanya ukaguzi huu.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru sana wafanyakazi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa jitihada walizoonyesha katika kuwandaa na kukamilisha ripoti hii. Kujitolea kwao na kujituma kumekuwa na manufaa na faraja sana kwangu. Ninawasihi waendelee kuwa na moyo huo kwa siku ijazo ili kuendelea kudumisha na kuinua heshima ya Ofisi yetu katika kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora, na kuhimiza uwajibikaji na kuzingatia thamani ya fedha katika makusanyo na matumizi ya rasilimali za umma.

DIBAJI

Ninayo furaha na heshima kuwasilisha Ripoti Kuu ya Mwaka ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa mwaka 2014/2015 ili linatekeleza matakwa ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sura ya 34 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

Ripoti hii ni mkusanyiko wa masuala muhimu yaliyojitokeza katika kaguzi za Mashirika ya Umma kwa vipindi vinavyoishia tarehe 30 Septemba 2014, tarehe 31 Disemba 2014 na tarehe 30 Juni 2015. Pia, ripoti hii imejumuisha mapendekezo yaliyotolewa kwa wasimamizi wa mashirika haya ili kupunguza mapungufu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi.

Ripoti hii pia inajumuisha masuala ya kimkakati na ufanisi katika utendaji wa Mashirika kwa lengo la kujibu maswali muhimu ya kisera au changamoto muhimu na vikwazo vya kiutendaji ambavyo vinaathiri mikakati, mipango, na ufanisi wa Mashirika ya Umma.

Ripoti pia inajumuisha matokeo ya kaguzi maalumu zilizofanyika katika mwaka wa mahesabu wa 2014/2015. Kaguzi hizi zilifanyika kwa mujibu wa Sura ya 29 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 ambayo inampa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mamlaka kufanya aina yoyote ya ukaguzi pale anapohitaji kufanya hivyo au, kwa kuombwa na mtu yeyote, taasisi, Mashirika ya Umma, Wizara, Idara, Wakala na Serikali za Mitaa na vyombo vyovyote vinavyohitaji kufanya ukaguzi maalumu.

Kutokana na mwamko wa jamii katika kuongezeka kwa uwajibikaji, uwazi na utawala bora; maamuzi sahihi ni muhimu sana. Kwa hiyo ni imani yangu kuwa ripoti hii itaisaidia Serikali pamoja na Bunge katika kuwakumbusha wasimamizi wa taasisi

hizi za umma ambao wamekasimiwa mamlaka ya kukusanya, kutumia na kusimamia rasilimali za umma ili kwa pamoja tuweze kuleta mabadiliko katika maisha ya Watanzania.



Prof. Mussa Juma Assad
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI
28 Machi 2016

MUHTASARI KWA WAANDAMIZI

i. Utangulizi

Muhtasari huu unaainisha kwa kifupi masuala mahususi yaliyojadiliwa kwa kina katika ripoti hii na ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti ya Taasisi husika ili kuhakikisha kuna ufanisi katika utendaji wa Mashirika ya Umma.

Ripoti hii inajumuisha hoja mbalimbali zilizotolewa katika ripoti za ukaguzi za Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma zinazoonesha kuwapo kwa mapungufu yanayokwamisha utendaji wa mashirika na taasisi hizo ambazo zinahitajika kufanyiwa kazi kwa haraka. Masuala yaliyoainishwa kwa kifupi ni kama ifuatavyo:

ii. Hati za Ukaguzi na Ripoti Zilizokaguliwa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2014/2015 nilikagua na kukamilisha kaguzi za mashirika 158 kati mashirika 185 yaliyotakiwa kukaguliwa. Kati ya kaguzi 158 zilizofanyika, kaguzi za hesabu za mashirika 115 zilitolewa maoni ya ukaguzi. Kati ya kaguzi za mashirika 115 zilizokamilika na kutolewa maoni (hati) ya ukaguzi, mashirika na taasisi za nyingine za umma, mashirika 3 yalipata hati yenye mashaka wakati mashirika 97 yalipata hati zinazoridhisha. Hati isiyoridhisha na hati mbaya hazikutolewa kwa shirika lolote au taasisi nyingine za umma katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha 2014/15

iii. Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka Iliyopita

Katika kipindi cha mwaka 2014/2015 , nilifuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za miaka iliyopita. Mapendekezo 10 yaliyotolewa miaka 7 iliyopita hayajatekelezwa hadi sasa. Mapendekezo haya yanapatikana katika sura ya tatu (3) ya ripoti hii. Mapendekezo hayo ni pamoja na haja ya kuwanzisha Mfuko wa Uwekezaji wa Umma; Usimamizi wa Mali Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM); Mauzo ya Hisa za UDA; kutelekezwa kwa Mita za Kupimia Mafuta Yanayoingia Bandarini katika Mamlaka ya Bandari Tanzania; Umiliki wa Azania Bancorp Limited na PRIDE Tanzania; na Ubinafsishaji wa Kiwanda cha Karatasi Mgololo-Southern Papaer Mill (SPM).

iv. **Masuala Yaliyopewa uzito katika Ukaguzi**

Kumekuwa na amana za makontena za muda mrefu zenye kiasi cha Shilingi milioni 536.19 kwa makampuni ya usafirishaji wa mizigo Bandarini; pamoja na upatikanaji wa dawa na kuhifadhiwa kwa muda mrefu vifaa vya matibabu yenye thamani ya Shilingi bilioni 17.19 katika Bohari ya Madawa (MSD). Aidha, Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) haikuweza kukagua chakula kilichoagizwa kutoka nje ya nchi chenye thamani ya Shilingi bilioni 4.64 kutokana na uwezo mdogo. Tulibaini mfumo wa mawasiliano (UCSAF) ulishindwa kukusanya madeni kiasi cha Shilingi milioni 827.98 ikiwa ni ada ya ushuru wa huduma. Tulibaini ucheleweshaji wa ujenzi kwa mashirika 6 ya umma. Ujenzi huo unagharimu kiasi cha Shilingi milioni 132.95.

Tuligundua kuwepo kwa mikopo mahsusi ambayo haikulipwa kiasi cha Shilingi bilioni 827.98, mikopo hiyo inawahusu wafanyakazi wa waliostaafu. Pia kuna dosari ya usimamizi wa mradi wa makazi ambao unatekelezwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii. Pia, tulibaini mapato haya kukusanywa kutokana na maji yaliyotumika yenye kufikia kiasi cha Shilingi bilioni 17.96 ya mamlaka tatu (3) za maji na ucheleweshwaji wa miradi katika taasisi sita (6)za umma.

Ukaguzi wa mapato ya Mamlaka ya bandari ulibaini kwamba, kati ya meli 1,253 ambazo zilikuwa zimeegeshwa katika bandari ya Dar es Salaam, meli 145 hazikujumlishwa kwenye mfumo wa mapato. Menejimenti iliweza kutoa maelezo na viambatanishi vya meli 60, lakini 85 zilizobaki hazikuwa na nyaraka ya kuwambatanisha, hivyo kuleta wasiwasi kama mapato yalikusanywa kutoka kwenye makontena haya. Bila kuwa na usimamizi bora, mapato mengi yanaweza kupotea.

Pia tulibaini kuwepo kwa tofauti ya mizigo 1742 kati ya taarifa za mfumo wa kielektroniki wa Mamlaka ya bandari na ule wa Mamlaka ya mapato. Tofauti inaweza sababisha mapato ya Mamlaka kupotea. Kuna uhitaji wa Mamlaka ya bandari na Mamlaka ya mapato kufanya usuluhishowa taarifa ili kuthibiti upotevu wa mapato.

Meli mbili ziliruhusiwa kutoka na maafisa wa idara ya uendeshaji badala ya kitengo cha mapato cha meli na pia meli moja iliruhusiwa kutolewa na idara ya majini ilitolewa lakini hakuna

taarifa iliyotumwa kwa idara ya mapato. Hii inaweza pelekea upotevu wa mapato kwa Mamlaka ya bandari na Mamlaka ya mapato.

Kiwanda cha SAAFI kilipewa mkopo kutoka benki ya TIB kiasi cha Shilingi bilioni 2.5, mpaka kufikia 31 Disemba, 2014 hakuna fedha iliyorudishwa.Tathmini zaidi kwenye taarifa ya banki ilibaini kiwanda cha SAAFI kilipewa mkopo mwingine kupitia Export Credit Guarantee Scheme wa Shilingi bilioni 14.95 iliyotolewa na serikali kupitia bank ya TIB. Aidha, makampuni matano pia yalikuwa yanadaiwa na ECGS kiasi cha Shilingi bilioni 45.71. Mikopo hii imekuwepo kwa zaidi ya miaka kumi (10) bila kufilisiwa.

Ukosefu wa mipango katika miridi , ubunifu na usimamizi ikiwemo ukosefu wa uTathmini wa mradi kabla ya kutoa mikopo zinapelekea utendaji na usimamizi mbaya katika mikopo,hivyo kuna uwezekano mkubwa wa serikali kupitia benki ya TIB kutolipwa deni hilo.
Hivyo basi mikopo inashauriwa itolewe kwa wakopaji ambao wame tathminiwa na wana uwezo wa kurudisha mikopo.

Mfuko wa Taifa wa hifadhi ya jamii (NSSF) ulianza mradi wa kujenga Satellite town ndani ya wilaya ya Arumeru-Arusha kupitia ubia wake na Kampuni ya Hifadhi Builders ltd. Mradi huu ulitegemewa kugharimu Dola za Marekani 3,340,589,543 sawa na shillingi trilioni 7.2. Tarehe 21 Januari, 2016 Mfuko wa Taifa wa hifadhi na AHEL waliingia makubaliano ya kusimamisha utekelezaji wa mradi huu kwa kuridhiana kati ya AHEL na Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Taifa wa hifadhi ya jamii.

Kampuni ya ubia Hifadhi Builders ilichukuwa mkataba kutoka AHEL kwa ajli ya kubuni mradi na kusimamia kwa gharama ya Dola za Marekani za 218,087,643 sawa na Shilingi milioni 468.9. Hata hivyo, wakati mkataba ulipokatishwa, jumla ya Shilingi bilioni 43.9 (sawa na Dola za Marekani bilioni 20.1) zililipwa ambazo kulingana na mkataba, kiwango hicho kiligeuzwa kuwa mkopo kwa AHEL kwa riba ya asilimia 3 kwa mwaka.

Kuingia kwenye mradi bila kuthibitisha upatikanaji wa fedha kusaidia miradi inaweza kusababisha gharama zisizo na lazima na

matumizi yasiyofaa ya rasilimali kwa upande wa Mfuko wa Taifa wa hifadhi ya jamii.

v. **Tathmini ya mikakati ya utendaji na ufanisi wa mashirika na taasisi za umma**

Tathmini ya utendaji na ufanisi wa Mashirika ya Umma iliyofanyika imegundua masuala muhimu yafuatayo:
Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ipo katika hali mbaya ya kifedha kutokana na kuzorota kwa hali ya kifedha pamoja na kupata hasara kwa zaidi ya miaka tisa mfululizo.

Manejimenti ya Kampuni ya Ndege Tanzania haijaweza kubuni mkakati wa kulirudisha shirika katika hali inayoridhisha kwa kuliondoa kwenye hali mbaya ya kifedha inayoikabili.

Ubinafsishaji wa kampuni ya Ndege Tanzania uliofanywa kwa kampuni ya Afrika Kusini haukuweza kuleta ufumbuzi wowote wa matatizo ambayo yalikuwa yanaikabili kampuni, Badala yake, iliendelea kuipa mzigo mkubwa Kampuni ya Ndege Tanzania kupitia ongezeko la gharama na ada ya usimamizi; gharama kubwa za matengenezo; gharama kubwa za kukodisha ndege; na gharama za uendeshaji.

Tulibaini changamoto kadhaa katika uendeshaji wa Mamlaka ya Anga Tanzania, ambapo kulikuwa na ukosefu wa utawala bora na usimamizi wa mradi wa ADSB, pamoja na uwezo duni ndani ya Mamlaka ya Anga Tanzania katika mipango ya matumizi ya teknolojia. Hii iliashiria kuwa wafanyakazi husika hawana uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia. Tuligundua, kutokubadilishwa kwa mfumo uliopo wa rada ambao unatumia teknolojia ya kizamani na ambayo kwa sasa wasambazaji wake hawapo tena katika soko kwa ajili ya kusaidia uendeshaji wa mfumo huo wa rada. Jambo hili ni la hatari zaidi kwa usalama wa nchi na anga zetu pamoja na ndege zinazopita katika anga yetu.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), haikufanya upembuzi yakinifu wala tathmini sahihi ya vihatarishi vya Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano. Pia, tulibaini kutokuwepo kwa mawasiliano sahihi miongoni mwa wadau wa mradi huu wa mawasiliano. Udhaifu huu umesababisha kutoingizwa kwenye mkataba wa Mfumo wa Usimamizi wa mawasiliano kwa baadhi

ya moduli muhimu za uhakiki wa mapato kwa watumiaji wa simu wa ndani ya nchi.

Mamlaka ya Usimamizi wa Nishati na Maji (EWURA) haikuweza kuwandaa taarifa ya mapitio ya utendaji kwa sekta za umeme na gesi asilia. Aidha, Mamlaka haikuwandaa taarifa ya mpango kazi na utekelezaji wa mpango huo kwa ajili ya kukabiliana na changamoto zote zinazokabili mpango kazi wake kwa mwaka husika.

Kituo cha Uwekezaji (TIC), hakikuwa na ufanisi katika ufuatiliaji na tathmini ya mifumo. Tuligundua, ukosefu wa taarifa za ushirikiano kati ya Kituo cha Uwekezaji na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Halikadhalika tuligundua kutokuwasilishwa kwa taarifa za mwekezaji na ukosefu wa ufahamu kwa wawekezaji juu ya shughuli zinazofanywa na Kituo cha Uwekezaji

RAHCO ilikuwa na viashiria vinne vya utendaji katika mwaka 2012/13-2014/15, baadhi ya viashiria vya utendaji vilitekelezwa lakini hatukuweza kuTathmini ni vipi matokeo yatapimwa, kwa sababu viashiria vya utendaji vilikuwa ni sentensi ambazo hazikutoa ufafanuzi jinsi malengo yatafikiwa. Kampuni ilipata changamoto kadhaa katika kutekeleza mipango wa mikakati ambayo inahusisha Shirika la Reli (TRL) kulipa ada ya mkataba na malipo mengine ya kisheria, fedha za miundombinu ya reli kutokuwa na utendaji, uwezo wa RAHCO kuchukuwa mipango mingine ya kitaifa na uwekezaji mkubwa unaohitajika kwa maendeleo ya mtandao wa reli. Mapungufu katika kuweka malengo, viashiria dhaifu vya utendaji vinaweza kuwathiri uwezo wa kampuni kufikia malengo yake.

Tumebaini kuwa, TPA wameshindwa kufikia sehemu kubwa ya Viashiria Muhimu vya Kiutendaji (KPI), ukaguzi wetu umebaini kuwa, moja ya maegesho ya meli haifanyi kazi kutokana na miundombinu yake kuwa ya kizamani, imeharibika kufikia kutotengenezeka na baadhi yake kuondolewa kutokana kuendelezwa kwa Gati Na. 13 na 14. Pia tumebaini matumizi ya Shilingi milioni 1,327.14 ambazo zilitumika kwa ajili ya ukarabati na matengenezo ya meli ambayo imekuwa katika bandari ya Mombasa kwa muda mrefu.

Pia tumebaini mapungufu katika utekelezaji wa miradi iliyoainishwa kwenye Mpango Mkuu wa Bandari wa hadi mwaka 2028, udhaifu katika mkataba ulioingiwa kati ya TICTS na TPA unaohusu makubaliano ya kusimamia na kuendesha Kituo cha

Kuhifadhi Makontena, Kusitishwa kwa ujenzi wa Kituo cha Kusafirishia Mizigo cha Kisarawe na udhaifu katika uendeshaji wa Bandari Kavu na Kituo cha Kusafirishia Mizigo kama kukosa udhibiti katika Bandari Kavu au Vituo vya Kusafirisha Mizigo na kukosekana kwa taratibu za wazi na vigezo ambavyo vinatumika kugawanya mizigo miongoni mwa Bandari Kavu na Vituo vya Kusafirisha Mizigo .

Mapungufu yafuatayo yamebainika ndani ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC); kutokufanyika kwa Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Rasilimali kwa miradi minne iliyoanzishwa na NDC, kutokuweka fedha za kutosha kwenye miradi ambayo imesababisha NDC washindwe kuwa na hisa nyingi zaidi kwa kuwa hakuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji, kiasi ambacho wawekezaji binafsi wanachangia zaidi hivyo kuwa wawekezaji wakubwa na hivyo kuwa katika nafasi ya kudhibiti maamuzi kwenye kampuni za ubia zilizoanzishwa.
Kumekuwepo kutumika chini ya kiwango kwa Kampuni ya Kutengeneza Zana ya Kilimanjaro (KMTC); kiwanda kimekuwa kikifanya kazi katika kiwango cha chini sana hivyo kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Taarifa ya maendeleo ya kiwanda imeonyesha uzalishaji wa hali ya chini ambapo katika kipindi cha Julai 2014 na Novemba 2015 mapato yaliyokusanywa yalikuwa Shilingi milioni 77.20 ambayo ni kidogo ukilinganisha na mapato yaliyokadiriwa katika mpango wa kuhuisha kiwanda ambacho ni Shilingi milioni 500.

Pia tumebaini udhaifu katika ununuaji wa hisa za kiwanda cha kutengeneza matairi General Tyres (EA). Uchambuzi wetu wa mauzo ya kampuni hii umebaini kuwa, bei ya kuuzia iliyokubalika ni Dola za Marekani milioni 1 ambayo ilitakiwa kulipwa kabla ya 30 Julai 2015 kama hakuna riba iliyojilimbikiza. Ukaguzi umebaini kuwa mpaka sasa hakuna hela ambayo imelipwa na serikali.

Tumebaini kuwa TANESCO, shirika halijaweza kutengeneza faida na limekuwa likitengeneza hasara kutokana na gharama za uzalishaji kuwa juu ukilinganisha na bei za kuuzia hususani kwa umeme unaozalishwa na Independent Powe Producers (IPPSs) na Emergency Power Producers (EPPs). Ni maoni yetu kuwa, hasara inazidi kula mtaji wa kampuni kwa kiasi cha kuongeza athari kwenye ukwasi wa shirika na kupunguza ufanisi wa shirika katika

kutimiza majukumu yake, hii pia ina athari katika uwezo wa shirika kukopesheka.

vi. Tathmini na Ufuatiliaji baada ya Ubinafsishaji

Tumegundua kutokuwepo kwa ufuatiliaji unaoridhisha wa ubinafsishaji wa taasisi za umma kiasi kwamba:

Madeni ya kibiashara ya kiasi cha Shilingi milioni 328 chini ya mashirika ya umma yaliyobinafsishwa hayakuingizwa kwenye vitabu vya Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) na kwamba wadaiwa walipelekwa kwenye Shirika la Kukusanya Madeni kwa hatua zaidi baada ya mfilisi kushindwa kuokoa kiasi hicho kutokana na ugumu wa kuwatafuta wadaiwa

Mapato ya ufilisi wa taasisi za umma yaliyokuwa kwenye kumbukumbu za taarifa za fedha zilizokaguliwa za Shirika Hodhi la Mali za Serikali hayahusiani na kiasi kilichopatikana wakati wa kuuza kama inavyoonekana katika taarifa ya taasisi za umma chini ya ufilisi

Ukaguzi ulibaini, Serikali kupitia Wizara husika iliongoza mchakato wa ubinafsishaji wa Kampuni ya Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira na Hoteli ya Kilimanjaro kinyume cha sheria ya Ex-PSRC/CHC. Hatua hii ya Serikali haiafikiani na majukumu ya usimamiaji yaliyoainishwa kwenye mamlaka ya Ex-PSRC/Ex- CHC.

Ukaguzi uligundua mapungufu kwenye udhibiti wa mapato ya kodi za upangaji mathalani majengo matatu ya Ex-Mwanza RTC ambayo hayakuuzwa baada ya ubinafsishaji wa Ex-Mwanza RTC kwenda kwa MZARTC yamekuwa yakikodishwa kwa wapangaji mbalimbali bila ya makubaliano yoyote kati ya Ex- CHC na MZARTC. Sehemu ya mapato ya kukodisha majengo hayo yanatumika kulipa kodi na gharama za matengenezo ya majengo hayo.

CHC haikuwahi kufungua na kuendesha akaunti maalumu kwa ajili ya makusanyo ya madeni hayo kinyume cha kifungu cha 34 (2) cha Sheria ya Mashirika ya Umma Namba 16 ya Mwaka 1993 (kama ilivyorekebishwa).

Kama ilivyoripotiwa katika ripoti yangu ya awali, hisa za Usafiri Dar es Salaam (UDA) ambazo hazikugawiwa ziliuzwa kwa Kampuni ya Simon Group kwa Shilingi 1,142,643,935. Kampuni ya Simon Group ililipa asilimia 24.9 tu ya makubaliano ya bei ya mwanzo (Shilingi milioni 285) katika akaunti ya UDA yenye namba 01J1021393700 katika benki ya CRDB. Hakukuwa na ushahidi wa malipo ya asilimia 75.1 (Shilingi milioni 858) iliyobakia. Mwenyekiti wa UDA alipokea Shilingi milioni 320 katika akaunti yake binafsi kwa ajili ya huduma ya ushauri wa kitaalamu kutoka Simon Group Limited, kiasi ambacho Simon Group alidai kuwa ni sehemu ya malipo ya mauzo ya hisa za UDA

Serikali kupitia Msajili wa Hazina inapaswa kufanya ufuatiliaji wa karibu juu ya ubia wa Serikali katika UDA ili kuhakikisha kuwa maslahi ya umma hayapotei.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA

1.0 Uanzishaji wa Ofisi ya Ukaguzi Kisheria

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni Ofisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara). Ibara ya 143 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008 na kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya Mwaka 2011 inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma angalau mara moja kwa mwaka wa fedha.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ana mamlaka ya kufanya ukaguzi wa hesabu na ukaguzi wa thamani ya fedha au kaguzi nyingine katika Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kama ilivyoainishwa kwenye vifungu Na. 26, 27, 28 na 29 vya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008. Kifungu cha 12 cha Sheria hiyo kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kutoa maoni kwa nia ya:

- Kuzuia au kupunguza matumizi ya fedha za umma yasiyokuwa na tija;
- Kuongeza makusanyo ya maduhuli ya umma;
- Kuzuia hasara inayoweza kutokea kwa uzembe, wizi, kukosa uaminifu, udanganyifu, au rushwa kuhusiana na fedha na rasilimali za umma;
- Kuongeza uchumi, tija na ufanisi katika matumizi ya fedha za umma.

Mashirika na Taasisi Nyingine za umma nchini zinafanya kazi kwa kutumia mifumo ya uhasibu (accrual basis of accounting) ambayo inayalazimu kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IFRSs) au Viwango vya

Kimataifa vya uandaaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSASs). Miongozo zaidi ya kisheria inayotumika kuwandaa hesabu ni pamoja na Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002 au sheria yeyote iliyopitishwa na Bunge ya kuwanzishwa kwa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008

Sheria namba 418 ya Msajili wa Hazina na kifungu cha 6 cha Sheria ya Mashirika ya Umma namba 16 ya mwaka 1992 zinahusiana na majukumu ya Msajili wa Hazina katika Mashirika ya Umma. Sheria hizo zinaelezea kuwa Msajili wa Hazina ana kazi na jukumu la kusimamia vyema uendeshaji wa shughuli za Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa kushirikiana na Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika husika. Vyombo vyote hivyo vinafanya kazi katika kusimamia na kuongoza kwa ukaribu Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa ufanisi na kwa kutoa maelekezo ya kiusimamizi.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha ripoti za mwaka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Katika kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma, ripoti hizo zinatakiwa kuwasilishwa kwa Rais ifikapo tarehe 31 Machi ya kila mwaka. Baada ya kupokea ripoti hizo, Rais atawataka wahusika kuwasilisha ripoti hizo Bungeni ndani ya siku saba tangu kuanza kwa kikao cha kwanza cha Bunge.

Kama Rais hatachukuwa hatua zozote za kuwasilisha taarifa hizo Bungeni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu atawasilisha nakala za ripoti hizo kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano (au Naibu Spika ikiwa kiti cha Spika kiko wazi wakati huo au ikiwa kwa sababu yeyote Spika hawezi kutekeleza majukumu yake) ambaye atawasilisha ripoti hiyo Bungeni. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inayohusu Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma itajadiliwa kwanza na Kamati za Bunge za Hesabu (PAC)

kwa niaba ya Bunge na kuwandaa ripoti ambayo itawasilishwa Bungeni.

1.1 Wigo wa Ukaguzi na Viwango vya Ukaguzi Vinavyotumika

1.1.1 Wigo na Madhumuni ya Ukaguzi

Wigo wa ukaguzi wangu unajumuisha tathmini ya ufanisi wa mifumo ya kihasibu na udhibiti wa ndani katika shughuli za taasisi husika. Pia inahusisha ukaguzi na uhakiki wa hesabu, ripoti za utekelezaji, na taratibu nyingine za kikaguzi ambazo ni muhimu katika kukamilisha ukaguzi. Ukaguzi huu ulifanyika kwa kuzingatia viashiria vya hatari na kiwango cha juu cha miamala kinachokubalika "risk and materiality". Kwa hiyo, matokeo ya ukaguzi yanatokana na kiwango ambacho kumbukumbu, nyaraka, na taarifa zilizoombwa kwa madhumuni ya ukaguzi na zikawasilishwa kwangu.

Madhumuni ya kufanya ukaguzi ni kumuwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serekali kutimiza jukumu la kutoa maoni huru kuhusu hesabu za Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa mwaka 2014/2015 ili kuona iwapo zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu. Ukaguzi huu unahusiana na hesabu zilizokaguliwa kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Septemba, 2014, tarehe 31 Disemba, 2014 na tarehe 30 Juni, 2015.

1.1.2 Viwango vya Ukaguzi Vilivyotumika

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni mwanachama katika Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi Duniani (INTOSAI), Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi za Nchi za Afrika (AFROSAI) na Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi kwa Nchi za Afrika Zinazoongea Kiingereza (AFROSAI-E). Hivyo, Ofisi inatumia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi vya Shirikisho la Ofisi za Taifa za Ukaguzi Duniani (ISSAI) vinavyotolewa na "INTOSAI" na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu (ISA).

1.2 Majukumu ya Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma

Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Mashirika na Taasisi Nyingine za umma zina jukumu la kutayarisha kwa usahihi hesabu kama inavyotakiwa katika Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu (IFRSs) au Viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Hesabu katika Taasisi za Umma (IPSAS). Majukumu hayo yanajumuisha:

- Kuhakikisha taarifa za hesabu zinaandaliwa kwa kiwango cha kimataifa ikiwa ni pamoja na kubuni, kutekeleza, na kudumisha mifumo thabiti ya ndani itakayowezesha kuwandaa mahesabu yaliyo huru, yasiyo na makosa, wala mapungufu yatokanayo na udanganyifu;
- Kuchagua na kutumia sera sahihi za uandaaji wa mahesabu, na
- Kufanya makadirio ya mahesabu yanayoendana na mazingira halisi.

Viwango vya Kimataifa vya Kihasibu (IAS 1) na viwango vya Kitaifa vya Utayarishaji wa Hesabu za Taasisi za Umma (IPSAS 1) vinaainisha aina za hesabu zinazotakiwa kuwandaliwa na taasisi hizi.

1.3 Mpangilio na Uteuzi wa Makampuni Binafsi kwa Kazi ya Ukaguzi

Ili Ofisi yangu iweze kutimiza majukumu ya ukaguzi kwa ufanisi katika Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma nchini, kaguzi za baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma yamekaguliwa na makampuni binafsi ya ukaguzi kwa niaba yangu. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 33 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, ambacho kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kumruhusu mtu au kampuni yeyote iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Wakaguzi wa Hesabu na Wahasibu Na. 33 ya Mwaka 1972 iliyorekebishwa mwaka 1995 kufanya ukaguzi

kwenye Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa niaba yake.

Kulingana na Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, wakaguzi watakaoteuliwa watafuata sheria kama inavyotakiwa na pia hawatatoa siri za mashirika wanayoyakagua. Wajibu wa kutoa hati ya ukaguzi unabaki kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kaguzi zitakazofanywa na Makampuni binafsi zitahakikiwa ubora wa kazi zake na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT).

SURA YA PILI
AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

2.0 Utangulizi

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi Namba 200 (ISA 200), lengo la kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumwezesha Mkaguzi kutoa hati ya ukaguzi inayoeleza iwapo hesabu zinaonyesha hali halisi ya kifedha ya Shirika na kama zimeandaliwa kwa kufuata viwango na mfumo unaokubalika. Ukaguzi wa hesabu unafanyika ili kumuongezea imani mtumiaji wa hesabu husika kwamba zimetengenezwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika, na kumfanya Mkaguzi kupata sababu za uhakika kwamba hesabu kwa ujumla wake hazina makosa na pia kutoa taarifa ya matokeo ya ukaguzi.

Jumla ya maoni ya ukaguzi 125 yalitolewa katika mwaka huu wa fedha, ambapo kati ya hayo, maoni 102 yanahusiana na ukaguzi wa mwaka 2014/2015 na 23 ni yale yanayohusu ukaguzi wa mwaka 2013/2014 kwa taasisi ambazo ripoti zake hazikujumuishwa katika mwaka uliopita.

Ripoti kwa Menejimenti za Taasisi 158, zikijumuisha 23 za mwaka wa fedha 2013/2014, kati ya ripoti za Taasisi 186, zimejumuishwa katika ripoti hii.

Kushindwa kwa Bodi za Wakurugenzi kuridhia taarifa za fedha, uhaba wa fedha uliopelekea kushindwa kufanyika kwa baadhi ya kaguzi kwa taasisi zisizo na uwezo wa kulipa ada ya ukaguzi na mabadiliko ya mfumo wa uandaaji wa hesabu kutoka kwenye Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IFRS) kuelekea katika Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu kwa Taasisi za Umma (IPSAS) ni kati ya masuala yaliyopelekea kuchelewa kukamilishwa kwa ukaguzi wa taasisi 51.

Kiambatanisho Na. 1 kinaonyesha maoni ya ukaguzi yaliyotolewa kwa Mashirika mbalimbali ya Umma katika mwaka wa fedha 2014/2015.

2.1 Aina za Hati za Kaguzi Zilizotolewa

2.1.1 Hati Inayoridhisha

Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu, na vile vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania au viwango vingine vya utoaji wa taarifa za fedha vinavyokubalika kimataifa. Kwa mwaka wa fedha 2014/15, kaguzi 76 za Mashirika ya Umma zilipata hati inayoridhisha.

2.1.2 Hati Yenye Shaka

Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anapokutana na mazingira ya kutokukubaliana na Menejimenti au mazingira yenye shaka ambayo yana athari lakini si za kimsingi katika usahihi wa hesabu. Maelezo ya hati yenye shaka yanafanana sana na hati inayoridhisha lakini aya ya ufafanuzi inaongezwa ili kuelezea sababu zinazoleta shaka.

Hivyo, hati itaonyesha kuwa hesabu kwa ujumla zinaonyesha vizuri uandaaji wa hesabu isipokuwa kwa kasoro zitokanazo na masuala yaliyohojiwa. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kaguzi tatu (3) za Mashirika ya Umma zilipata hati yenye shaka.

2.1.3 Hati Isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha inatolewa pale Mkaguzi anapoona kuwa, taarifa za fedha za Shirika au Taasisi Nyingine za Umma kwa kiasi kikubwa zina makosa, na zikiangaliwa kwa ujumla wake zinakuwa hazikufuata viwango vinavyokubalika vya uandaaji wa hesabu. Hakuna hati isiyoridhisha iliyotolewa kwa shirika lolote kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

2.1.4 Hati Mbaya

Aina hii ya hati ni mojawapo ya sababu zinazoweza kubadilisha hati ya ukaguzi. Hati hii hutolewa pale mkaguzi

anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu hesabu zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo inaathiri hesabu kiasi cha kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kuhusiana na hesabu hizo. Hakuna hati mbaya iliyotolewa kwa shirika lolote.

2.1.4.1 Aya za Msisitizo wa Jambo Kwenye Ripoti ya Mkaguzi

Aya za msisitizo wa jambo hujumuishwa kwenye ripoti ya mkaguzi kwa lengo la kutoa maelezo ya ziada kwa watumiaji wa taarifa za hesabu ili kuvuta umakini wa watumiaji husika kwa jambo ambalo limeoneshwa au kuwainishwa kwenye taarifa ya fedha na ambalo limeonekana ni muhimu na la msingi kwa ajili ya kuleta uelewa wa taarifa hizo kwa ajili ya kufanya maamuzi yenye tija.

Ujumuishaji wa suala lenye msisitizo kwenye ripoti ya mkaguzi hauathiri hati ya ukaguzi iliyotolewa na mkaguzi na si mbadala wa: (a) Hati Isiyoridhisha, Hati yenye shaka na hati mbaya iliyotolewa na mkaguzi pale inapohitajika kutokana na mazingira maalumu ya ukaguzi au (b) masuala ambayo yanaonyeshwa kwenye taarifa ya fedha ambayo Menejimenti ilipaswa kufanya kutokana na mahitaji au matakwa ya mfumo uliokubalika wa uaandaaji wa taarifa za hesabu.

Katika kipindi cha mwaka ninaoripoti, hati zinazoridhisha zipatazo thelathini na tano (35) na hati mbili (2) zenye mashaka zilitolewa kwa Mashirika ya Umma zikiwa na aya msisitizo wa jambo kama ilivyoainishwa kwenye Kiambatanisho Na. I.

Jedwali 1: Hati zilizotolewa kwa kipindi cha miaka minne mfululizo kutoka 2011/2012 hadi 2014/2015.

Aina za Hati	Ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi			
Mwaka wa Fedha	**2011/12**	**2012/13**	**2013/14**	**2014/15**
Hati zinazoridhisha	**85**	**92**	**115***	**99**
Hati zenye shaka	**9**	**1**	**2**	**3**
Hati mbaya	1	0	0	**0**

Hati zisizoridhisha	0	0	0	**0**
Jumla	**95**	**93**	**117**	**102**

*Inajumuisha ripoti 23 ambazo hazikujumuishwa mwaka uliopita.

SURA YA TATU

MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA MIAKA ILIYOPITA

3.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha kwa muhtasari mapendekezo ya Ripoti za Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma kwa miaka iliyopita, ambayo bado hayajatekelezwa au yapo kwenye hatua za utekelezaji hadi ilipofikia wakati wa kuwandaa ripoti hii.

3.1 Majibu ya Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka Uliopita (2013/2014)

Nimepokea majibu ya Serikali ya ripoti ya mwaka uliopita ya Mlipaji Mkuu wa Serikali katika ripoti yake ya mwezi Juni, 2015. Ninapenda kutambua juhudi zilizofanywa na Mlipaji Mkuu wa Serikali katika kujibu masuala na mapendekezo yaliyotolewa kwa Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma. Tathmini ya majibu zimeonyesha kuwa mapendekezo mengi bado hayajatekelezwa na mengine yapo kwenye hatua za utekelezaji. Kwa hali hiyo, hatua za ziada zinahitajika katika utekelezaji wa mapendekezo hayo ili menegimenti za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine ziweze kuwajibika juu ya matumizi ya rasilimali za umma

Ningependa kurejea mapendekezo yote niliyoyatoa katika ripoti zilizopita ambayo hayajatekelezwa au yametekelezwa kwa kiwango kidogo na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi, na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma kama ifuatavyo:

3.2 Mapendekezo ya Mwaka 2008/2009 ambayo Bado Hayajatekelezwa

3.2.1 Haja ya Kuwanzishwa kwa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma

Ni dhahiri kwamba Mashirika na Taasisi Nyingine za Umma zimegubikwa na matatizo mengi, kubwa ikiwa ni ukosefu wa mitaji ya kutosha ambayo ni muhimu kwa maendeleo

katika utelekezaji wa malengo katika mashirika husika. Serikali inapaswa kuwanzisha Mfuko wa Uwekezaji wa Umma ili kuweza kukabiliana na changamoto hizi, Serikali iongeze juhudi katika uanzishwaji wa Mfuko wa uwekezaji wa Umma kama ilivyoahidiwa.

3.2.2 Mkopo wa Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Umma Shilingi Bilioni 51.1 kwa Bodi ya Mikopo

Mkopo wa PSPF Shilingi bilioni 51.1 kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu bado haujarejeshwa kwa zaidi ya miaka 9 sasa. Serikali inapaswa ichukue hatua kuhakikisha kwamba inalipa ya deni lote la mkopo huu (ikiwa ni kiasi cha mkopo na riba) uliokopwa kutoka Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Umma inalipwa, ili kuepuka gharama zaidi za riba na adhabu itokanayo na kuchelewa kulipa mkopo husika.

3.3 Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kwa mwaka 2010/2011

3.3.1 Majengo ya Shirika la Maendeleo ya Taifa Kwenye Kitalu Na.2338 yaliyopo Mbezi Beach, Barabara ya Bagamoyo Hayana Mkataba wa Pango

Nilibaini kuwa Shirika la Maendeleo la Taifa halina mkataba wa pango na mpangaji wa sasa wa jengo hilo, Messrs Vignan Education Foundation (IMTU) baada ya mkataba na Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) kwisha mwezi Agosti, 2011. Vignan Education Foundation limekataa kukubali masharti ya mkataba ulioandaliwa na Shirika la Maendeleo ya Taifa ambao pamoja na mambo mengine una kodi ya mwezi ya Shilingi milioni 60, ambayo ilikadiriwa na mthamini. Nashauri Shirika la Maendeleo ya Taifa iendelee kufuatilia kwa karibu muendelezo wa kesi hii. Serikali iliunda kamati ya ufundi kupitia upya jambo ambalo matokeo yake yamekuwa hayana mafanikio. Kwa hali hiyo bado naendelea kusisitiza mapendekezo yaliyotolewa kwa Shirika la Maendeleo ya Taifa yatekelezwe na suala hili kupatiwa ufumbuzi.

3.3.2 Usimamizi wa Rasilimali za UDOM

Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Umma (PSPF), Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (LAPF), Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Pensheni wa PPF yalitumia jumla ya Shilingi bilioni 415.4 kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), chini ya makubaliano ya buni, jenga, endesha, na kisha hamisha miliki baada ya miaka kumi (10). Majengo haya hayapo kwenye vitabu vya Chuo Kikuu cha Dodoma wala katika vitabu vya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii husika. Japokuwa Mlipaji Mkuu wa Serikali amejibu kuwa majengo haya yataingizwa kwenye vitabu vya Chuo Kikuu cha Dodoma katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, bado UDOM imepewa Hati Yenye Mashaka kutokana na kutokuwepo kwa majengo hayo kwenye vitabu vyake. Hivyo basi, naendelea kusisitiza majengo hayo kuingizwa kwenye vitabu vya UDOM kama nilivyopendekeza awali.

3.4 Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kwa mwaka 2011/2012

3.4.1 Matatizo ya Kifedha katika Shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC)

Shirika la Utangazaji Tanzania limeripotiwa kuwa na hasara kwa miaka mingi mfululizo. Shirika hili lina matatizo ya ukwasi na linaitegemea Serikali kwa kiasi kikubwa katika mahitaji yake ili kujiendesha na kulipia madeni mbalimbali. Hali hii inaleta mashaka na endapo itaendelea kwa kipindi kirefu, Shirika linaweza kushindwa kujiendesha. Nashauri Serikali iongeze mchango wa kibajeti kwa Shirika hili ili liweze kujiendesha.

3.4.2 Usafiri Dar es Salaam (UDA)

3.4.2.1 Uuzwaji wa Hisa za UDA

Bodi ya Wakurugenzi ya UDA iliuza hisa za Shirika hilo bila kupata kibali cha Serikali. Hisa za Shirika la UDA

zilithaminishwa kwa bei ya Shilingi 744.79 kwa kila hisa mwezi Oktoba, 2009, na mwezi Novemba, 2010 thamani ya kila hisa ikawa 656.15. Hata hivyo, katika uuzaji huo, Bodi ya Wakurugenzi ya UDA ilitoa punguzo la asilimia 60 kwa kila hisa kwa mwekezaji huyo (kwa Tathmini ya bei ya hisa ya mwezi Oktoba, 2009), bila kuwepo na sababu za kufanya hivyo. Kwa mujibu wa majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali, Serikali haitambui uuzwaji wa hisa hizo.

Hata hivyo, Serikali inaandaa mapendekezo ya kuuza asilimia 49 ya hisa za UDA na kufikishwa mbele ya Baraza la Mawaziri. Majibu haya hayasemi chochote kuhusu mustakabali wa hisa ambazo zilishauzwa na hatua zilizochukuliwa dhidi ya Bodi ya Wakurugenzi wa UDA. Pendekezo hili halijawahi kutekelezwa kwa sababu hakuna njia yeyote muamala huo ambao haukuwa sahihi ungeweza kupitishwa na Baraza la Mawaziri.

3.4.2.2 Kuthibitishwa Kiasi Kilicholipwa na Mnunuzi

Mkataba wa kuwasilisha hisa wa tarehe 11 Februari, 2011 unaeleza kwamba mnunuzi (mwekezaji) atalipa jumla ya Shilingi bilioni 1.14 kama bei ya ununuzi wa hisa zote ambazo hazijagawiwa na UDA ingawa mkataba haukuonyesha akaunti ya benki ambayo malipo yangefanyika. Mnunuzi (mwekezaji) alilipa kiasi cha Shilingi milioni 285 katika akaunti namba 0J1021393700 ya benki ya CRDB inayomilikiwa na UDA. Hakukuwa na malipo mengine ya ziada yaliyofanywa na mwekezaji kuhusiana na ununuzi wa hisa za UDA. Mwenyekiti wa Bodi alipokea kiasi cha Shilingi milioni 320 kupitia akaunti yake binafsi kutoka kwa Mwekezaji ambayo kwa mujibu wa mwenyekiti huyo ilikuwa ni ada ya ushauri alioutoa kwa Mwekezaji. Malipo haya yalizua mgongano wa kimaslahi. Wakati Serikali haitambui uuzwaji wa hisa za UDA, ninashauri Shirika la UDA lirudishwe chini ya usimamizi wa Serikali hadi hapo mgogoro huu utakapotatuliwa.

3.5 Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kwa mwaka 2012/2013

3.5.1 Mita za Kupima Mafuta Zilizotelekezwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania

Mamlaka ya Bandari Tanzania ilinunua mita kwa ajili ya kudhibiti upimaji wa shehena za mafuta yanayoingia nchini. Mita hizo ziliwekwa kwa ajili matumizi kwenye bandari za Tanga na Dar es Salaam kwa ajili ya kusaidia kudhibiti mapato yanayopotea kutokana na kutokuwa na vifaa vizuri vya kupimia shehena za mafuta zinazoingia nchini. Hata hivyo Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo aliamua vifaa hivyo kusimamishwa kwa madai ya kutokidhi viwango vilivyotakiwa. Hivyo, mamlaka ikaamua kuendelea kutumia njia zisizo za kielektroniki (kwa kutumia kijiti cha kuzamisha) katika kupima shehena za mafuta yanayoingia nchini. Kitendo hicho kina athari kwa mapato ya Mamlaka ya Mapato (TRA) katika uhakiki wa usahihi wa kiasi cha kodi kinacholipwa. Upimaji wa shehena hizo za mafuta bila ya kutumia vifaa stahiki na athari katika uendeshaji wa shughuli za Mamlaka ya Bandari Tanzania.

Ninaendelea kusisitiza matumizi ya mita za kupimia mafuta katika Mamlaka ya Bandari ili kuhakikisha Mamlaka zote (Bandari na TRA) zinakusanya mapato stahiki kulingana na vipimo vilivyo sahihi vya upimaji wa mafuta.

3.5.2 Umiliki wa Benki ya Azania

Benki ya Azania (hapo mwanzo ikiitwa 1st Adili Bancorp Limited) ni benki binafsi iliyoanzishwa mnamo mwaka 1995. Wanahisa wake ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (36%), Mfuko wa Pensheni wa PPF (30%), Mfuko wa Pensheni wa Watumishi Umma (12%), Mfuko wa Pensheni wa LAPF (14%), Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (2.3%), wafanyakazi wa Benki ya Azania na wanahisa wengine (1.4%). Mifuko ya Pensheni kwa pamoja inamiliki asilimia 91 ya hisa zote

katika Benki hiyo. Hii inamaanisha kuwa Mifuko hii ina uwezo wa kuisimamia Benki hii kwa kutoa miongozo na maamuzi muhimu yanayohusu shughuli za uendeshaji. Kwa upande mwingine, Mifuko yote ya Pensheni inamilikiwa na Serikali kupitia Msajili wa Hazina. Kwa kuzingatia uhusiano huu, ni wazi kuwa Benki ya Azania inamilikiwa na Serikali kupitia Mifuko ya Pensheni.

Benki ya Azania inatakiwa iwe chini ya Msajili wa Hazina, Hivyo, kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 9(a) iii na iv cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kinaitaka Benki hii kuwasilisha hesabu kwenye Ofisi yangu kwa ajili ya kukaguliwa.

3.5.3 Ubinafsishaji wa Kiwanda cha Karatasi Mgololo (SPM)

Kiwanda cha Karatasi Mgololo kiliuzwa kwa kampuni ya Rai Group kupitia ubinafsishaji. Mkataba wa mauziano kati ya Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) na kampuni ya Rai group ulitamka kwamba bei iliyokubaliwa ni Dola za Marekani milioni 26 itakayolipwa kama ifuatavyo: Dola za Marekani milioni moja (1) wakati wa kusaini mkataba, Dola za Marekani milioni tatu (3) kuwekwa kwenye akaunti ya scrow na Dola za Marekani milioni ishirini na mbili (22) kutumiwa na mnunuzi (i) kuwekeza katika kampuni katika kipindi cha miaka miwili ya kwanza Dola za Marekani milioni kumi na sita (16.2) na (ii) Dola za Marekani milioni tano (5.8) katika mwaka wa tatu.

Kwa kuzingatia ukweli kwamba Dola Za Marekani milioni tatu (3) zilizowekwa kwenye Akaunti ya Escrow zitarejeshwa kwa mwekezaji na Dola za Marekani milioni ishirini na mbili (22) zitawekezwa katika kiwanda, kiasi kinachobaki ni Dola za Marekani milioni moja (1) tu kuwa bei halisi ya kuuzia mali za SPM. Tuliweza kubaini kuwa hakuna fedha yeyote ya uuzwaji wa mali za Kiwanda cha Karatasi Mgololo kilichoingia serikalini kwavile mapato ya mauzo huwekezwa katika kiwanda hicho. Kiasi cha Dola za

Marekani milioni ishirini na mbili (22) kilichowekwa SPM kama sehemu ya bei ya kuuzia zilitakiwa kuwa sehemu ya uwekezaji wa Serikali katika SPM.

Msajili wa Hazina anatakiwa kufuatilia utekelezaji kwenye ubinafsishaji wa kiwanda hiki kama ilivyoainishwa na kuwahidiwa katika mkataba wa mauziano na Mlipaji Mkuu.

3.5.4 Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo Vijijini (PRIDE Tanzania Limited)

Taasisi ya PRIDE Tanzania ilianzishwa mnamo tarehe 5 Mei, 1993 chini ya Sheria ya Makampuni (CAP 212) kwa dhamana. Madhumuni ya kuwanzishwa kwa chombo hiki ni kutoa mikopo midogomidogo kwa wajasiriamali. Taarifa ya Msajili wa Hazina iliyoonyesha kuwa uwekezaji wa Serikali katika kampuni hii kufikia tarehe 30 Juni, 2008, ilionyesha kuwa hisa zote za PRIDE zinamilikiwa na Serikali.

Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa ya Msajili wa Hazina inayoishia tarehe 30 Juni, 2012, Shirika hili liliondolewa katika orodha ya Mashirika ya Umma. Uhalali na sababu za kuondolewa kwa Shirika hili katika orodha ya Msajili wa Hazina haukuweza kubainika. Kwa mujibu wa kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, kila Shirika la Umma linatakiwa kupeleka hesabu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukaguliwa katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha. Hata hivyo, hesabu za PRIDE Tanzania hazijawahi kuwasilishwa kwenye Ofisi yangu kama inavyotakiwa na sheria.

Pamoja na majibu ya serikali kuwa kampuni imeacha kupata fedha kutoka Serikali ya Kifalme ya Norway na Tanzania mwaka 2005, haijawekwa wazi jinsi hisa za kampuni hii zilivyohamishwa kwenda kwa wamiliki binafsi. Hivyo basi ninaendelea kusisitiza kuwa Msajili wa Hazina anapaswa kufuatilia kwa karibu juu umiliki wa kisheria wa hisa za PRIDE Tanzania zilizokuwa zinamilikiwa na Serikali na baadaye kuwamishiwa kwa wamiliki binafsi.

SURA YA NNE

MASUALA YALIYOPEWA UZITO KATIKA UKAGUZI

4.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha masuala muhimu yaliyojitokeza wakati wa Ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine pamoja na Mapendekezo ya nini kifanyike ili kutoa ufumbuzi wa masuala hayo. Masuala hayo ni kama yanavyooanishwa kwenye sura hii:-

4.1 Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)

4.1.1 Kupungua kwa Ufanisi wa kifedha

Kampuni imekuwa ikiendelea kutengeneza hasara mfululizo mwaka hadi mwaka, hali iliyopelekea iwe na hasara ya jumla ya kiasi cha Shilingi milioni 360,847 kwa mwaka 2014 (mwaka 2013 ikiwa Shilingi milioni 334,480). Hasara hii imechangiwa na uwepo wa vizuizi vya kusambaa kwa mtandao, kutokuwepo kwa tekinolojia ya kisasa, kukosekana kwa ufanisi wa mgawanyo wa masoko, na ukosefu wa fedha za kujikuza kibiashara ikilinganisha na kampuni nyingine za simu.

Kampuni pia ina gawio la muda mrefu ambalo halijalipwa lipatalo Shilingi milioni 503.1 zilizotokana na gawio la Shilingi bilioni 1 zilizoidhinishwa na Bodi ya wakurugenzi mwaka 1999, ambapo kiasi cha Shilingi milioni 469.9 kati ya bilioni 1 pekee ndicho kilicholipwa.

Menejimenti inashauriwa kuwandaa randama ya taarifa kwenda kwenye Bodi ya Wakurugenzi ikiomba ibatilishe maamuzi yake na kuidhinisha kurudishwa kwa gawio la muda mrefu kwenye vitabu vya hesabu.

4.2 Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

4.2.1 Kuwepo kwa Madawa na Vifaa Tiba Zaidi ya Mahitaji Pamoja na Bidhaa za Muda Mrefu Zilizopo Njiani Kufika

Ukaguzi ulibaini kuwa Bohari ya Dawa imekuwa na vifaa tiba aina ya "Gauze absorbent BPC" ambazo zimezidi kiwango kilichopaswa kuwepo pamoja na kwamba Bohari inakabiliwa na upungufu wa kifedha kumudu kununua aina nyingine za madawa. Thamani ya jumla ya vifaatiba hivyo inakadiriwa kufikia Shilingi bilioni 17.19 ambayo ni asilimia 19 ya jumla ya bidhaa zote ilizokuwa nazo kufikia mwisho wa mwaka 2013/2014. Hata hivyo, hapakuwa na uwiano wowote wa kununua vifaa tiba hivi zaidi ya kiwango kinachohitajika kwa mwaka. Vilevile, ilibainika kuwa kuna bidhaa zenye thamani ya Shilingi milioni 295.95 zilizokuwa njiani kwa kati ya siku 10 mpaka siku 341 hali inayoashiria kuwepo kwa mapungufu ya kimfumo kuhusiana na bidhaa zinazokuwa njiani.

Ninaishauri Bohari Kuu ya Dawa kutumia rasilimali chache zilizopo ili kufikia malengo na kuhakikisha kuwa uchunguzi unafanyika kuhusiana na taarifa ya bidhaa au mizigo iliyopo njiani.

4.2.2 Fedha zilizowekwa kama dhamana ya Makontena na Huchukuwa muda mrefu bila kurejeshwa MSD

Bohari Kuu ya Dawa kwa kawaida huweka kiasi cha fedha kwenye Kampuni za Meli zinazojihusisha na usafirishaji majini ikiwa ni dhamana ya makontena na hurejeshewa kiasi hicho pindi wanapoyarudisha makontena hayo kwenye Kampuni husika za usafirishaji. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2015 kiasi cha Shilingi Milioni 536.19 zilikuwa hazijareshwa kutoka kwenye makampuni hayo za usafirishaji ambapo asilimia 67 ya fedha hizo zilikuwa hazijarejeshwa kwa zaidi ya mwaka mmoja. Pia, hapakuwa na uthibitisho wowote juu ya makontena haya iwapo bado yanamilikiwa na Bohari Kuu ya Dawa. Kutokana na hali hiyo, ilikuwa vigumu kubainisha tarehe ya kupokelewa na kurudishwa kwa

makontena hayo, kiasi kilichowekwa kama dhamana na hali halisi ya makontena au mahali yalipo. Bila kuwa na njia bora za kufuatilia taarifa za makontena, inakuwa vigumu kubainisha ni kiasi gani cha pesa hakitaweza kurejeshwa kutokana na muda wa kimkataba wa kurudisha makontena kwisha. Menejimenti inashauriwa kuratibu kwa usahihi uchukuwaji na urejeshaji wa makontena hayo ili kuweza kuzuia upotevu wa dhamana ya fedha zilizowekwa kwenye Kampuni za Usafirishaji majini.

4.3 Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA)

4.3.1 Kutokukaguliwa kwa mizigo ya Chakula yenye Thamani ya Shilingi bilioni 4.64

Mizigo ya chakula yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 2.3 (kwa wastani wa viwango vya ubadilishaji ya fedha wa Benki Kuu ya Tanzania, Shilingi 2,020.35 kwa kila Dola ya Marekani; sawa na Shilingi bilioni 4.64) iliingizwa nchini ndani ya mwaka 2014/2015 bila kukaguliwa. Hali hii ilichangiwa zaidi na bidhaa nyingi kupenyezwa kwenye soko la ndani bila kuhakikiwa ubora na usalama wake kupitia sehemu za kuingilia ambazo hazijaidhinishwa. Pia, ukosefu wa nguvukazi ya kuweza kuwepo muda wote katika njia zote zikiwemo bandari, mipaka ya nchi, na bandari kavu. Serikali inashauriwa kuiruhusu Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania kuwajiri wakaguzi zaidi ili kuweza kustahimili ongezeko la usafirishaji wa mizigo katika sehemu za kuingilia pamoja na kuimarisha ukaguzi katika njia za usambazaji.

4.4 Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF)

4.4.1 Ongezeko la hasara katika thamani (Actuarial) na kutokulipwa kwa deni la Serikali

Ripoti ya Tathmini (Actuarial) ya Mfuko ya mwaka 2014 inaonesha kwamba, Mfuko una hasara ya thamani ya Shilingi trilioni 11.15 (2014: Shilingi trilioni 6.49 kwa mujibu wa tathmini iliyofanyika mwaka 2010). Msingi wa hasara hii ni matokeo ya Serikali kuchelewa kulipa madeni ya mafao ya wanachama waliokuwepo kabla ya

kuwanzishwa kwa Mfuko tarehe 01 Julai 1999. Pia, Mfuko una madai ya mikopo kutoka taasisi za Serikali yenye thamani ya Shilingi bilioni 499.7 kufikia tarehe 30 Juni 2015 (2014: Shilingi bilioni 382.9). Tabia ya ucheleweshwaji wa malipo ya mikopo hii ina athari kubwa kwenye ukwasi wa Mfuko ambapo mwishowe itaathiri utendaji na uwezo wa Mfuko kufikia malengo ya muda mfupi na mrefu ikiwa ni pamoja na malipo ya mafao ya kustaafu kwa wanachama wastaafu.

Serikali inashauriwa kuusadia Mfuko kulipa deni lililobaki hususani kwa Hati Fungani kama inavyopendekezwa. Hii itasaidia uwezo wa Mfuko kufikia majukumu yake yakiwemo mafao kwa wanachama wastaafu. Pia, taasisi zinazohusiana na Serikali zinashauriwa kuweka kipaumbele malipo ya madeni kutoka kwenye Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) ili kuokoa Mfuko katika hatari ya kufilisika.

4.5 Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF)

4.5.1 Hatari za Urejeshaji wa Mikopo iliyotolewa kwa Serikali

Deni ambalo Wizara ya Fedha imelikubali kuhusu mikopo iliotolewa kwa chuo za serikali za mitaa Hombolo na Chuo Kikuu cha Dodoma ni Shilingi bilioni 84.3 kati ya Shilingi bilioni 96.92 ambazo zipo kwenye kumbukumbu za uhasibu. Utofauti wa Shilingi bilioni 12.66 haukutambulika na Wizara ya Fedha. Mikopo mingine iliyotolewa kwa Serikali kupitia Pension Property Limited (PPL), Bunge na Nelson Mandela haikutambuliwa na Wizara ya Fedha hivyo kupelekea kutolipa limbikizo la Shilingi bilioni 10.41.

Menejimenti inashauriwa kuendelea na juhudi za kuifuatilia Serikali ili kuhakikisha kuwa kiasi chote cha mkopo (mtaji pamoja riba) kimelipwa. Pia, Menejimenti ihakikishe usuluhishi wa kumbukumbu unafanyika kwa utofauti wa kiasi cha Shilingi bilioni 12.66 ambazo hazikutambulika na Serikali kwa kuwasilisha vielelezo muhimu Wizara ya Fedha ili deni litambulike.

4.5.2 Ucheleweshaji wa Mkubwa wa Urejeshwajiwa wa Madeni "Treasury Back-Purchase Receivable"

Serikali ilikuwa tayari kutoa Shilingi bilioni 107 ili kuwezesha wanachama wote wa Mfuko waliokuwapo wakati wa kubadilishwa mfuko kutoka "Provident Funds" kwenda Mfuko wa Pensheni (Pension Fund) kufurahia faida za pensheni. Serikali ilikubali kulipa kiasi hicho kwa kipindi cha miaka 10 kinachoishia tarehe 30 Juni 2017. Zaidi ya hapo, mwezi Julai 2010 Serikali ilikubali kulipa riba kwa kiwango cha asilimia 11.08 kwa mwaka kwa deni lililobakia. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, hakukuwa na mzunguko wa kiasi kilichobaki kwa miaka mitano iliyopita na kupelekea kiasi kilichobakia kuwa Shilingi bilioni 75.21.

Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa unatakiwa kujadiliana na Serikali ili kuhakikisha kuwa kiasi kilichobaki kinajumuishwa kwenye thamani ya dhamana ambayo Serikali inatazamia kutoa iwe tayari kulipa kiasi chote kilichobaki kwenye bajeti za mwaka.

4.6 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

4.6.1 Udhaifu kwenye Ukusanyaji Madai

Madai ya Shilingi bilioni 2.4 yalikuwa hayajakusanywa kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja kutoka mashirika binafsi kumi na tano (15). Pamoja na hilo, Mfuko haukuweka riba na faini kwa malipo yaliyocheleweshwa kama Sheria ya Mfuko inavyotaka. Kulingana na Sheria ya Mfuko na mahesabu yaliyofanywa na wakaguzi, Mfuko ulipaswa kutoza riba ya kiasi cha Shilingi bilioni 3.52 inayotokana na ucheleweshwaji wa malipo hayo kwa zaidi ya miezi sita (6). Hatua hizi hazijachukuliwa hivyo kuwepo na uwezekano wa Mfuko kupoteza kiasi hicho cha mapato.

Mfuko unashauriwa kutathmini madai ya tozo hizi za muda mrefu kwa leseni zilizotolewa ili kujihakikishia ukusanyaji wake. Pia napendekeza riba na faini zitozwe kwa madai hayo toka kipindi yalipoanza.

4.7 Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)

4.7.1 Udhaifu kwenye Ukusanyaji wa Madeni ya shilingi bilioni 4.33 Kwa Wanafunzi

Chuo kinadai wanafunzi madeni ya Shilingi bilioni 4.33, kwa mgawanyo wa waliokosa sifa kuendelea na masomo, walioacha chuo na madai yanayohusu Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Madeni hayo hayajalipwa kwa kipindi cha miaka mitatu na hakuna jitihada za kutosha zinazofanywa na Chuo kuyakusanya. Idadi kubwa ya wanafunzi walioorodheshwa kama wadaiwa hawapo tena Chuoni kwa sasa hivyo kuwepo na uwezekano mdogo wa kukusanya madai hayo. Hapo baadaye, Menejimenti ya Chuo inashauriwa kuwanzisha mikakati ya usimamizi wa ukusanyaji wa madai kutoka kwa wanafunzi. Kuhusu madai ya sasa ambayo ukusanyaji wake umeshindikana, Chuo kinashauriwa kuomba kibali kutoka Bodi ya Chuo ili kufuatilia madai hayo.

4.7.2 Malipo ya Mishahara yaliyozidi kiwango Shilingi milioni 206

Kwa kipindi cha miezi tisa (9) kuwanzia Febuari, 2014 hadi Oktoba,2014. Hii inamaanisha Hazina iliidhinisha kiasi cha Shilingi bilioni 7.07 kwenda Chuoni ikiwa ni malipo ya mishahara badala ya malipo stahiki ya Shilingi bilioni 6.87. Hii inamaanisha kulikuwa na malipo ya ziada yaliyofanywa na Hazina ya Shilingi milioni 206 na hakuna marejesho yoyote yaliyofanywa na Chuo kwenda Hazina. Malipo ya ziada yaliyofanywa yanawezekana kutumika katika kazi ambazo hazijapangwa.

Uongozi wa Chuo unapaswa kufanya ulinganishi wa kila mwezi kati ya orodha ya mishahara iliyoandaliwa na Chuo na ile kutoka Hazina na kuwasilisha mapungufu yote yanayojitokeza Hazina. Pia, Uongozi wa Chuo unapaswa kurejesha kiasi kilichozidi Hazina au kutoa ufafanuzi wa matumizi ya kiasi hicho.

4.8 Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)

4.8.1 Dhana na Uchambuzi wa Miradi

Mradi wa majaribio wa nyumba nafuu Kibada ulifanyika bila ya uchambuzi wa mahitaji ambao unalenga mahitaji ya wateja ili kuweza kujenga biashara imara ambayo inajumuisha huduma zinazohitajika na jamii katika mradi huo. Mapungufu ya uandaaji wa mradi ulipelekea kuongezwa kwa huduma za maduka, zahanati, nyumba, barabara na taa za barabarani ambazo hazikuwa kwenye mpango wa awali wa mradi huo. Maamuzi ya kuongeza huduma ambazo hazikupangwa awali ziliongeza gharama za mradi na hivyo kuufanya mradi ukose faida.

Jumla ya gharama ya mradi zilikuwa Shilingi bilioni 9.46 wakati makadirio ya gharama iliyotumika kama kigezo cha kutambua bei ya kuuza ilikuwa shillingi bilioni 7.08. Hili ni ongezeko la asilimia 34 katika gharama ya mradi na hivyo kupunguza kiasi cha faida kwa asilimia 15.

Kutofanya uchambuzi wa masoko kwa undani inaweza kusababisha Shirika kuingia gharama zisizokuwa katika bajeti ambazo zitaathiri faida ya mradi kwa sababu bei haziwezi kubadilika kufikia ngazi ambazo zitaruhusu Shirika kuweza kupata faida iliyotarajia. Menejimenti inashauriwa kufanya uchambuzi wa masoko kabla ya kuwekeza katika mradi wowote ili kufikia malengo ya kupata angalau asilimia 20 ya faida ya uwekezaji kama ilivyoainishwa katika sera za uwekezaji za Shirika la Nyumba la Taifa.

4.8.2 Kushindwa kukusanya mapato kwenye mauzo ya nyumba ndogondogo kiasi cha Shilingi milioni 464

Ukaguzi wetu umebaini uwepo wa kiasi cha Shilingi milioni 464 kutokana na mauzo ya nyumba ndogondogo ambacho hakijakusanywa kwa kipindi cha zaidi ya miezi 24. Pia, tumebaini hakuna hatua za ufuatiliaji zilizochukuliwa na Menejimenti.

Ili kuhakikisha ukusanyaji wa madai, Menejimenti inashauriwa kuongeza mikakati ya ukusanyaji wa madai hayo ili kuongeza uwezo wa kifedha wa Shirika.

4.9 Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

4.9.1 Kiwango cha madai kilichokataliwa na Benki ya Exim

Benki ya Exim inaidaiwa na Mamlaka kiasi cha Dola za Marekani 741,910 ambacho ni sawa na Shilingi bilioni 1.6152. Madeni haya yalitokana na udanganyifu uliofanywa na wafanyakazi wa benki ya Exim kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013. Benki ya Exim ilikubali kulipa kiasi cha Dola za Marekani 333,960 tu pamoja na riba ya asilimia 2.5 ambazo ni sawa na Dola za Marekani 8,349 ambapo baada ya malipo hayo kulibakia salio ya Dola za Marekani 404,950. Kiasi hiki hakikuweza kuthibitishwa na timu ya uchunguzi ya Benki ya Exim. Vilevile, hadi kufikia tarehe 17 Disemba 2015, benki ya Exim iliweza kulipa Mamlaka kiasi cha Dola za Marekani 331,070 badala ya Dola za Marekani 330,960 ambazo Benki ilikubali kulipa, hivyo Dola za Marekani 2,890 hazikulipwa. Deni hilo lililosalia kulipwa na ambalo halijathibitishwa linatia mashaka kwenye urejeshwaji wake na benki ya Exim. Hivyo, tunaishauri Menejimenti ya Mamlaka kuhakikisha inaweka nguvu za kutosha ili kuhakikisha kiasi cha fedha kilichobakia kinakusanywa kutoka Benki ya Exim na ikishindikana hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya Benki ya Exim.

4.9.2 Uwezekano wa Kupotea kwa Mapato kwenye Malipo ya Mikataba ya Upangishwaji

Hoteli, nyumba za kupangisha, na kambi wanailipa Mamlaka tozo kwa ajili ya kuendesha biashara ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Kuna njia mbili za kutoza tozo hizo yaani asilimia 10 ya yanayopatikana kwa kila mteja kwa kwa siku au kiwango kilichokubalika.

Mapitio ya taarifa za Hifadhi yaligundua kwamba Mamlaka imekuwa ikipokea mapato kutoka kwenye mikataba hii ya asilimia 10 kutoka Dola za Marekani 5.66 hadi Dola za Marekani 13.11 kwa kila mteja kutoka kwenye hoteli. Maeneo mengine yenye mahema ya Esirwa na Masek yanalipia Dola za Marekani 25 kwa siku kwa kila mteja kama ilivyo makubaliano.

Kwa kipindi cha ukaguzi huu, tumegundua kwamba, taarifa za wateja wanaolala kwenye hifadhi zinahifadhiwa na kutolewa na wamiliki wa hoteli, nyumba za kupangisha, kambi, na Mamlaka kutokuwa na utaratibu wa kuhakiki usahihi wa taarifa husika. Hivyo, inapelekea Mamlaka kutegemea na kutumia taarifa kutoka kwa wamiliki wa hoteli hizo. Kwa hali hiyo, kuna hatari isiyopingika ya kupotea kwa mapato ya Mamlaka kutokana na Menejimenti ya Hifadhi kutokuwa na uwezo wa kugundua ukamilifu na umakini wa taarifa kutoka kwa wamiliki wa hoteli.

Hatukuweza kubaini ukamilifu wa malipo yote ambayo Hifadhi haikuwa na taarifa za wageni waliolala kwenye hoteli hizo zinafanya kazi zake ndani ya eneo la hifadhi.

Menejimenti ya Hifadhi inashauriwa kuwa na chombo cha kuiwezesha Mamlaka kugundua ukamilifu wa taarifa za wageni wanaolala kwenye hoteli kama zinavyotolewa na wamiliki wa mahoteli hayo. Pia, kuwepo na kiwango maalumu kwenye tozo hizo.

4.10 Shirika la Ranchi za Taifa

4.10.1 Kuvunjwa kwa Mkataba wa Upangishwaji

Shirika la Ranchi za Taifa iliingia mkataba na kampuni ya M/s. Agri Vision Global Limited kwa ajili ya uendelezaji wa Ranchi za Mabale, Kagoma, na Kikukula. Mwekezaji alitakiwa kujenga machinjio (abattoir) eneo la Ranchi ya Mabale. Hata hivyo, machinjio hiyo haikuweza kujengwa kabisa. Kwa maana hiyo, shirika la Ranchi za Taifa ilipata kiasi cha Dola za Marekani 72,881 ambapo ingeweza kupata kiasi cha Dola za Marekani 996,000 kama ilivyo oainshwa kwenye mpango wa kwanza wa biashara katika mkataba endapo machinjio hayo yangejengwa.

Menejimenti ya shirika la Ranchi za Taifa ihakikishe vipengele vyote kuhusu ujenzi wa machinjio Umefuatwa kama ilivyotiwa saini kwenye mkataba ili kuiwezesha kampuni ya Ranchi za Taifa kupata mapato yake kama ilivyokuwa imepangwa ya Dola za Marekani 996,000.

Endapo kampuni haitaweza kukubaliana na vipengele hivi vya mkataba, shirika la Ranchi za Taifa ivunje mkataba huo kutokana na mwekezaji kukiuka vipengele muhimu vya mkataba na hivyo kuleta manufaa hasi kwa kampuni.

4.11 Bodi ya Nyama Tanzania

4.11.1 Ufanisi wa Bodi ya Nyama Tanzania

Kifungu cha 25 cha Sheria ya Nyama ya mwaka 2006, inaeleza moja ya majukumu ya Bodi ni kusaidia maendeleo mbalimbali kwenye sekta ya nyama, ikihusisha huduma, tafiti, mafunzo, maelekezo, maendeleo na kukuza sekta ya nyama na bidhaa zake, matumizi na mauzo nje ya nchi.

Ingawaje Serikali imekuwa ikijitahidi kupunguza uingizwaji wa nyama kutoka nje ya nchi na kujitahidi kuimarisha uuzwaji wa nyama nje ya nchi, bado uingizwaji nyama umeizidi uuzwaji wa nyama nje ya nchi kwa tani 891 kwa kipindi hiki cha ukaguzi. Bodi ya Nyama Tanzania imechangia kufungwa kwa machinjio na kushuka kwa uzalishaji. Bodi ya Nyama Tanzania inashauriwa kupitia upatikanaji ya bidhaa ya nyama kwa ajili ya kuuza nje ya nchi, na pia Bodi ya nyama inashauriwa kupunguza uingizwaji wa bidhaa za nyama kutoka nje ya nchi ili kuwezesha ukuwaji wa sekta ya nyama na maendeleo yake ya kiuchumi hapa nchini.

4.12 Chuo cha Mabaharia cha Dar es Salaam

4.12.1 Hatari ya kupoteza Hadhi ya Jumuiya ya Kimataifa ya Mabaharia

Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Kimataifa ya Mabaharia, na imewekwa katika kundi hilo la hadhi ya jumuiya ya kimataifa ya mabaharia. Ili nchi iingie kwenye hadhi hii inatakiwa iwe mwanachama hai katika kukidhi vigezo vya Jumuiya ya Kimataifa ya Mabaharia. Kigezo muhimu cha Jumuiya ya Kimataifa ya Mabaharia ni mwanachama aweze kukidhi viwango katika elimu, mafunzo na kutunuku vyeti kama inavyotakikana na kanuni za mafunzo na uangalizi za mwaka 1978 na marekebisho

yake ya mwaka 2010 Manila, Ufilipino na inatakikana kukaguliwa na Jumuiya ya Kimataifa ya Mabaharia mara kwa mara.

Katika mwaka husika wa ukaguzi chuo kilikaguliwa na SUMATRA kwa niaba ya Jumuiya ya Kimataifa ya Mabaharia na mapendekezo hayo yakatolewa. Kati ya mapendekezo 25, ni mapendekezo 2 tu (asilimia 8) yaliyoweza kutekelezwa na mapendekezo 23 (asilimia 92) hayakuweza kutekelezwa hali inayotishia kuondolewa katika jumuiya huyo ya kimataifa. Naushauri uongozi wa chuo kutekeleza mapendekezo ya Jumuiya ya Kimataifa ya Mabaharia ili kuepuka kupoteza hadhi hiyo.

4.13 Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingiraya Jiji la Mwanza

4.13.1 Usimamizi wa Mradi wa Ujenzi

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingiraya Jiji la Mwanza ilitoa zabuni ya Awamu ya Pili ya ujenzi wa Makao yake Makuu kwa Kampuni ya DF Mistry (1974). Mradi ulikuwa na gharama ya jumla ya Shilingi bilioni 2.44 pamoja na kodi ya ongezeko la Thamani. Imegundulika kuwa Shilingi milioni 425.47 zimelipwa kwa mkandarasi kwa kutumia hati za malipo Na. 1 na 3 bila hati husika kuthibitishwa na mshauri wa ujenzi. Pamoja kwamba mkandarasi husika hakuweza kukamilisha awamu ya Pili bado aliweza kupewa zabuni ya kuendelea na awamu ya tatu ya ujenzi wa jengo hilo. Awamu ya Tatu ya ujenzi ulikuwa ina gharama ya jumla ya Shilingi milioni 960 ambayo inaundwa na Shilingi milioni 650 zilizolipwa kwa mkandarasi na Shilingi milioni 310 zilizolipwa kwa mshauri ujenzi.

Zaidi ya hapo, gharama za ujenzi wa awamu ya tatu hazikuwepo katika mpango wa manunuzi wa mwaka kinyume cha matakwa ya Sura ya 49 ya Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011 na kanuni yake Na. 69 ya mwaka 2013. Pia stakabadhi ya kielektroniki haikuweza kutolewa kwa malipo

ya Shilingi milioni 605.47 yaliyofanyika kwa ajili ya mradi. Maamuzi ya uongozi ni kinyume na usimamizi bora wa fedha na ilipelekea kuelekeza rasilimali za mamlaka katika matumizi yasiyo rasmi na kuzuia juhudi za serikali katika kukusanya kodi. Menejimenti inashauriwa kufuata sharia, taratibu na kanuni za manunuzi, kodi na usimamizi bora wa pesa. Pia, uchunguzi unatakiwa kufanywa na Bodi ya Wakurugenzi ili kubaini kama kulikuwa na ukiukwaji katika kutoa zabuni kwa mkandarasi husika.

4.14 Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF)-2013/2014

4.14.1 Udhaifu katika Kusimamia Mradi wa Kukopesha Nyumba wa Mtoni Kijichi

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii unatekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba wa Mtoni Kijichi wenye thamani ya Shilingi bilioni 158.50 ambapo kwa mpango wa awali zilipangwa kuuzwa kwa njia ya mikopo ya benki na baadaye kubadilishwa kuwa chini ya usimamizi wa shirika na kukopesha moja kwa moja kwa watu. Katika mfumo wa shirika kukopesha lenyewe, mteja atatakiwa kulipa marejesho kwa kipindi kisichozidi programu sanifu miaka kumi na tano (15). Hata hivyo, imebainika kuwa hakuna programu sanifu Kwa ajili ya kukusanya gharama ya nyumba, taarifa zote zinahifadhiwa kupitia programu ya "Excel Spread sheet".

Hali hii inaliweka shirika katika hatari ya kupoteza kumbukumbu za taarifa na kuingia katika migogoro na wateja wake na wakopaji kama mteja ataamua kwenda mahakamani. Menejimenti inatakiwa kuwangalia hatari ambazo zinaweza kulipata shirika na kuchukuwa hatua stahiki kuzuia uwezekano wa kupoteza taarifa na madhara yake.

4.14.2 Ubia wa Kuendeleza Mji wa Kisasa wa Kigamboni

Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii limeingia ubia na Kampuni ya Azimio Housing Estates kuwanzisha kampuni maalumu kwa jina la Hifadhi Builders Limited. Katika

mkataba huo, Azimio Housing Estates itatakiwa kuendeleza ekari 20,000 za ardhi zilizopo Kigamboni ambapo kwa hatua ya awali itaanza na ekaris 300.

Katika ubia huu, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii inamiliki asilimia 45 ya hisa wakati Azimio Housing Estates inamiliki asilimia 55 ya hisa. Jumla ya gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 653.44 na utaratibu wa uchangiaji mtaji ni kuwa shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii litatoa fedha zenye thamani ya asilimia 45 ya gharama za mradi na azimio itatoa fedha zenye thamani ya asilimia 35 ya gharama za mradi pamoja na ardhi ambayo itathaminishwa kuwa asilimia 20 ya gharama za mradi.

Ukaguzi wa hatimiliki umeonyesha kuwa Azimio Housing Estates inamiliki viwanja viwili, kiwanja chenye hatimiliki Na. 81828 kiwanja chenye ukubwa wa hekta 1.98 na chenye hatimiliki Na. 105091 chenye ukubwa wa hekta 114.11. Viwanja vyote vinapatikana katika eneo la Rasi Dege ambavyo kwa pamoja vilihamishiwa kwa Hifadhi Builders kutoka kwa Azimio Housing Estates kwa ajili ya Awamu ya Kwanza ya mradi. Kwa kutumia kizio cha ekari 2.47 kwa hekta, hatimiliki hizi zitakuwa na ukubwa wa jumla wa ekari 286.74, pungufu ya ekari 13.26 kutoka kwenye ekari 300 ambazo zilipangwa kwa ajili ya Awamu ya Kwanza ya mradi.

Sijaweza kupatiwa hatimiliki za ardhi ambayo Azimio aliahidi kutoa kama uchangiaji wa mtaji. Hivyo imekuwa vigumu kwangu kuthibitisha uwepo wa viwanja hivyo. Kwa kukosekana kwa hatimiliki, umiliki wa ekari 19,700 za ardhi ambazo sehemu ya mtaji wa Azimio Housing Estates kwa asilimia 20, fedha za shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii zinakuwa kwenye hatari ya kupotea.

Menejimenti inashauriwa kuwasiliana na Wizara ya Ardhi ili kuhakiki umiliki wa heka 19,700 za Azimio Housing Estates katika eneo la mradi. Pia, hatimiliki za ekari 13.26

zilizokuwa pungufu kwenye Awamu ya Kwanza ya mradi zinahitajika kuonekana.

4.14.3 Udhaifu katika Mifumo ya Usimamizi wa Taarifa za Kifedha

Katika kukagua Mfumo wa Kihasibu wa Shirika la Hifadhi ya Jamii, imebainika kuwa shirika lina Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Rasilimali ambao unaweza kuunganishwa na Mfumo wa Usimamizi wa Fedha. Hata hivyo, mfumo mkuu unakosa moduli ya uhasibu kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za kifedha. Kwa kukosekana moduli hii, mfuko unatumia "spreadsheet" kwa ajili ya shughuli za kihasibu.

Matumizi ya "spreadsheet" kunafanya taarifa za kihasibu ziwe kwenye hatari ya kukosewa au kupotea hivyo kuleta mashaka juu ya taarifa za kihasibu zinazozalishwa. Shirika linashauriwa kununua na kufunga Moduli ya Uhasibu ya uhakika na yenye ufanisi ambayo itatumika kutoa taarifa za fedha.

4.14.4 Deni la Shilingi bilioni 723.22 ambalo shirika linadai serikali

Shirika la Hifadhi la Taifa ya Jamii limekuwa likikopesha serikali katika miradi yake mbalimbali. Hata hivyo, Serikali imekuwa hailipi madeni yake kwa muda mrefu. Hali hii imesababisha kuongezeka kwa limbikizo la riba na adhabu hadi kufikia asilimia 39 ya salio la deni la Shilingi bilioni 729.22 kufikia tarehe 30 Juni 2014. Katika kikao kilichofanyika tarehe 20 Oktoba 2014, Serikali ilikubali kulibadilisha deni hilo kuwa Hati Fungani. Hata hivyo, maamuzi hayo hayajatekelezwa hadi leo.

Kutokulipwa kwa madeni hayo kunaathiri mtiririko wa fedha wa shirika hivyo kuleta shaka juu ya kukamilika kwa miradi yake mbalimbali. Uongozi unashauriwa kupitia mikakati yake ya ukopeshaji na urejeshaji wa mikopo kwa kuwangalia mbinu mpya kama vile kusitisha mikopo kwa muda na kuifuatilia Wizara ya Fedha juu ya ubadilishaji wa deni hilo kuwa Hati fungani.

4.14.5 Wafanyakazi Walio ondoka Bila Kulipa Madeni yao katika Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii

Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii lina utaratibu wa ndani wa kutoa mikopo kwa wafanyakazi wake. Ukaguzi wa mikopo ya wafanyakazi umeonyesha kiasi cha Shilingi milioni 827.98 bado kinadaiwa kwa wafanyakazi ambao si waajiriwa tena wa NSSF. Menajimenti ya shirika umeweza kuwatambua waajiri wa sasa wa wafanyakazi hao lakini haujaanza kukusanya fedha hizo kutoka kwa waajiri hao hadi muda wa ukaguzi. Hali hii imeonyesha kusababishwa na usimamizi dhaifu katika urejeshaji wa mikopo ambao umesababisha fedha hivyo zisikusanywe na hivyo kupotea kwa rasilimali za Shirika. Menejimenti inashauriwa kutumia njia kali zaidi ili kuwa na ufanisi katika ukusanyaji wa fedha ilizokopesha kwa wafanyakazi.

4.15 Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF)- 2014/15

4.15.1 Utekelezaji wa Mkataba wa Ubia katika Mradi wa Mji wa Kisasa wa Arumeru kati ya NSSF na Azimio Housing Estate Ltd (AHEL)

Kama ilivyoonekana katika mwaka wa fedha uliopita na katika mwaka huu wa fedha, shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii ilianzisha mradi mwingine wa kujenga mji wa kisasa katika Wilaya ya Arumeru mkoa wa Arusha kupitia kampuni iliyoanzishwa kwa ubia na kampuni ya Azimio kwa jina la Hifadhi Builders Ltd

Kifungu cha 5 cha mkataba huo kinaonyesha pande zote zimekubaliana kutoa kiasi cha mtaji unaofikia Dola za Marekani bilioni 3.34 (Shilingi Trilioni 7.2) na ushauri wa kiufundi kwa ajili ya uanzishaji wa mji huo wa kisasa ambapo asilimia 20 (sawa na Dola za Marekani milioni 668.12) imefanywa kuwa thamani ya ardhi ambayo Azimio amekubali kutoa ardhi ya ekari 500 kwa ajili ya uendelezaji wa mradi huo.

Katika ukaguzi imeonekana, shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii limepokea upembuzi yakinifu wa mradi pendekezwa

kutoka Azimio Housing Estate Ltd kupitia barua yake ya tarehe 16 Mei 2013 yenye kumbukumbu Na. AZIMIO/NSSF/ARUMERU/13/5. Ambapo Bodi ya Wadhamini iliidhinisha kuingiza katika ubia ardhi iliyotolewa na kampuni ya Azania katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Mwanza na Arusha kwa ajili ya uwekezaji unaofanana na huu.

Ada ya ushauri kwa ajili ya kubuni mradi huo ni Dola za Marekani milioni 218.09 (Shilingi bilioni 468.9) na ilipangwa Shilingi bilioni 2.4 itumike katika awamu ya upangaji wa mradi. Hata hivyo, kiasi hicho kiliongezwa hadi kufikia Shilingi bilioni 102 bila ya idhini ya Bodi. Kiasi halisi cha ada ya ushauri mpaka kufikia mwisho wa mwaka kilikuwa Dola za Marekani milioni 20.1 (Shilingi bilioni 43.9) kutoka katika Dola za Marekani bilioni 102 za ongezeko.

Tarehe 20 Januari 2016, shirika na kampuni ya Azania walisaini makubaliano ya kusitisha utekelezaji wa mradi huu kwa makubaliano ya pamoja.

Uongozi wa shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii umetoa sababu ya kutokulipwa marejesho ya mikopo yake kutoka kwa Serikali kama sababu ya kusitisha mradi huo. Kama ilivyoainishwa katika makubaliano ya usitishaji, kiasi cha Shilingi bilioni 43.9 ilicholipwa na shirika kama sehemu ya ada ya ushauri ibadilishwe kuwa mkopo ambao utarejeshwa na kampuni ya Azimio kupitia sehemu ya Mauzo ya nyumba katika mradi wa Dege ndani ya miaka mitatu kwa riba ya asilimia 3 kwa mwaka.

Kuingia katika mradi bila kujihakikishia uwepo wa fedha kungeweza kusababisha gharama zisizo za lazima pamoja na matumizi mabaya ya rasilimali kwa upande wa shirika. Uongozi unatakiwa kuhakikisha uwepo wa fedha za kutosha kuendesha mradi uliopangwa kabla ya kuingia katika mkataba. Pia, linapaswa na kuhakikisha kiasi cha Dola za Marekani milioni 20.1 (Shilingi bilioni 43.9) kinarejeshwa katika muda stahiki kwa kuzingatia mabadiliko ya thamani ya fedha kulingana na muda. Pia, kiasi cha riba kinatakiwa

kuwakisi kiasi cha riba kinatakiwa kuwakisi kiasi kinachotozwa na soko.

4.15.2 Malipo yaliyofanywa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii kwa zaidi ya kiasi kilichokubaliwa cha Dola Za Marekani milioni 9.01

Katika mwaka huu wa Ukaguzi imegundulika kuwa mpaka sasa shirika limewekeza kiasi cha Shilingi bilioni 205.14 (makadirio ya Dola za Marekani milioni 123). Kampuni ya Azania imechangia kiasi cha ziada cha Dola za Marekani milioni 5.5 kwenye mradi husika. Makubaliano kati ya pande husika ni kuwa shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii litawekeza mpaka pale thamani ya uwekezaji wao uwe sawa na thamani ya ardhi iliyotolewa na kampuni ya Azania, ndipo pande zote zianze kuchangia katika uwiano ulio sawa. Hii ina maana kuwa shirika la Hifadhi ya Jamii limechangia Dola za marekani milioni 9.01 zaidi ya kiasi kilichotakiwa kuchangia ili kuwa sambamba na vigezo vya makubaliano ya ubia.

Utaratibu dhaifu wa ufuatiliaji wa uchangiaji wa kila mbia ungeweza kusababisha mbia mmoja kuchangia zaidi ya mbia mwingine, wakati mbia aliyechangia kidogo akiendelea kupata mgao wa mauzo ya nyumba kwa mgawanyo ulio katika makubaliano.

Uongozi unashauriwa kuhakikisha uwepo wa ufuatiliaji wa uchangiaji wa kila mbia kwenye mradi. Pia, viwango vya uchangiaji kwa mujibu wa makubaliano vizingatiwe.

4.15.3 Kutolewa kwa Mkopo zaidi ya asilimia 50 ya Thamani ya Mali za SACCOS

Katika kupitia uwekezaji ulio katika mfumo wa mikopo, imegundulika kuwa shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii limetoa kiasi cha mikopo kwa SACCOS tisa kinachozidi asilimia 50 ya thamani ya mali za saccoss husika kinyume na Sera ya kukopesha ya shirika. Upembuzi wa awali wa maombi ya mkopo ulionyesha kuwa SACCOS zimeomba kiasi ambacho hazikustahili. Hata hivyo, ushauri huo ulipuuzwa

na uongozi na maombi ya mkopo kuidhinishwa. Kukosekana Kwa ufanisi katika taratibu za kupitisha mikopo kunaliweka shirika katika hatari ya kutorejeshewa mikopo husika. Uongozi unashauriwa kufuata taratibu na sera zilizoidhinishwa na Bodi ya Wadhamini katika utoaji wa mikopo kwa SACCOS. Mchanganuo wa SACCOS husika umewekwa katika jedwali hapa chini.

Jedwali 2: Mikopo Iliyotolewa zaidi ya Asilimia 50 ya Thamani ya Mali za SACCOS

Na.	JINA LA SACCOS	50% YA MALI (Shilingi)	KIASI KILICHOTOLEWA (Shilingi)	ZIADA ILIYOTOLEWA (Shilingi)	% YA ZIADA
1	Bumbuli Development Corporation	51,043,808	1,000,000,000	948,956,192	1859%
2	Korongo Amcos Saccos	18,369,360	500,000,000	481,630,640	2621.92%
3	UMMA Saccos	6,531,000	70,000,000	63,469,000	972%
4	SBC Saccos Ltd	115,229,745	500,000,000	384,770,255	334%
5	Hekima Saccos	32,117,967	71,900,000	39,782,033	124%
6	Ukombozi Saccos Ltd	302,902,754	440,000,000	137,097,246	45%
7	Uzinza Saccos Ltd	80,943,104	150,000,000	69,056,896	85%
8	Harbour Saccos	193,000,000	200,000,000	7,000,000	4%
9	Umoja Saccos	247,651,403	300,000,000	52,348,597	21%

4.16 Bodi ya Pamba Tanzania

4.16.1 Kutofikiwa kwa Malengo ya Miaka 2011 - 2015

Bodi ya Pamba Tanzania imejiwekea malengo katika mpango mkakati wake wa miaka mitano, 2011 – 2015. Malengo yalikuwa na dhumuni la kuongeza uzalishaji wa zao la pamba kutoka kilo 750 kwa hekta moja mpaka kilo 1000 kwa hekta moja kufikia mwaka 2015. Ingawa mazao yamebakia kilo 750 kwa hekta kwa miaka mitano mfululizo, pia TCB imepanga kuongeza uzalishaji wa pamba kitaifa kutoka kiwango cha marobota 700,000 hadi marobota

1,500,000 kufikia mwaka 2015. Hata hivyo, kwa miaka mitano iliyopita, uzalishaji kitaifa umekuwa chini ya marobota 700,000. Ni marobota 282,809 tu yalizalishwa katika mwaka 2015. Pamoja na hayo, Bodi ilitakiwa kuboresha mfumo wa masoko kwa kuongeza thamani katika mazao na kuwahamasisha wawekezaji wa nje na wa ndani kuwekeza katika sekta ya pamba.

Hata hivyo, malengo haya yote hayakuweza kufikiwa. Bodi inashauriwa kupitia mpango mkakati wake na kuweka juhudi katika kutatua mkosa vilivyopelekea kushindwa kufikiwa malengo yaliyowekwa katika kipindi kilichopangwa kwa mujibu wa mpango mkakati.

4.17 Kampuni ya Nyumba za Watumishi

4.17.1 Utekelezaji wa Sera Muhimu Kucheleweshwa na Serikali na Kampuni ya Nyumba za Watumishi

Kifungu cha 9.0 cha wazo la uanzishaji wa mpango wa Kampuni ya Nyumba za Watumishi kinaelezea sera za kukabiliana na nguvu ya soko kwa nyumba zilizojengwa ili watumishi wa umma waweze kuimudu bei zake. Hata hivyo, serikali bado haijaanza kuzifanyia kazi sera muhimu ikiwemo kuondolewa kwa kodi ya ongezeko la thamani kwa nyumba mpya zitakazouzwa; serikali za Mtaa kutoa ardhi ya bure inapowezekana; kuwekewa miundombinu na huduma muhimu za kijamii kupitia wakala wa huduma na Serikali za Mitaa (hii inachangia karibu asilimia 20 ya gharama za ujenzi) ;na mwisho kutoa motisha ya kodi kwa wafanyakazi kwa kuruhusu makato ya mkopo wa nyumba kutolewa katika mshahara kabla ya tozo ya kodi ya lipa kadri unavyopata (P.A.Y.E)

Utekelezaji wa sera hizi utazifanya gharama za nyumba zilizojengwa kuwa nafuu kwa watumishi wa umma. Serikali inashauriwa kuanza kutekeleza hatua za kisera zilizopendekezwa kukabiliana na nguvu ya soko ili kuzifanya nyumba zitakazojengwa na Kampuni ya Nyumba za Watumishi kuwa za bei nafuu.

4.17.2 Ucheleweshaji wa Utekelezaji wa Shughuli Zilizopangwa

Kampuni ya Nyumba za Watumishi ilikuwa na mpango wa kujenga nyumba 2,500 kufikia Juni 2015. Hata hivyo, hakuna nyumba hata moja iliyokamilishwa kufikia Juni 2015 kutokana na kuchelewa kwa taratibu za manunuzi. Ucheleweshaji huu umesababisha kutofikiwa kwa lengo kuu la kampuni la kuwawezesha watumishi wa umma kumiliki nyumba bora kwa njia ya mkopo kupitia utaratibu mzuri wa uendelezaji wa majengo.

Uongozi unashauriwa kuchukuwa hatua madhubuti kuhakikisha shughuli zilizopangwa zinatekelezwa ndani ya muda ili kuhakikisha kampuni inafikia malengo yake ya kimkakati.

4.18 Hospitali ya Taifa Muhimbili

4.18.1 Madawa na vifaatiba ambavyo havijapokewa kwa muda mrefu kutoka Bohari Kuu ya Madawa vyenye Thamani ya Shilingi bilioni 2.03

Ukaguzi umebaini kuwa madawa na vifaatiba vyenye thamani ya Shilingi bilioni 2.03 havijafika Hospitali ya Taifa Muhimbili tangu Mei 2012 licha ya kuonekana kwenye ankara 23 za Bohari Kuu ya Madawa. Kwa hali ya kawaida haikutarajiwa bidhaa hizi kuchukuwa zaidi ya wiki moja kufikishwa sehemu husika ukizingatia ofisi za Bohari Kuu ya Madawa na Hospitali ya Taifa Muhimbili zote ziko Dar es Salaam. Hali hii inaashiria uwezekano wa upotevu wa madawa na vifaatiba pasipo uongozi kuwa na taarifa. Menejimenti inashauriwa kuchunguza jambo hili ili kubaini kama kweli bidhaa hizo bado zipo safarini.

4.19 Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania

4.19.1 Kufilisika kwa Msambazaji na Kukosekana kwa Uhakika wa Kukamilika kwa Miradi Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 7.10.

Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania ilikuwa na mikataba mitatu na kampuni ya COMSOFT Gmbh yenye thamani ya Shilingi bilioni 7.10 kwa ajili ya zabuni tatu za mfumo wa

malipo ya ankara, ADSB awamu 1 na ADSB awamu ya 2. Mikataba miwili ilisainiwa na mmoja haukusainiwa kutokana na ya kutokukamilika kwa majadiliano. Mapungufu yafuatayo yamebainishwa:-

Msambazaji alitangaza kufilisika hivyo mradi wa ADS-B awamu ya 1 uliotarajiwa kumalizika Octoba 2013 haukuweza kukamilika kwa wakati hadi Novemba 2015. Pia, mfumo wa malipo ya ankara uliotakiwa kukamilika mwezi Septemba 2015 hadi November 2015 mkataba wake ulikuwa katika hatua ya usanifu. Gharama za ADS-B awamu 1 na AMHS kama ilivyodhinishwa katika mpango wa manunuzi zilikuwa Shilingi bilioni 1.02 (yuro 422,525) lakini mkataba huo ulisainiwa kwa thamani ya Shilingi billion 3.81 (yuro 1,580,000) bila idhini ya bodi.

Pia, mfumo wa ADS-B haukuunganishwa na mtandao wa intaneti. Kabrasha la zabuni lililowasilishwa na kampuni ya COMFORT Gmbh liliondolewa baadhi ya vipengele kama vile moja ya udhibiti wa ndani na mfumo wa ufuatiliaji – LCMS kipakatarishi katika kila kituo cha ADS-B kuonyesha ujumuisho wa nafasi nane (8) za udhibiti. Kwa sababu zisizojulikana, timu ya kutathmini haikuweza kubaini mapungufu hayo. Iwapo timu hii ya kutathmini ingebaini mapungufu hayo kwenye kampuni ya COMSOFT GmbH isingeweza kushinda zabuni. Wakati wa usainishaji wa mkataba ni vipengele vitatu (3) tu ndivyo walivyokubaliana kati ya vitano (5) kama ilivyoainishwa kwenye rasimu ya mkataba.

Kuna uwezekano mkubwa wa kutokukamilishwa kwa miradi inayotekelezwa na Kampuni ya COMSOFT GmbH. Kulingana na mapungufu yaliyoonekana kwenye mkataba, hata kama wasimamizi au wanunuzi wapya wa COMSOFT GmbH watatekeleza masharti kama ilivyooneshwa kwenye mkataba huo. Kukosekana kwa baadhi ya vipengele kama

ilivyoainishwa hapo juu, watumiaji wa ADS-B hawatakuwa kwenye nafasi ya kutumia kwa kiwango kilichokusudiwa.

Menejimenti ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania inashauriwa kuchunguza Kwa kina uwezo wa sasa wa kifedha na kiutendaji wa kampuni ya COMSOFT GmbH. Hivyo, itahitaji uhusishwaji wa ubalozi ya Tanzania nchini Ujerumani kwa ajili ya kupata taarifa sahihi na za uhakika. Pia uongozi utahitaji kupata dhamana ya benki kutoka kwa kampuni ya COMSOFT. Pamoja na hilo, Uongozi unatakiwa kuwangalia jinsi ya kupata fidia kutokana na ucheleweshwaji uliyosababishwa na mzabuni huyo. Zaidi ya hayo, Serikali inashauriwa kuingilia kati uwekezaji katika vifaa vya mifumo ya udhibiti wa usafiri wa anga. Pia tunashauri kadri iwezekanavyo kuendelea kufanya kazi moja kwa moja na watengenezaji kwa ajili ya ununuaji na uwekaji wa mifumo ya uangalizi.

4.20 Mamlaka ya Bandari Tanzania

4.20.1 Upotevu wa kumbukumbu za Hesabu za Meli kwenye Vitabu vya Mamlaka

Katika ukaguzi wa mapato uliofanyika, ilibainika kati ya meli 1253 zilizotiwa nanga katika bandari, meli 145 hazikuonekana kwenye mfumo wa mapato. Kati ya meli hizi ambazo hazikuonekana kwenye mfumo, uongozi umeweza kutoa maelezo na viambatisho vya meli 60 tu, na meli 85 hazikuwemo kwenye mfumo wa mapato.

Kuna hatari ya mapato yatokanayo na meli kutumika vibaya. Uongozi unatakiwa kufanya uchunguzi wa kina kujua meli hizi zilipo. Kufanyike mapitio ya ziada kwenye meli zote ambazo hazina viambatisho na kutambua kama mapato husika yalikusanywa na kuwekwa kwenye kumbukumbu.

4.20.2 Utofauti wa kumbukumbu kati ya bidhaa zilizowekwa kwenye mfumo wa Mamlaka ya Bandari na zile za kwenye Mfumo wa Mamlaka ya mapato Tanzania kwa mwezi Disemba mwaka 2014

Katika mapitio ya shehena za mizigo iliyopokelewa mwezi Disemba 2014 kulikuwa na tofauti mbalimbali za kumbukumbu kati ya jumla ya bidhaa kwenye mfumo wa TANCIS na mfumo wa CMS kama ilivyoainishwa kwenye jedwali lifuatalo:

Jedwali 3: Utofauti wa kumbukumbu kati ya bidhaa zilizo katika mfumo wa Mamlaka ya bandari na mfumo wa Mamlaka ya Mapato

Jumla ya Meli – 89	Mizigo kwenye CMS	Mizigo kwenye TANCIS	Mizigo kwenye TICTS	Utofauti
Mizigo kwenye meli 56, ambayo ilionekana pande zote mbili (Mamlaka ya Mapato na Mamlaka ya Bandari)	22,252	22,395	-	-143
Meli 15 ambazo hazikuwa na mizigo ndani yake, iliyoonekana pande zote mbili(Mamlaka ya mapato na Mamlaka ya bandari)	-	-	-	-
Mizigo kwenye meli 12 iliyoonekana kwenye CMS,TICTS na TANCIS	4,726**	5,557	5,868	311
Mizigo kwenye meli 2 ambayo imeonekana kwenye TANCIS na TICTS	-	91	74	17
Mizigo kwenye meli 4 ambayo imeonekana kwenye CMS tu na haijaonekana TANCIS	1,557	-	-	1,557
Jumla	**23,809**	**28,043**	**5,942**	**1742**

**Mizigo hii iliripotiwa TICS na pia ilikuwa inatunzwa na kituo cha Huduma za makontena ya kimataifa lakini baadae ikahamishiwa Bandari kavu. Utofauti uliojitokeza unamaanisha hakukuwa na kumbukumbu sahihi ya mapato kama inavyoonesha hapa chini:

- Shehena yenye bidhaa 143, kumbukumbu inaonesha kuwa na utofauti wa kiasi kidogo kupokelewa kwenye mfumo wa CMS kuliko kiasi kilichotolewa TANCIS. Hii inamaanisha kuwa Mamlaka ya Bandari haikurekodi mapato kwenye mizigo hii;

- Shehena yenye bidhaa 311; Kumbukumbu zinaonesha kuwa shehena nyingi zinaonekana kwenye mfumo wa TICTS kuliko shehena zilizotolewa na Mamlaka ya mapato. Hii inaonyesha kuwa Mamlaka ya Mapato haikuweka tozo kwenye mizigo hii.

- Shehena yenye bidhaa 17; Kumbukumbu zinaonesha kiasi kidogo cha mizigo kilionekana katika mfumo wa TICTS kuliko mizigo iliyo tolewa na TANCIS. Hii inamaansha Mamlaka ya bandari haikurekodi mapato yoyote kwenye mizigo hii.

- Shehena yenye bidhaa 1,557; Hii inamanisha mizigo ambayo ilijumuishwa na Mamlaka ya Bandari lakini haikuwepo kwenye kumbukumbu za Mamlaka ya Mapato. Hii inatafsiri kuwa Mamlaka ya Mapato haikuweka tozo kwenye mizigo hii.

- Meli 15; Inamaanisha kuna uwezekano mkubwa Mamlaka ya Bandari na Mamlaka ya Mapato kuwa hazikupata mapato ya mizigo iliyokuwepo kwenye meli hizi.

Kuna hatari ya kutumia vibaya mapato yatokanayo na meli. Uongozi unatakiwa kupitia mizigo yote iliyopokelewa kwenye mifumo yote ili kuhakikisha kunakuwa na kumbukumbu sahihi za mapato. Uongozi unatakiwa kuwandaa usimamizi mzuri wa mizigo inayopokelewa bandarini na uwekaji wa kumbukumbu sahihi kwa huduma zinazotolewa na bandari. Uboreshaji wa huduma hizi unajumuisha vitu vifuatavyo:

i. Utaratibu wa ulinganifu wa hesabu unatakiwa kufanyika kielectroniki na vifaa kama kompyuta za mkononi zinatakiwa zitumike kwa ufasaha.
ii. TANCIS na CMS zinatakiwa kuboreshwa/kubadilishwa haraka ili kuendana na kumbukumbu za hesabu za kutali.
iii. Usawazishaji wa taarifa kati ya zile za tali, CMS na TANCIS unatakiwa ufanyike mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa idadi ya mizigo inayopokelewa ni sawa na ile iliyo katika mifumo yote.
iv. Kwa kuwa ni mchakato wenye uwezekano mkubwa wa athari, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kinatakiwa mara kwa mara kupitia taratibu za udhibiti ili kupunguza kasoro.

4.20.3 Udhibiti Hafifu wa Mapokezi ya Bidhaa Bandarini

Kuhakikisha kuna ukamilishaji wa hesabu za mapato; bidhaa zinazopokelewa bandarini zinahesabiwa na kitengo cha tali katika idara ya uendeshaji na matokeo ya hesabu yanahifadhiwa katika karatasi za tali. Kupitia mchakato huu, kumbukumbu za bidhaa zilizozidi au kupungua idadi ya bidhaa zilizopokelewa zinakusanywa pamoja. Hata hivyo, hakukuwa na ulinganishaji kati ya karatasi za tali na mfumo wa mapato wa mamlaka (CMS). Matokeo yake, tumegundua kiasi kikubwa cha bidhaa ambazo zilikuwa katika karatasi za tali hazikuwandikwa kwenye mfumo wa CMS. Angalia kiambatisho namba II

Pamoja na ukweli kuwa kitengo cha Mahesabu cha tali kinapewa vifaa aina ya kompyuta za Mkononi ambazo vimeunganishwa na mfumo wa mapato wa mamlaka kwa ajili ya kujumlishwa. Kompyuta za mkononi hazitumiki muda wote kama ilivyokusudiwa, itashindwa kufuatilia bidhaa zilizopokelewa na kuhudumiwa bandarini na kupelekea kupoteza mapato.

4.20.4 Mapungufu katika Kuongoza na Kuruhusu Meli katika Bandari Dar es Salaam

Ukaguzi ulibaini kuwa kati ya meli zilizoruhusiwa kwa miezi Septemba na Oktoba 2014, meli mbili ziliruhusiwa kuondoka na mfanyakazi ambaye si wa Idara ya Mapato, Kitengo cha Baharini na meli nyingine moja iliruhusiwa kuondoka na mfanyakazi wa kitengo hicho cha baharini bila kutarifu Idara ya Mapato, kitengo cha Tathmmini ya tozo. Utaratibu wa Mamlaka ya Bandari unataka meli ziwe zinaruhusiwa na Kitengo cha Mapato cha Baharini baada ya kukitaarifu kitengo cha tozo. Meli hizo pia zilikosekana katika kumbukumbu za TANCIS kwenye Mamlaka ya Mapato. Ifuatayo ni orodha ya meli hizo:

NAMBA YA UITO	JINA LA MELI	TAREHE YA KUFIKA	MUDA	TAREHE YA KUONDOKA	MUDA
5566	MORNING CORNET	10-Sep-14	14:41	10-Oct-14	18:00
5480	JPO SCORPIUS	22-Sep-14	10:35	25-Sep-14	11:28
5547	COMMODORE	12-Oct-14	12:45	13-Oct-14	14:12

Uongozi (Meneja wa Mapato) alithibitisha kuwa Meli hizo ziliruhusiwa kinyume cha utaratibu na maofisa wafuatao:

NAMBA YA UITO	JINA LA MELI	Jina la Ofisa	Kitengo
5566	MORNING CORNET	Said Milanzi	Marine section
5480	JPO SCORPIUS	Michael Msanga	Operation Clerk 'C'
5547	COMMODORE	Michael Msanga	Operation Clerk 'C'

Hali hii huenda inapelekea kuongezeka kwa viashiria vya hatari ya upotevu wa mapato kwa mashirika yote yaani TPA na TRA. Uongozi unatakiwa kuhakikisha kuwa maofisa husika wanachukuliwa hatua kwa kufanya kinyume na mamlaka yao. Kwa wakati ujao uongozi unatakiwa uhakikishe kwamba hatua madhubuti zinafuatwa. Mamlaka ya mapato na Mamlaka ya Bandari wanatakiwa kufanya uchunguzi wa upotevu wa mapato kutoka katika meli husika.

4.20.5 Mapungufu Kwenye Ukusanyaji wa Mapato ya Bandari

Wateja wa Mamlaka ya Bandari wanatakiwa kulipa tozo moja kwa moja kupitia akaunti za benki ya Mamlaka kwa

kuzingatia Ankara iliyotolewa na kitengo cha tozo. Baada ya malipo hayo, wateja wanatakiwa kupeleka hati ya kuweka fedha kwa ajili ya kuthibitisha kabla ya mizigo kutolewa. Mapitio yetu yameonyesha kuwa hati za madai 3,278 zilizotolewa mwezi wa Desemba 2014, hazikuweza kuwiana na malipo yaliyofanyika kwenye akaunti yoyote ya benki au kuwepo kwenye akaunti ya madeni (receivables) ya mamlaka hiyo mwisho wa mwaka.

Kuna hatari ya mamlaka kuwa fedha zake zinapotea. Hivyo mamlaka inatakiwa kufanya mapitio ya hati zote kwa kulinganisha na mapato yaliyokusanywa na kudai hati ambazo hazikulipwa kutoka kwa wateja.

4.20.6 Mapungufu yaliyobainika kwenye mapato yaliyoingizwa kwenye hesabu(General Ledger) za mamlaka

Ukaguzi wa taarifa za mapato yaliyoingizwa kwenye hesabu za mamlaka ulibaini mapungufu yafuatayo;

i. Hakuna taratibu za kuhakikisha mapato yote yaliyopatikana kupitia Bandari Kavu na Sehemu ya kuhifadhiwa magari yanazingatiwa vyema kwenye vitabu vya kutunzia miamala ya fedha (General ledger) ya mamlaka. Matokeo yake kwenye sampuli ya mizigo 130 vilivochaguliwa kufanyiwa ukaguzi tulibaini kuwa kuwa mizigo 9 ilitolewa bila kutolewa Ankara ya malipo. Pia tulibaini sampuli ya makontena 6 na magari 3 yaliyopelekwa bandari kavu (ICD'S) na Sehemu ya kuhifadhia mizigo kwa mwaka wa fedha (2014/2015) yalikabidhiwa kwa watu husika bila kulipiwa.

ii. Tathimini juu ya viwango mbalimbali kwenye mfumo wa utozaji kodi umebaini mapungufu yafatayo:

(a) Utumiaji wa kiwango cha chini cha ada ya kuongoza Meli chenye makosa

Tumebaini kiwango cha chini cha ada ya Pilotage kilichotumika kilikuwa ni Dola za Marekani 55 badala ya Dola za Marekani 150 ambazo zipo kwa mujibu wa mwongozo wa tozo wa April 2013. Baada ya ufatiliaji

wa kina nilibaini ya kuwa Dola za Marekani 150 ilikuwa inakiukwa kwa makusudi na kutoza dola za kimarekiani 55.

(b) Ukokotoaji wa gharama za utunzaji mizigo wenye makosa

Tumebaini kuwa menejimenti ilitumia taarifa zisizo sahihi pale ilipokuwa ikikokotoa siku ambazo mizigo ilikaa bandarini zaidi ya kipindi cha msamaha. Makosa hayo yalipelekea kuripoti mapato ya utunzaji wa mizigo pungufu kwa Dola za Marekani 15,865. Taarifa hizi zilitokana na sampuli ndogo iliyochaguliwa kufanyiwa ukaguzi.

i. Miamala ya mapato kutokana na baadhi ya sampuli niliyoichagua haikuwa na viambatisho sawia.

ii. Kukosekana kwa usawazishwaji wa usimamizi wa mapato yaliyopatikana kwenye kipindi cha ukaguzi wa mwaka. Kwa mfano, nilibaini kuwepo kwa makosa ya kihesabu kwenye mapato yaliyoingizwa kwenye mchanganuo wa taarifa za mamlaka hali iliyopelekea mapato hayo kuwa chini kwa upungufu wa Shilingi bilioni 1.1.

Tofauti ya mapato yaliyorekodiwa yalitokana na Ankara (invoices) 309 (100 za uingizaji,24 kuuza nje na 185 za MPS) zilizojumlishwa kimakosa na kutoa mapato ya jumla ya kiasi cha Dola za Marekani 675,451 badala ya kiasi cha Dola za Marekani 1,330,645. Pia mapato ya mrahaba wa magari yanayochajiwa kwenye "CFS" yalionyeshwa pungufu kutokana na gharama zilizotumika kukokotoa mrahaba kutokuwa sahihi.

i. Kutokufanyika kwa usuluhishi wa "credit notes" zilizotolewa kwenye rekodi ya mapato ("revenue journal") na taarifa zilizopo kwenye mfumo wa utozaji (billing systems records). Kwa mfano, baadhi ya "credit

notes” hazikusahihishwa kwa kipindi husika wakati baadhi haziendani na rekodi za mfumo ulipo.

Menejimenti inatakiwa kuhakikisha viwango vilivyomo kwenye mfumo wa utozaji ni ule ulioidhinishwa kama inavyooneshwa kwenye mwongozo wa tozo ya Aprili, 2013. Pia Menejimenti inatakiwa kufanya uchunguzi katika mapungufu yaliyotokea na kuchukuwa hatua stahiki kwa maofisa waliosababisha mapungufu hayo

4.20.7 Kukosekana kwa nyaraka zenye utaratibu wakudhibiti matumizi ya simu (HVP na CMS)

Tathmini yangu katika utaratibu wa kuthibiti meli zinazotia nanga katika bandari ya Dar es salaam kwa ajili ya mizigo ya kawaida ,magari na makontena ilionyesha kuwa, hakukuwa na nyaraka rasmi ambazo zipo kimaandishi zinazoelezea utaratibu wa kufuatwa na udhibiti kuwanzia wakati ambao wakala wa kampuni za meli hupiga simu kwenye “HVP” mpaka kipindi ambacho meli inakuwa imekwishahudumiwa. Aidha, hakuna tathmini ya uwazi kuthibitisha kwamba taratibu zote zilizingatiwa.

Kukosekana kwa nyaraka zenye utaratibu wa kimaandishi inapelekea kutokuwepo kwa mpangilio na udhibiti mzuri. Uongozi unatakiwa uandae mwongozo wa kimaandishi kushughulikia taratibu za kuratibu mizigo.

4.21 Benki ya Maendeleo ya TIB

4.21.1 Urejeshaji Usioridhisha wa mkopo wa Kilimo uliotolewa kwa Viwanda Vya SAAFI na ECGS

Benki ya Maendeleo ya TIB ilipewa jukumu la kuendesha shughuli za kifedha na masuala ya kitendaji katika kiwanda cha SAAFI ili kuwezesha ulipaji wa mikopo ya awali liyotolewa na Serikali. Baadae, Serikali ilitaka Benki ya TIB kuipatia mkopo kiwanda cha SAAFI. Benki ilitoa kiasi cha Shilingi bilioni 2.5. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2014 hakuna fedha iliyolipwa.

Benki iliamua kugeuza mkopo kuwa hisa baada ya kuona utendaji wa SAAFI hauridhishi.

Menejimenti ya benki ilikadiria thamani ya uwekezaji wa Shilingi bilioni 1 na kutoa upotevu wa thamani wa Shilingi bilioni 1.5 (provision for impairment). Hata hivyo, TIB haikuwa na ushahidi wowote kuhusu thamani ya hisa zake kwa SAAFI.

Pia, Katika kupitia taarifa za benki ilionekana kiwanda cha SAAFI kilikuwa kinadaiwa na Serikali kupitia Export Credit Guarantee Scheme (ECGS) kiasi cha Shilingi bilioni 14.95. Serikali ilitoa mamlaka kwa benki ya TIB kusimamia shughuli za kiwanda cha SAAFI. Deni hili limekuwepo kwa zaidi ya miaka 10 bila kulipwa.

Aidha, kampuni 5 pia zilikuwa na deni kupitia mfuko wa usafirishaji nje (ECGS) lenye thamani ya Shilingi 45,712,589,000 ambalo nalo limekuwepo zaidi ya miaka 10 bila kulipwa na bila kufungwa kwa makampuni hayo kama inavyooneshwa hapo chini.

Makampuni	**Shilingi '000**
Nyenzo za kifedha	
Arusha Blooms Ltd	2,614,000
Nyenzo za kifedha zilizorekebishwa	
Kiliflora Ltd	11,813,123
Arusha Blooms Ltd	7,500,000
Tengeru Flowers Ltd	7,500,000
Mount Meru Flowers	16,285,466

Urejeshaji wa mikopo hiyo si wa kuridhisha. Hivyo, Menejimenti inatakiwa kuimarisha usimamizi wa madeni ili kuhakikisha malengo ya Serikali ya kukuza kilimo yanafikiwa.

4.21.2 Madeni ya muda mrefu ya kilimo kwanza (Agricultural Financing Window)

Mnamo tarehe 31 Disemba, 2014 wadaiwa wa dirisha la mikopo ya miradi ya kilimo walikuwa kiasi cha Shilingi bilioni 34, kati ya hiyo, kiasi cha Shilingi bilioni 11.3 kilikuwa kimepitiliza muda wa kulipa. Deni la SACCOS ni kiasi cha Shilingi bilioni 7.5, ambayo ni sehemu ya deni lililopitiliza muda wa kulipa. Kwa mujibu wa makadilio ya menejimenti, deni hilo lina muda zaidi ya mwaka mmoja.

SACCOS iliweka wadaiwa wake kama dhamana ya deni la benki. Wadaiwa haohao waliwekwa kama dhamana kwenye deni lingine ambalo SACCOS alikuwa anadaiwa bila benki kujua. Hali hii inapelekea ulipwaji wa deni kuwa mgumu. Menejimenti inatakiwa kuongeza juhudi katika kukusanya madeni.

4.21.3 Wakopaji Kutumia Fedha kwa Malengo Yasiyokusudiwa

Benki ya Maendeleo ya TIB ina mkataba na Serikali kutoa mikopo ya kilimo kupitia mradi wa kilimo kwanza. Mkataba huo unahitaji TIB kuhakikisha kuwa wakopaji wanakidhi matakwa ya Serikali. Wakati wa ukaguzi tulibaini baadhi ya wakopaji walituma mkopo kwa malengo shughuli zingine tofauti na malengo ya kuchukuwa mikopo. Katika baadhi ya matukio, SACCOS ilitoa kiasi cha mkopo ambacho kilikuwa chini ya kiasi ambacho kilitakiwa kutolewa. Pia, tulibaini baadhi ya wakopaji walikuwa hawatunzi kumbukumbu sahihi za miradi yao. Hivyo Benki, haikufuata makubaliano iliyowekeana na Serikali kuhusu usimamizi wa wakopaji.

Jedwali 4: **Wakopaji Waliotumia Fedha kwa Malengo Yasiyokusudiwa**

Jina la SACCOS	Fedha iliyotolewa na benki Shilingi '000	Fedha iliyopokelewa na wakopaji Shilingi '000	Maoni
Wafanya biashara Njombe SACCOS	194,000	193,110	Tofauti ya Shilingi 890,000 haijatolewa maelezo
Mtibwa SACCOS	200,880	180,580	Tofauti ya Shilingi 20,300,000 haijatolewa maelezo

TPAWU SACCOS Kilombero	199,760	174,120	Tofautii ya Shilingi 25,640,000 haijatolewa maelezo
Mpunga Mmoja	100,000	100,000	Hakuna taarifa za maendeleo ya mradi zilitunzwa.
Kago Farm	400,000	400,000	Marejesho ya Shilingi 43,190,000 yalifanyika hadi Disemba 2012 na hakukuwa na taarifa zilizotunzwa
Laila Agro Diary	385,170	385,170	Hakuna taarifa ya mradi ilitunzwa.
Jumla	**1,479,810**	**1,432,980**	

Menejimenti ya Benki ya maendeleo inashauriwa kuongeza usimamizi wa miradi ili kuhakikisha kwamba fedha zinatumika kama ilivyokusudiwa na Serikali.

4.21.4 Mkopo wa Shilingi Bilioni 5.3 wa PRIDE ambao bado haujalipwa Hadi kufikia Disemba 2014 PRIDE ilikuwa na deni la Shilingi bilioni 5.3 ambao ni mkopo uliotolewa na Benki ya Uwekezaji. Mkopo huu umedhaminiwa na wadaiwa wa Pride, ikimaanisha wakati kampuni ikishidwa kulipa madeni, madeni hayo yatalipwa kwa kutumia wadaiwa wa Pride. Dhamana ya aina hii haina uhakika na inaweza kusababishia benki hasara.

Menejimenti inatakiwa kuongeza nguvu ili kuhakikisha kwamba mkopo unalipwa. Pia, Menejimenti inatakiwa kutoa mkopo kwa wakopaji wenye dhamana ya kueleweka.

4.22 Shirika la umeme la Tanzania (TANESCO)

4.22.1 Ukosefu wa mpango sahihi wa kazi ya ujenzi

Mnamo Machi 2011, shirika la Taifa la umeme la Tanzania (TANESCO) ilimshirikisha Aviation and General Security Consultant kwa ajili ya kusambaza, na kufunga mfumo wa usalama TANESCO Makao Makuu, Kituo cha kuongoza Gridi ya Taifa na kituo cha Kurasini kwa bei ya Dola za Marekani 602,550 (sawa na Shilingi bilioni 1.22 pamoja na VAT). Mgavi alipatikana kwa njia ya zabuni ya ushindani wa kimataifa na zoezi lilitakiwa kuendeshwa kwa awamu mbili.

Hata hivyo, baada ya kukamilika kwa awamu moja, ambayo ilikuwa na gharama ya Dola za Marekani 361,500, Kampuni kupitia Bodi ya Zabuni ilifuta mkataba kwa matatizo ya kifedha yanayoikabili kampuni.

Mnamo tarehe 27 Mei, 2015 TANESCO illingia mkataba mwingine na Mzabuni yule yule kwa kazi ile ile kama aliyopewa mwezi Machi 2011 ila walipanua wigo wa kazi ambayo ilikuwa na bei ya Dola za Marekani 975,000.

Kulingana na Menejimenti, hii ilitokana na kupita miaka minne iliyopelekea Mkandarasi kutotumia taarifa ya uchunguzi wa ardhi ya mwaka 2011. Aidha, mabadiliko ya wigo ambayo ni pamoja na kufanya uchunguzi wa usalama na mabadiliko ya muda wa mkataba kutoka mwaka 1 hadi miaka 3 ilisababisha Mkandarasi kurudia uchunguzi wa ardhi ambao ulishafanyika. Ni dhahiri kwamba kulikuwa na ukosefu wa umakini kuhusu wigo wakati wa kutoa mkataba.

4.22.2 Miamala ya Udanganyifu Iliyofanywa na Wachuuzi wa LUKU Shilingi bilioni 2.76

TANESCO iliingia mikataba na mawakala mbalimbali kwa ajili ya kuuza LUKU. Awali mawakala waliweka amana katika akaunti ya benki ya Shirika la Taifa la Umeme. Baada ya hapo mawakala waliweka amana katika mfumo wa Elipse LUKU katika sehemu yake ya mauzo. Mfumo wa mauzo wa mchuuzii utatoa risiti ya amana ambayo wakala ataiwasilisha kwenye Ofisi ya Shirika la Taifa la Umeme kwa ajili ya uthibisho wa muamala.

Wakati wa ukaguzi tulibaini kwamba kitengo cha ukaguzi wa ndani kiligundua mapungufu katika matukio 381 ya uthibitisho wa amana ya Shilingi bilioni 2.76 kufanyika zaidi ya mara moja kwa muamala mmoja. Hii iliwezekana kwa sababu ya udhaifu uliopo kwenye mfumo wa LUKU (Elipse) ambao una hifadhidata mbalimbali zilizounganishwa pamoja. Uthibitisho mbalimbali wa fedha zilizowekwa amana na wachuuzi inasababisha hasara kwa Shirika la Taifa la Umeme. Tulitaarifiwa kwamba wafanyakazi wote

waliohusika walisimamishwa kazi na kesi bado ipo chini ya uchunguzi wa polisi.

Nashauri Menejimenti kuimarisha udhibiti wa mfumo wa LUKU katika namna ambayo haitaruhusu uthibitisho mwingi. Zaidi ya hayo, Menejimenti inatakiwa kuwanzisha utaratibu wa kusahihisha mapungufu ikiwemo kuzuia wachuuzi kujihusisha na miamala ya udanganyifu.

4.23 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

4.23.1 Mapungufu yaliyobainika katika kutekeleza mkataba na Star Media

Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) liliingia mkataba na Star Media tarehe 2 Agosti 2011 (ukafanyiwa mapitio tarehe 1 Julai 2014) ambapo Star Media ilipewa jukumu na TBC la kutoa Matangazo ya Kidigitali ya Televisheni (DTT). Kwa kuzingatia huduma inayotolewa na mtoa leseni kwenda kwa mpokea leseni. Mpokea leseni alikubali kutoa huduma ya matangazo kwa mtoa leseni.

Katika mkataba, hakuna malipo yatakayofanyika kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine. Pande mbili inabidi zikubaliane kwamba upande mmoja utatoa kwa upande mwingine kiasi cha ziada baada ya kulinganisha madeni. Kutokana na mkataba, thamani ya muamala wa mwaka kati ya pande mbili unatakiwa usizidi Shilingi milioni 1.40. Mapungufu yafuatatayo yalibainika:

- Maelezo na mchanaganuo wa gharama kwa kila huduma iliyotolewa na cha Star Media kwa Shirika la Utangazaji la Taifa hazikuoneshwa lakini Hati ya madai ilitolewa.

- Shirika la utangazaji la Taifa (TBC) lilitoa Shilingi bilioni 1.335 kwa Star Media kwa ajili ya kurusha matangazo. Hata hivyo kiasi kilichoandikwa kwenye vitabu vya

hesabu ni Shilingi bilioni 1.40. Hakuna maelezo yaliyotolewa kuhusu tofauti ya Shilingi milioni 65. Zaidi ya hayo, kiasi kilichotumika si kama kilichopo kwenye kumbukumbu; na

- Sikuweza kupatiwa maridhiano na uthibitisho kati ya pande mbili kuhusu makubaliano ya kiwango cha mwisho kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2015. Mikataba inaruhusu kulipana kati ya pande husika kwa tofauti yeyote.

Mkataba ulioingiwa unaweza sababisha hasara kwa Shirika la Utangazaji la Taifa kwa sababu mchanganuo wa huduma inayotolewa haujaoneshwa. Inashauriwa kila upande kuendesha shughuli kutokana na uwezo na kulipana kiwango kilichobakia kwa kuzingatia kazi iliyofanyika.

Menejimenti inatakiwa kuhakikisha kwamba mchanganuo wa gharama ya kila huduma inayotolewa na Star Media unakuwemo kwenye mkataba. Pia, Menejimenti inatakiwa kuhakikisha kuwa urushaji wa matangazo unaotumiwa na Star Media unapewa thamani kwa kuzingatia kiasi kilichopo kwenye kadi.

4.24 Shrika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

4.24.1 Madeni yaliyokaa muda mrefu yenye thamani ya Shilingi bilioni 138.37

Tulibaini salio la wadaiwa ambalo limekuwepo kwa zaidi ya mipaka ya muda wa mikopo iliyotolewa kwenye ankara. Mkusanyiko wa salio la madeni umesababishwa na kutowepo kwa ufanisi katika usimamizi wa madeni hayo. Mchanganuo wa madeni umeoneshwa hapa chini:

Jedwali 5: Madeni yaliyokaa muda mrefu

Maelezo	Kiasi (Shilingi)
Songas Limited.	50,275,344,006
Pan African Energy Limited	60,665,839,011
TANESCO-Somanga Fungu.	143,194,010
Marejesho ya kibiashara	17,076,268,987
Marejesho ya Watumishi	412,920,214

Maelezo	Kiasi (Shilingi)
Marejesho ya Ada za leseni za muda mrefu	884,906,735
Marejesho ya Ada za mafunzo za muda mrefu	3,456,653,543
Malipo ya madeni ya utafiti wa masoko	5,451,947,252
Jumla	**138,367,073,758**

Kiwango ni kikubwa sana na kinaweza kuwathiri shughuli za Shirika kwa sababu pesa taslimu inashikiliwa na wateja badala ya kutumika kutekeleza shughuli za Shirika.

Menejimenti inashauriwa kuongeza juhudi za kurejesha madeni ili kuepuka kuwathiri shughuli za Shirika.

4.24.2 Gawio la Dola za Marekani 467,997 halijalipwa na Songas

Wakati wa ukaguzi tulibaini, Songas Limited ililipa gawio la Dola za Marekani 3,873,003 kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC). Katika kuthibitisha usahihi wa gawio liilolipwa, tuliomba madokezo ya vikao vya Bodi yaliyoidhinisha gawio lililotamkwa na hitimaye kulipwa. Hata hivyo hazikuwasilishwa kwetu. Uchunguzi wa vitabu vya hesabu vya Songas kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Disemba, 2014 ulibaini kwamba gawio lililopitishwa ni Dola za Marekani milioni 15. Gawio lililokokotolewa tena kwa kuzingatia asilimia 29 ya hisa inazomiliki Shirika kwa Songas ni Dola za Marekani 4,350,000. Hii inaonesha kwamba kuna gawio kiasi cha Dola za Marekani 476,997 ambayo haikulipwa. Kiasi cha gawio ambacho hakijalipwa kitapunguza mapato ya Shirika kutoka kwenye uwekezaji wa Songas. Hii inaonesha udhibiti duni wa Shirika katika uwekezaji wake.

Menejimenti inatakiwa kuhakikisha kwamba gawio lililolipwa chini ya kiwango lilipwe kiasi kilichobakia ili kuimalisha shughuli za Shirika.

4.24.3 Kukosekana kwa hati ya hisa

Tuliomba hati ya hisa ya Songas Limited lakini haikuweza kuwasilishwa kwetu kwa ajili ya uthibitisho wa Shirika kumiliki hisa. Ni vigumu kujiridhisha thamani ya uwekezaji

wa Shirika la Maendeleo ya Petroli bila ya kuwepo hati za hisa. Tunashauri Shirika la Maendeleo ya Petroli ahifadhi hati zote katika sehemu salama.

4.25 Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi ya Elimu ya juu (HESLB)

4.25.1 Thamani ya Fedha kwenye Ubainishwaji wa Gharama za Ukusanyaji wa Mikopo

Tuliweza kubaini jumla ya Shilingi bilioni 1.06 ililipwa kwa mawakala wanaokusanya madeni. Kati ya hiyo, Shilingi milioni 895.36 ilikuwa ni kwa ajili ya kubaini madeni na Shilingi milioni 164.64 kwa ukusanyaji. Ukaguzi ulibaini kuwa jumla ya Shilingi milioni 615.27 zililipwa kwa mawakala kwa ajili ya kubaini madeni ya taasisi za serikali ambayo ni sawa na asilimia 89 ya hela iliyolipwa.

Kwa maoni yangu, Bodi kupitia wafanyakazi wake wenyewe bila kutumia mawakala inaweza kufuatilia kwa urahisi chanzo cha madeni ya wafanyakazi wa serikali kupitia Ofisi ya Raisi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma au Serikali za Mitaa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na kubaini madeni hayo. Hivyo basi, kama ukusanyaji ungefanywa na wafanyakazi wa Bodi, Bodi ingeweza kuokoa kiasi hiki cha fedha ambazo zingetumika katika masuala mengine ya uendeshaji wa Bodi ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo kwa wanafunzi.

Menejimenti inashauriwa kutumia wafanyakazi wake kwenye kubaini na kukusanya mikopo katika taasisi za umma ambako wanafanyakazi wadaiwa. Hii inaweza kufanikiwa endapo Bodi ya mikopo itaweza kushirikiana na taasisi zote za serikali kwa ajili ya kubaini madeni.

4.25.2 Mapungufu Kwenye Uwekezaji wa Amana za Akiba

Bodi ya mikopo imekuwa ikiwekeza kwenye akiba za muda mrefu kwa miaka kadhaa sasa. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Bodi iliweza kuwekeza kiasi cha Shilingi bilioni 6.5. Uwekezaji huo ulifanywa kwenye Bank M (Shilingi bilioni 3.4) kwa muda wa miezi mitatu kwa riba ya asilimia 14, na Benki ya Posta (Shilingi bilioni 3.1) kwa miezi sita kwa riba ya asilimia 15.

Katika mapitio ya usimamizi wa uwekezaji wa amana za akiba tumebaini kuna ukosefu wa sera ya uwekezaji katika Bodi ambayo ingeweza kuonyesha taratibu zinazotakiwa kufuatwa wakati wa uwekezaji kwenye amana za akiba. Hii ni kinyume na matakwa ya kanuni ya fedha ya Bodi ya mikopo.

Pia tuliweza kubaini kuwa hakuna vigezo vyovyote ambavyo Bodi ya mikopo inatumia kwenye kuwamua benki gani inawekeza. Hii inatokana na ukosefu wa sera ambayo ingechanganua taratibu zote.

Kutokana na kukosekana kwa sera hiyo ya uwekezaji, uhalali wa maamuzi yaliyotolewa na menejimenti kwenye uwekezaji wa Shilingi bilioni 6.5 katika Bank M na Benki ya Posta haukuweza kuthibitika.

Pia, Kukosekana kwa sera hiyo ya uwekezaji kunadhoofisha maamuzi ya kuwekeza benki ambazo zingetoa masharti yenye tija kwenye uwekezaji. Hali hii inapelekea kuongeza athari za upotevu wa fedha kutokana na kutokuwa na ufanisi kwenye vipaumbele vya uwekezaji.

Napendekeza Menejimenti ya Bodi ya mikopo iandae sera ya uwekezaji kulingana na matakwa ya kanuni za fedha za Bodi ya mikopo. Pia sera hiyo inapaswa ielezee taratibu zote za uwekezaji wa amana ya akiba.

4.25.3 Salio la Madeni ya Mikopo kwa Wanafunzi

Tathmini ya madeni kwa wanafunzi ilibaini kwamba, Bodi ya mikopo ilikuwa inadai mikopo ya Shilingi bilioni31.91 mwishoni mwa mwaka wa fedha unaoishia June,2015. Bodi haijafanya makadirio ya kupunguza madeni ya wanafunzi yasiyolipika. Zaidi ya hayo, hakukuwa na viambatisho vya kutosheleza vinavyo onyesha madeni inayowadai wanafunzi kutoka kwenye mifumo ya kielektroniki ya mikopo ikilinganishwa na mchanganuo wa madeni hayo.

Kutokana na kukosekana kwa mchanganuo wa mikopo huo, hatukuweza kujua usahihi wa taarifa iliyotolewa kwenye vitabu vya Bodi.

Tunapendekeza yafuatayo kwa menejimenti:

i. Kuwandaa mchanganuo ambao utalinganisha taarifa iliyopo kwenye vitabu dhidi ya taarifa halisi ya mikopo iliyopo kwenye mfumo wa kielektroniki
ii. Kubuni na kuendeleza taarifa ambazo zitatumika kama msingi wa kulinganisha mchanganuo wa mikopo (General ledger) na taarifa itokanayo na mfumo wa kielektroniki;
iii. Menejimenti inapaswa kupitisha makadirio (provision) ya madeni ambayo hayalipiki kwenye taarifa zake za fedha; na
iv. Juhudi zaidi ziongezwe kwenye ukusanyaji wa madeni hayo.

4.26 Mambo Muhimu Yanayoathiri Taasisi Mbalimbali za Umma

4.26.1 Ucheleweshaji wa Ukamilishaji wa Ujenzi wa Miradi

Mashirika sita ya umma yaliingia mikataba na makandarasi kwa ajili ya miradi mbalimbali ya ujenzi. Niliweza kubaini ucheleweshaji wa miradi ambayo iligharimu taasisi kiasi cha Shilingi bilioni132.43. Orodha ifuatayo ni ya miradi iliyocheleweshwa katika taasisi mbalimbali:-

Jedwali 6: Ucheleweshaji wa Kukamilika kwa Ujenzi wa Miradi

Namba	Taasisi za Umma	Miradi	Matarajio ya Kukamilisha	Shilingi "Milioni"
1	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa MazingiraDar es Salaam	Uchimbaji wa visima nane (8)	Mei-13	7,543
2	Mamlaka ya Maji Safi na Majitaka Dar	Ujenzi wa usambazaji maji Ruvu	Disemba-13	120,256

	es Salaam	chini		
3	Mamlaka ya Maji Safi na Majitaka Dar es Salaam	Uhamishwaji wa bomba katika daraja la Kigamboni	Mei-14	198
4	Mamlaka ya Maji Safi na majitaka Njombe	Awamu ya pili ya Mradi wa maji safi Nyenga	Novemba-14	1,100
5	Mamlaka ya Maji Safi na majitaka Arusha	Uchimbaji wa visima nane (8)	Aprili-15	3,190
6	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam	Mradi wa uhifadhi wa mmomonyoko wa udongo	Julai-13	144
Julmla				**132,431**

Ucheleweshaji wa miradi hii unapelekea gharama za miradi kuongezeka kutokana na bei za malighafi kupanda. Menejimenti katika taasisi husika zinashauriwa kuzingatia matakwa ya namba 114 ya kanuni ya manunuzi mwaka 2013 katika suala la usimamizi bora wa mikataba.

4.26.2 Ufanisi katika Ukusanyaji wa Kodi ya Pango

Mashirika matatu ya umma yaliingia mikataba ya kupangisha majengo yao kwa makubaliano ya ulipaji wa kodi. Niliweza kubaini jumla ya Shilingi bilioni 18.69 haijalipwa na wapangaji wa majengo hayo kinyume na mikataba hiyo kama inavyoonekana kwenye Jedwali Namba 8. Zaidi ya hapo, tuligundua baadhi ya wapangaji waliondoka kwenye majengo hayo bila kulipa madeni yao.

Jedwali 7: Ufanisi katika Ukusanyaji wa Kodi ya Pango

Namba	Taasisi	Kipindi	Kiasi kisicholipwa	Wapangaji Waliotoka bila kulipa

			'Million"	'Million"
1	Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma	30-Juni-15	2,040	-
2	Shirika la Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii	30-Juni-14	8,751	6,091
3	Shirika la Nyumba la Taifa	31-Disemba-14	7,900	-
Jumla			**18,69**1	**6,091**

Hali hii ina athari kubwa kwenye ukwasi wa taasisi kwa sababu mapato yatokanayo na upangishaji yana mchango mkubwa kwenye uongezaji wa mapato ya taasisi hizo. Hivyo basi, menejimenti ya taasisi hizo inashauriwa kufanya jitihada za ziada kwenye ukusanyaji wa kodi ikiwa ni pamoja na kuchukuwa hatua za kimahakama na marekebisho ya mikataba ya majengo kwa kuwanzisha malipo ya awali na amana ya usalama.

4.26.3 Mapato yaliyopotea kutokana na upotevu wa Maji-Shilingi bilioni 17.965

Uchambuzi wa upotevu wa maji ulibainisha kuwa kuna asilimia kubwa ya maji yanayopotea katika Mamlaka za Maji. Upotevu huo wa maji ni zaidi ya asilimia zinazoruhusiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji. Hivyo basi, tuliweza kubaini hasara ya takribani Shilingi bilioni 17.97 ikiwa ni hasara kwenye taasisi tatu za maji kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la 8

Jedwali 8: Mapato yaliyopotea Kutokana na Upotevu wa Maji

Namba	Taasisi	Hasara Inayokubalika na Wizara	Jumla ya Hasara ya maji yaliyopotea	Shilingi 'Million"
1	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa MazingiraDar es Salaam	25%	57%	11,580

Namba	Taasisi	Hasara Inayokubalika na Wizara	Jumla ya Hasara ya maji yaliyopotea	Shilingi 'Million"
2	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa MazingiraNjombe	20%	36%	175
3	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa MazingiraArusha	35%	45%	6,210
Total				**17,965**

Hasara hiyo inasababishwa na matatizo ya kiufundi na kibiashara kama vile uvujaji wa mabomba, na wateja wasiosajiliwa kutodaiwa hupelekea upotevu wa maji na hasara ya mapato kwa mamlaka za maji. Hasara ni kubwa hivyo inazuia utekelezaji na utendaji wa mamlaka hizo. Hivyo basi, inashauriwa kupunguza upotevu wa maji kwa kudhibiti matatizo ya kiufundi na kibiashara hadi kwenye kiwango kinachokubaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji.

4.26.4 Ucheleweshaji na Kutopelekwa kwa Makato ya kisheria – Shilingi Milion 743.4

Tathmini ya makato ya kisheria ilibaini kwamba baadhi ya mashirika hayakupeleka makato yake kwa muda uliowekwa. Mafao hayo ya wafanyakazi ambayo hayajapelekwa yanajumuisha kodi na michango ya pensheni kwa kiasi cha shilingi milioni 743.40. Ucheweleshaji wa makato hayo utapelekea kulipa faini, riba, na adhabu ambayo itaathiri hali ya kifedha ya mifuko na hivyo kupelekea kushindwa kufikia malengo yaliyopangwa. Mafao ya wafanyakazi na kodi ambayo hayajapelekwa kwa wakati imeelezewa kwenye jedwali Namba 9

Jedwali 9: Ucheleweshaji na kutopelekwa kwa makato ya kisheria

Namba	Taasisi	Mafao hayo yanajumisha PAYE 'Milioni"	Kodi(VAT, WHT) 'Milioni	Jumla 'Milioni"

1	COSTECH	504.39		504.39
2	TBT	69.93		69.93
3	BAUWASA	18.23		18.23
4	NIT	15.42		15.42
5	MWAUWASA		92.36	92.36
6	TNBC		9.47	9.47
7	IFM		33.6	33.6
8	TANESCO		1,360	1,360
9	TPRI	251.61		251.61
10	NIP	30.15		30.15
11	Wizara Ya Fedha	24240		24240
Jumla		**25,129.73**	**1,495.43**	**26,625.15**

Madeni hayo yameendelea kuongezeka kwa miaka kadhaa ambayo yanaathiri ulipaji wa mafao kwa wafanyakazi kutoka kwenye mifuko ya pensheni husika kipindi cha kustaafu.

Menejimenti inashauriwa kuchukuwa hatua muhimu ili kuhakikisha makato yote ya kisheria yanapelekwa kwenye mifuko husika kwa wakati ili kuepuka faini/ riba na adhabu ambazo zitatozwa kwenye mashirika na taasisi kutokana na kucheleweshwa kwa makato hayo.

4.26.5 Kutokuwepo kwa Bodi ya Wakurugenzi na Bodi ya Wadhamini

Kwa mwaka huu wa ukaguzi, kulikuwa na Bodi 19 ambazo zimemaliza muda wake na hakuna Bodi mpya zilizochaguliwa mpaka tunakamilisha ukaguzi wetu mwezi Machi 2016. Baadhi ya taasisi zimekuwa zikiendelea na utendaji wa kazi bila ya Bodi kwa zaidi ya mwaka mmoja. Taasisi ambazo hazina Bodi zimeonyeshwa kwenye kiambatanisho Namba tatu.

Pia, baadhi ya taasisi zilikuwa na Bodi ingawa Bodi zao hazikuweza kukaa kwa wakati kuidhinisha na kupitisha taarifa za mahesabu yao. Kutokuwepo kwa Bodi ya Wakurugenzi na Wadhamini kunazorotesha shughuli za kiutendaji za mashirika hayo. Taasisi ambazo zina Bodi lakini hazikuweza kukaa kujadili na kupitisha taarifa za

mahesabu zimeonyeshwa kwenye kiambatanisho Namba nne.

Tunashauri serikali iteuwe Bodi ya Wakurugenzi na wadhamini mara tu inapomaliza kipindi chake, pia Bodi zikae kwa muda muafaka kupitisha na kukubalina na taarifa za mahesabu ili kufanikisha ukaguzi wetu ufanyike kwa muda muafaka.

4.26.6 Kutokufanyika kwa ukaguzi kutokana na upungufu wa fedha

Kwa mwaka huu wa ukaguzi, nimeshindwa kufanya kaguzi 34 kutokana na upungufu wa fedha. Hata hivyo, baadhi ya taasisi hazikuweza kulipa wakaguzi binafsi walioteuliwa hivyo kupelekea kuchelewa kwa kaguzi hizo. Taasisi ambazo hazikuweza kukaguliwa na ambazo kaguzi zake zilichelewa zimeonyeshwa kwenye kielelezo namba sita.

Tunaishauri Hazina itoe fedha kwa muda muafaka kama ilivyoidhinishwa katika bajeti ili kufanikisha ufanyikaji wa ukaguzi ambao utapelekea utoaji wa taarifa kwa muda muafaka kama sheria inavyotaka.

SURA YA TANO

MAPITIO YA MIKAKATI NA UENDESHAJI WA KIUFANISI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

5.0 UTANGULIZI

Usimamizi wa kimkakati unajumuisha mipango endelevu, ufuatiliaji, uchambuzi, na Tathmini ya mambo yote muhimu kwa ajili ya shirika kuweza kufikia malengo na madhumuni yake. Usimamizi wa kimkakati unahusisha kuchambua uwezo na udhaifu wa ndani na nje; kutengeneza mipango na Tathmini ya utekelezaji wake, pamoja na kutathmini ni kwa kiwango gani hatua za mipango zimefanikiwa kuleta mabadiliko, au pale matokeo tarajiwa hayakuweza kupatikana.

Katika muktadha wa kibiashara, ufanisi katika uendeshaji ni uwiano kati ya mtaji uliowekwa katika kuendesha biashara na mapato yatokanayo na biashara. Ufanisi katika uendeshaji unajumuisha mikakati kadhaa iliyotumika ili kutimiza lengo la msingi la kutoa bidhaa zenye ubora au huduma kwa wateja katika gharama nafuu na kwa wakati muafaka. Pia, inahusisha upatikanaji wa thamani zaidi kutoka kwenye rasilimali na upotevu katika shughuli za uzallishaji au uendeshaji wa biashara kwa lengo la kuongeza tija.

Tathmini yangu ya ufanisi katika uendeshaji inajumuisha mashirika nane ya umma ambayo ni:

- Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)
- Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA)
- Mamlaka ya Udhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA)
- Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA)
- Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)
- Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)
- Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na
- Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO)

5.1 Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)

5.1.1 Tathmini ya Machakato wa Ubinasfishaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)

Mnamo mwaka 2002 kama sehemu ya utekelezaji wa sera ya Serikali ya ubinafsishaji na uchumi huria, Serikali ya Tanzania iliweka asilimia 49 ya hisa zake kwenye Shirika kwa wakati huo likiitwa Shirika la Ndege Tanzania (ATC) na kukabidhi usimamizi wa hisa hizo kwa Shirika la Ndege la Afrika Kusini. Baada ya hapo Kampuni ya Ndege Tanzania ilianzishwa chini ya sheria ya makampuni namba 212 kama kampuni binafsi.

Wakati wa ubinafsishaji, Shirika la Ndege lilikuwa na ndege mbili ambazo ni B737-200 iliyokuwa ikimilikiwa na shirika hilo na B737-300 ikiwa imekodishwa chini ya mkataba wa matengenezo kuwa juu ya anayekodi. Zoezi la ubinafsishaji lilipelekea upunguzaji wa rasilimali watu kutoka nguvu kazi ya wafanyakazi 493 mpaka kufikia 251 ili kuhakikisha muundo mpya wa uendeshaji unaanza kampuni ikiwa na rekodi safi za fedha. Serikali ya Tanzania ilichukuwa madeni yote ya Shirika la Ndege Tanzania (ATC) kwa kuyaweka madeni hayo chini ya Shirika Hodhi la Ndege (ATC) linalomilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali. Shirika Hodhi la Ndege liliundwa kwa ajili ya kuchukuwa rasilimali zote za Shirika la Ndege Tanzania ambazo hazihusiani moja kwa moja na biashara ya kampuni pamoja na madeni yake yote ambayo hayajalipwa.

Ukaguzi umegundua kuwa, ingawa iliaminika kwamba mabadiliko haya ya kimuundo yangeleta ufanisi na kuongeza tija ndani ya Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) kama ilivyothibitika na kuonekana katika baadhi ya mashirika machache yaliyobinafsishwa, matokeo yalikuwa ni kinyume na matarajio.

Matokeo ya ubinafsishaji huu yalipelekea kampuni kupata hasara kupitia:

- Kuongezeka kwa gharama za usimamizi kwa njia ya ada ya usimamizi iliyotozwa na Shirika la Ndege la Afrika Kusini (SAA;

- Kuongezeka kwa gharama za matengenezo zinazolipwa kwa Kampuni ya Ufundi ya Afrika Kusini (SAT), ambayo ni kampuni tanzu ya Shirika la Ndege la Afrika Kusini (SAA) ;

- Kuongezeka kwa gharama za uendeshaji

- Kuwacha kazi kwa wafanyakazi wengi tegemezi wenye uwezo hasa wahandisi ; na

- Gharama kubwa za kukodi zilizolipwa kwa Shirika la Ndege la Afrika Kusini (SAA) kwa ajili ya ndege zilizokodishwa.

Kampuni iliendelea kupata hasara mpaka mwaka 2006 Serikali ilipoamua kununua tena hisa kwa asilimia 49 kutoka Shirika la Ndege Afrika Kusini (SAA). Kwa mara nyingine tena Serikali iliendelea kuwa mdau pekee kwenye umiliki wa Shirika la Ndege la Taifa. Wakati huo, Kampuni ya Ndege ya Taifa (ATCL) ilikuwa na mtaji hasi wa thamani ya Shilingi bilioni 6.9.

Ni dhahiri kwamba ubinafsishaji wa chombo hiki haukuzingatia kwa kina malengo mafupi ya ubinafsishaji na jinsi yanavyohusiana na malengo ya muda mrefu ikiwa ni pamoja na maendeleo ya mahitaji ya soko ndani ya sekta ya usafiri wa anga.

Hakukuwa na ushahidi kuwa Serikali ilifanya tathmini yoyote ya awali juu ya manufaa ambayo yangetokana na kuingia ubia kati ya Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na Kampuni ya Ndege ya Afrika Kusini. Tathmini yetu iliyofanywa juu ya matokeo baada ya ubinafsishaji ilibaini kuwa Serikali, kupitia Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) haikufanya uchambuzi wowote wa kina ili

kubaini gharama na vikwazo vitakavyopelekea kutofikiwa kwa malengo ya muda mrefu ya kampuni.

5.1.2 Kutokuwepo kwa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi vya Kibiashara

Mfumo wa usimamizi wa athari kwa kawaida huhusisisha kanuni za misingi ya utawala bora kwa kutambua kwamba usimamizi wa vihatarishi ni mbinu muhimu katika kufikia madhumuni na malengo ya taasisi.

Nilibaini kuwa Kampuni haijaanzisha mfumo wa sera ya usimamizi wa viashiria vya hatari za kampuni. Pia nilibaini kuwa hakuna utaratibu wa kutathmini athari zinazoikabili Kampuni. Kampuni bado haijaanzisha majukumu yanayohusiana na usimamizi wa viashiria vya hatari na miundo yake inayojumuisha uundaji wa kamati ya usimamizi wa viashiria vya hatari kwa ajili ya kusimamia utaratibu mzima wa usimamizi wa viashiria vya hatari.

Kukosekana kwa mfumo wa usimamizi wa athari unaoelezea kwa kina taratibu zote za mfumo wa athari zinazoikabili Kampuni kunaathiri uwezo wa Kampuni kutambua, kuchambua, au kudhibiti kiwango cha kukabiliwa na athari za kiutendaji na kimfumo ndani ya mfumo mzima wa utendaji wa Shirika.

5.1.3 Ukodishaji wa Ndege Usiokuwa na Faida

Ukaguzi umebaini kuwa tarehe 9 Oktoba, 2007, Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) ilisaini mkataba wa ukodishaji wa ndege (Airbus namba A320-214 yenye usajili namba MSN630) kutoka Kampuni ya Wallis Trading Co. Ltd. Hata hivyo, mkataba wa kukodi haukufuata utaratibu muhimu na rasmi wa uendeshaji wa kampuni.

Kwa mujibu wa taratibu hizi, Kitengo cha Ufundi ndani ya Kampuni kinawajibika kufanya uchunguzi wa ubora na kupata maelezo yote ya ndege kabla ya kuingia katika makubaliano yoyote ya kukodisha. Kwa upande mwingine, TCAA pia ni inawajibika kuchunguza na kukagua ndege ili

kuhakikisha kwamba inaendana na viwango vya sayansi na ufundi wa vyombo vya anga vya kimataifa kabla ya kusajili ndege husika katika nchi.

Nilibaini kuwa vitengo vyote viwili vya ufundi cha Kampuni ya Ndege Tanzania na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania lifanya uchunguzi wao kati ya tarehe 14 na 22 Januari, 2008 wakati mkataba wa kukodi ulikuwa umekwisha kusainiwa. Matokeo ya ukaguzi yalionyesha kuwa ndege haikufikia viwango vinavyohitajika hivyo Mamlaka ya Usafiri wa Anga ilimpa maelekezo mkodishaji kurekebisha mapungufu yaliyoonekana kabla ya kukabidhi ndege hiyo kwa Kampuni ya Ndege Tanzania. Aidha, nilibaini kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mnamo tarehe 8 Oktoba, 2007 aliishauri Kampuni kupitia barua yake yenye kumbukumbu no.JC/I.30/308/3 lakini ushauri wake haukuzingatiwa wakati mkataba wa kukodi ndege unasainiwa.

Ili kutimiza matakwa ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga kufuatia ukaguzi wao waliofanya, kampuni ya Wallis Trading Co LTD ilifanya matengenezo yaliyoelekezwa mwezi Februari, mwaka 2008. Hata hivyo, Mkodishaji hakukabidhi ndege kwa Kampuni ya Ndege Tanzania mpaka ilipofika mwezi Mei, mwaka 2008 baada tu ya Serikali kutoa barua ya dhamana ya thamani ya Dola za Marekani milioni 60 tarehe 2 Aprili mwaka 2008.

ATCL ilikuwa ikigharamika kodi ya mwezi ya Dola za Marekani 370,000 kiasi kwamba kati ya Oktoba mwaka 2007 na Mei mwaka 2008 Kampuni ilikuwa ikidaiwa limbikizo la kodi la kiasi cha Dola za Marekani 2,590,000 kabla ya ndege kukabidhiwa rasmi kwa Kampuni ya Ndege Tanzania. Ndege ilifanya kazi kwa muda wa miezi sita hadi mwezi Novemba mwaka 2008. Ilipofika mwezi Disemba mwaka 2008 ndege ilitupelekwa katika Kampuni ya Ndege ya Mauritius kwa uchunguzi mkubwa wa kiufundi ambapo ilikaa hadi mwezi wa Juni mwaka 2009. Mwezi Julai mwaka

2009 ndege ilihamishiwa kwenye Kampuni ya Ndege ya Ufaransa kwa uchunguzi wa C+12. Makadirio za matengenezo yaliyofanyika yalikuwa Dola za Marekani 593,560 dhidi ya gharama halisi ambapo iliongezeka kufikia Dola za Marekani 3,099,495 baada ya matengenezo ya kina kufanyika. Mmiliki alitoa dhamana ya kuchangia Dola za Marekani 300,000 tu na gharama nyingine kubebwa na Kampuni ya Ndege Tanzania.

Matengenezo yalikamilika mwezi Oktoba mwaka 2010 lakini ndege haikuweza kurudishwa Tanzania kutokana na Kampuni ya Ndege Tanzania kushindwa kulipa gharama husika. Ndege ilikaa Ufaransa kwa kipindi chote cha mkataba wa kukodi hadi tarehe 17 Oktoba 2011 mpaka mkataba ulipositishwa. Wakati mkataba wa kukodi unasitishwa, gharama za kukodi kwa muda wa miezi 43 ambayo ndege hiyo ilikuwa chini ya matengenezo zilifikia Dola za Marekani 15,910,000. Jumla ya gharama ikijumuishwa na ada ya kila mwezi ya kukodi na gharama nyingine kama vile riba ilifikia Dola za Marekani 42,459,316.

5.1.4 Kukosekana kwa Mkakati Mahususi wa Kufufua Shirika

Mkakati wa kufufua taasisi inayotetereka kiutendaji ni mchakato wa kubadilisha kampuni inayopata hasara kuwa kampuni inayopata faida. Mkakati huo ni wa kiutawala na kimuundo, uliopangwa vizuri. Katika kufufua kampuni na kuiletea mafanikio kwa kufuata mpango huo hatua kwa hatua mpango huo unahitaji muda, uwekezaji na ushiriki wa nguvu kazi yenye ufanisi wa hali ya juu.

Sababu nyingi za kushindwa kwa makampuni mengi, mara nyingi, si za moja kwa moja kama vile: washindani wapya katika soko, ongezeko la bei ya malighafi, na mabadiliko katika mahitaji ya soko. Kwa upande mwingine, mambo yanayosababisha kampuni kutofanikiwa ni kama vile menejimenti kushindwa kufanya kazi yake ipasavyo; kuwa na maamuzi mabaya ya kifedha na kushindwa kukabiliana

au kujua mwelekeo mpya uliopo katika sekta husika. Tathmini ya utendaji wa Shirika inaonyesha kwamba Kampuni ya Ndege Tanzania haina uwezo wa kulipa madeni pamoja na kuwa na nguvu kazi yenye watu wenye umri mkubwa kwenye vitengo muhimu kama vile Kitengo cha Ubora na Usalama, wahandisi wa ndege; marubani; na kuwa na uwezo duni wa rasilimali.

Kampuni ya Ndege Tanzania ina wafanyakazi 231 ambao kati yao 127 (sawa na asilimia 55) ni wafanyakazi wa kudumu; 54 wafanyakazi wa mkataba (ambao ni sawa na asilimia 23); na wafanyakazi 50 (sawa na asilimia 22) ni wenye mkataba wa muda. Kati ya wafanyakazi 127 wa kudumu, 39 (sawa na asilimia 31) wako karibu na umri wa kustaafu (yaani zaidi ya miaka 55). Nilibaini kuwa Idara zina idadi kubwa ya maafisa wenye umri unaokaribia kustaafu. Mfano, Idara ya Ufundi ina Wahandisi watano (5) kati ya wahandisi saba wana umri wa zaidi ya miaka 55.

Tathmini ya orodha ya wafanyakazi wenye vyeo vya juu wa Kampuni ya Ndege Tanzania imebaini kuwa baadhi ya idara zinaongozwa na wafanyakazi ambao hawana ujuzi sahihi kulinganisha na nafasi zao kazini. Kwa mfano, katika Kurugenzi ya Biashara, baadhi ya wafanyakazi wana sifa za chini za kitaaluma ambazo hazilingani na nafasi za kazi walizonazo kwa sasa.

Kampuni ina madeni makubwa kiasi cha kushindwa kukidhi gharama zake za uendeshaji. Kampuni hasa inategemea mgao wa fedha kutoka Wizara mama ambazo hautabiriki. Kampuni inakabiliwa na gharama kubwa za matengenezo; kushindwa kuzingatia kanuni za lazima kama vile Chama cha Usafiri wa Anga wa Kimataifa (IATA) ya Ukaguzi wa Usalama wa Usafiri wa Anga (IOSA), ugumu katika kuendesha mafunzo ya lazima kwa marubani na wafanyakazi wa Idara ya ufundi, ugumu katika kufanya ukarabati wa hanga za kutengenezea ndege (airport hangars) na jengo la makao makuu kwa ajili ya kuongeza

kipato kutokana na kodi na huduma za matengenezo ambazo zingetolewa.

Kuwepo kwa uhaba wa kifedha kunaathiri uendeshaji wa Kampuni na kushindwa kutimiza malengo yake kifedha kwa ajili ya kupata muundo sahihi utakaoiwezesha kampuni kutoa huduma zenye ushindani kwenye sekta ya usafiri wa anga.

Nilibainisha kuwa Menejimenti ya Kampuni ya Ndege Tanzania haijaandaa mkakati wowote wa kuifufua kampuni kutoka kwenye hali yake ya sasa ya kupata hasara na kushindwa kulipa madeni na kuwa kampuni inayopata faida. Mapitio ya Mpango Mkakati wa Kampuni kwa vipindi viwili vya mwaka 2007-2012 na mwaka 2015-2020 havionyesha dalili zozote za kuitoa kampuni katika hali yake ya kutokuwa na uwezo wa kulipa madeni.

5.1.5 Kushindwa kupata vyeti muhimu vya usafiri wa anga

Nimebaini kwamba Kampuni ina uhaba wa vyeti muhimu vya usafiri wa anga vinavyotakiwa. Kwa maelezo ya uongozi, zoezi la haraka na muhimu linalotakiwa kukamilika mapema ni ukaguzi wa usalama wa usafiri wa anga wa Chama cha Usafiri wa Anga wa Kimataifa. Kulingana na taratibu na kanuni za uendeshaji, makampuni yote ya ndege yalitakiwa kufuata taratibu za ukaguzi wa usalama za usafiri wa anga (IOSA) kufikia mwisho wa Disemba mwaka 2008. Hata hivyo kutokana na vikwazo vya uhaba wa fedha, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) halikuweza kulipia gharama ambazo zilikadiriwa kuwa Dola za Marekani 1,000,000 kwa mwaka 2008 ili kuwezesha utekelezaji wa ukaguzi huo.

Pia nilibaini kwamba, kutokana na kutofuata kanuni za usafiri wa anga (IOSA), Kampuni ya Ndege Tanzania ilisimamishwa kuwa mwanacahma wa IATA Disemba mwaka 2008 na kubakia mwanachama wa kupitishia wasafiri tu. Uchunguzi zaidi umebaini kwamba, Kampuni ya Ndege Tanzania haifuati taratibu zinazohitajika za Cheti

cha Uendeshaji wa Usafiri wa Anga (AOC). Kampuni inaendeshwa kwa taratibu za uendeshaji wa usafiri wa anga zilizomalizika muda wake toka tarehe 31 Machi mwaka 2010. Ili Kampuni ya Ndege Tanzania ipate Cheti cha Uendeshaji wa Usafiri wa Anga kiasi cha Dola za Marekani 1,400,000 kilitakiwa mwaka 2010. Hii ilikuwa hasa kwa ajili ya kununua kiwango cha chini cha mahitaji ya vipuri ili kuwa na uwezo wa kufanya matengenezo muhimu ya ndege ya shirika aina ya Dash 8; ununuzi wa programu ya matengenezo ya ndege nakuwapatia mafunzo marubani na wahandisi wa ndege ambao Shirika haliwezi kuwapata kutoka wizarani.

Bila kukidhi mahitaji ya vyeti vya usalama wa usafiri wa anga, Shirika linahatarisha usalama wa usafiri kwa ndege zake na kuongeza ugumu kwa Shirika kupanua wigo wa safari zake ili kujikwamua kutoka kwenye hali mbaya ya kifedha ambayo imekuwa ikilikabili kwa muda mrefu sasa.

5.1.6 Kuporomoka kwa Hali ya Kifedha ya Shirika.

Moja ya changamoto zinazoikabili Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ni uhaba wa fedha. Changamoto ambayo imelikabili Shirika hili kwa miaka mingi sasa. Kutokana na taarifa za fedha ambazo hazijakaguliwa, nimegundua kuwa shirika limekuwa likipata hasara kwa miaka 9 mfululizo.

Sehemu kubwa ya mapato ya Shirika yanatokana na mauzo ya tiketi. Mapato ya Shirika yamekuwa yakishuka mwaka hadi mwaka tangu mwaka 2007. Mfano; Kati ya mwaka 2008 na 2013, mapato ya Shirika yalishuka kwa kiwango kikubwa. Kati ya mwaka 2014 na 2015 mapato ya shirika yaliboreka kwa kiwango fulani kufikia mauzo ya Shilingi bilioni 16.24 kwa mwaka 2014 na Shilingi billioni 15.01 kwa mwaka 2015, ikilinganishwa na wastani wa mauzo ya Shilingi bilioni 4.77 kwa kipindi cha kati ya mwaka 2008 mpaka 2013.

Matumizi ya Shirika yamekuwa yakiongezeka kwa kiasi kikubwa mwaka hadi mwaka ambapo mwaka 2008 yalifikia

kiwango kikubwa kuliko miaka yote cha Shilingi bilioni 85.11. Jedwali namba 10 na takwimu namba 1 vinafafanua mwenendo wa mapato, matumizi, na hasara kwa Shirika.

Jedwali 10: Mwenendo wa hali ya kifedha wa Shirika la Ndege Tanzania

Mwaka	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	Jumla
	Kiasi kwa bilioni (Shilingi)									
Mapato	61.99	64.77	35.54	12.57	8.94	4.01	4.71	**16.24**	**15.01**	**223.79**
Matumizi										
Gharama za uzalishaji/uendeshaji	58.91	66.01	40.19	17.89	19.96	7.75	6.74	8.96	10.48	**236.9**
Gharama za Uendeshaji	22.18	19.10	20.72	14.64	12.02	10.36	8.14	8.01	8.6	**123.78**
Jumla ya Matumizi	**81.1**	**85.11**	**60.91**	**32.54**	**31.99**	**18.11**	**14.88**	**16.97**	**19.07**	**360.67**
Hasara	**-19.11**	**-20.34**	**-25.37**	**-19.96**	**-23.04**	**-14.10**	**-10.16**	**-0.73**	**-4.07**	**-136.88**

Takwimu 1: Mwenendo wa hali ya kifedha wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)



Moja kati ya vikwazo vilivyochangia kuporomoka kwa hali ya kifedha na kutokukopesheka kwa Shirika ni madeni makubwa yaliyopelekea kutokuwa na ufanisi. Mfano, mwaka 2014, Shirika lilikuwa na deni la Shilingi bilioni 140 na baada ya mazungumzo na wadai, deni likapungua hadi kufikia Shilingi bilioni 111.

Mapitio ya mpango mkakati wa Shirika kuwanzia mwaka 2015 mpaka mwaka 2020; mpango na makisio ya mapato na matumizi ya mwaka 2015/2016; pamoja na makisio ya fedha yaliyoandaliwa na Shirika kama mojawapo ya masharti ya kupata mkopo kutoka Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) wa kiasi cha Dola za Marekani milioni 20 yameonesha kuwa kulikuwa na tofauti kati ya taarifa hizo ukilinganisha na mpango mkakati unaotekelezwa na shirika katika kufikia malengo yake. Mpango mkakati wa shirika wa 2015/2020 unaainisha kwamba ili Shirika liwe na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake, linahitaji kununua ndege mpya au karibu na mpya ambazo ni Bombadier DHC8Q400 moja kwa gharama ya Dola za Marekani 24,500,000 na Boeing B737NG kwa gharama ya Dola za Marekani 80,000,000.

Kinyume na mpango mkakati huo, baada ya majadiliano na uongozi wa Shirika pamoja na mapitio ya andiko la mkopo, ilibainika kuwa Shirika limedhamiria kununua ndege nne zilizotumika ambazo ni Boing 737-500B mbili kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 4 kwa kila moja na CRJ200 mbili kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 3 kwa kila moja. Ndege hizi zitanunuliwa kwa kutumia fedha za mkopo wa Dola za Marekani milioni 20 unaotarajiwa kupatikana kutoka benki ya Benki ya Uwekezaji Tanzania.

Hakukuwa na ushahidi wowote wa kuthibitisha kuwa Shirika lilifanya tathmini na uchambuzi wa ndani ili kutambua athari za kubadilisha malengo kati ya yale yaliyoainishwa katika taarifa hizo mbili.

Kutofautiana kwa taarifa hizo mbili kunaweza kupelekea mkanganyiko ndani ya shirika katika kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Inatia shaka kutokana na mkwamo wa hali ya kifedha unalolikumba Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) tangu mwaka 2007. Hii inaashiria kuwa kuna udhaifu ndani ya Shirika katika kuweka mpango mkakati utakaopanua biashara yake ili liweze kufufuka kutoka kwenye mkwamo huo wa kifedha.

Mapendekezo

i. Serikali inashauriwa kufanya upembuzi yakinifu kati ya faida na hasara zinazoweza kupatikana kutokana na shughuli zozote za kibiashara zinanazohusisha ubinafsishaji pamoja na ushirikiano na sekta binafsi kabla ya kuingia mkataba wowote na sekta binafsi ili kuhakikisha maslahi ya umma yanalindwa.

ii. Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) inatakiwa kutengeneza mfumo, sera na mkakati wa usimamizi wa athari zinazoweza kujitokeza. Pia inapaswa kuwanzisha na kuendeleza regista ya vihatarishi ikiwa ni pamoja na

mapitio ya kila mwaka ili kuimarisha muundo wa uongozi unaoshughulikia vihatarishi. Pia, uongozi wa Shirika unashauriwa kuwandaa mpango wa utelelezaji ambao utaboresha utendaji kazi wa Shirika na kuwa wa kisasa zaidi.

iii. Kampuni ya Ndege Tanzania itengeneze mkakati utakaoliwezesha kurudi katika hali nzuri ya kifedha kwa kufanya tathmini ya kina kubaini sababu na matatizo yaliyopelekea kuwa na matatizo ya hali ya kifedha iliyopo, pamoja na kuboresha mifumo na namna ya kuendesha biashara hiyo ili kuwa na Shirika jipya lenye ufanisi na kujiendesha kwa faida.

iv. Kampuni ya Ndege Tanzania iweke utaratibu wa kuwajengea uwezo watumishi au kuwajiri watumishi wapya wenye sifa stahiki pamoja na kuwa na mpango wa kurithishana ujuzi kwa nafasi muhimu za uongozi wa Shirika ili kuwa na watumishi wasomi, wazoefu, waliohamasika na wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani katika soko linalokuwa kwa kasi la usafiri wa anga.

v. Kampuni ya ndege Tanzania (ATCL) linatakiwa kupata vyeti vyote kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Kimataifa (IATA) pamoja na ukaguzi wa usalama wa usafiri wa anga. Kulingana na taratibu na kanuni za uendeshaji wa makampuni yote ya ndege kufuata taratibu za usalama za usafiri wa anga.

vi. Ninapendekeza kuna ulazima Serikali iangalie changamoto zinazolikabili Shirika na kutafuta njia nzuri za kufanyia mageuzi Shirika la Ndege la Taifa na kuweka mfumo ambao utaliwezesha shirika kutoa huduma za kiushindani na pia kujiendesha kwa faida.

vii. Kampuni ya ndege Tanzania (ATCL) inatakiwa kufanya Tathmini ya kina na uchambuzi ili kutambua athari za kubadilisha malengo kati ya yale yaliyoainishwa kwenye

mpango mkakati wa mwaka 2015/2020 na kwenye andiko la mkopo kabla ya kuchukuwa mkopo huo kutoka Benki ya Uwekezaji Tanzania ili kununua ndege.

5.2 Mamlaka ya Udhibiti Wa Nishati Na Maji (EWURA)

Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Sura ya 414 na ilianza kufanya kazi Juni 2006 ikiwa ni Mamlaka inayodhibiti na kusimamia sekta mbalimbali za nishati na maji.

Mamlaka ina jukumu la kusimamia shughuli zote za kiuchumi na kitaalamu katika sekta ya nishati (umeme, petroli na gesi asilia) pamoja na sekta ya maji. Ukaguzi wa mwaka huu umebaini masuala muhimu ya usimamizi wa kimkakati ambayo Mamlaka inahitaji kuyatekeleza ili kuongeza ufanisi katika utendaji wake wa kazi

5.2.1 Kutokuwa na Ufanisi wa Kusimamia Vihatarishi Ndani ya Mamlaka.

Mfumo wa usimamizi wa vihatarishi na vyenye madhara ndani ya EWURA unalenga kutoa mwongozo wa kushughulikia vihatarishi na kutoa fursa kwa Menejimenti ya kupambana navyo kikamilifu ili kuimarisha uwezo wa Mamlaka kutimiza malengo yake. Mfumo wa usimamizi wa vihatari una lengo la kutoa mwongozo kwa Mamlaka juu ya mfumo wa usimamizi wa vihatari na kujenga utaratibu wa Menejimenti kufanya kazi kwa ufanisi katika mazingira yenye vihatarishi.

Nimebaini kwamba licha ya Mamlaka kuwa na mwongozo wa kusimamia vihatarishi tangu Aprili 2013, haijafanikiwa kuwanzisha na kuwandikisha rejista ya vihatarishi pamoja na kuwanzisha kamati ya kusimamia vihatarishi hivyo. Kamati ina jukumu la kutambua, kutathmini, kuweka vipaumbele, kuchukuwa hatua na kufuatilia viashiria vyote vya vihatarishi vinavyoikabili Mamlaka.

Mapitio zaidi ya utendaji wa kila mwaka wa sekta ya mafuta kwamba ulidhihirisha masuala kadhaa mathalani, Mamlaka haina mwongozo wa tathmini ya vihatarishi unaotumika wakati wa ukaguzi kusaidia timu ya wakaguzi wa vituo vya mafuta kuhusu utaratibu wa kutambua vituo hivyo na wasambazaji wa mafuta ili kubaini kama kuna ukiukaji wa utaratibu katika usambazaji wa mafuta. Hali hii inapelekea ukaguzi kufanyika bila mpangilio na mara nyingi ukitegemea malalamiko kutoka kwa wateja.

Kutokuwa na sera ya kutathmini vihatarishi pamoja na mwongozo wa kutambua wasambazaji wanaokiuka taratibu unaweza kusababisha kazi ya kufuatilia na kusimamia usambazaji wa mafuta kutokuwa na ufanisi, na hivyo kusababisha ukiukaji huo kutokupungua katika kiwango kinachokubalika.

5.2.2 Mapitio ya Taarifa za Utendaji wa Kazi kwa Sekta Zinazosimamiwa na EWURA

Ripoti za utendaji wa sekta zinazosimamiwa na Mamlaka huonyesha shughuli ambazo zinafanya na sekta husika. Shughuli hizo ni usimamzi na udhibiti wa umeme, petroli, gesi asilia, maji safi na majitaka. Ripoti hizo hutakiwa kujumuisha undani wa kazi zinazofanywa, mafanikio, changamoto zilizopompango mkakati wa kutatua changamoto katika mwaka husika.

Mahojiano na Menejimenti yalibaini kwamba kwa kawaida Mamlaka huandaa ripoti za utendaji kwa sekta ya mafuta ya petroli pamoja na maji safi na majitaka tu. Hali hii inaonyesha ripoti ya utendaji kwa sekta ya umeme na gesi asilia kutoandaliwa.

Kutoandaliwa kwa ripoti za utendaji kwa sekta ya umeme na gesi asilia kunapunguza uwezo wa Mamlaka kupima kwa ufanisi utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na sekta hizo. Pia iligunduliwa kuwa Mamlaka haikuwandaa mpango wa

utekelezaji kwa ajili ya kutatua changamoto walizokutana nazo wakati wa utekelezaji wa mpango kazi wa mwaka.

5.2.3 Mapitio ya Utaratibu wa Utunzaji wa Malalamiko

EWURA ina kitengo ndani ya Idara ya Sheria kinachoshughulikia malalamiko ya wateja dhidi ya sekta inazozisimamia. Kitengo hicho kina wajibu wa kutatua malalamiko yote kiliyoyaokea kutoka kwa walalamikaji ndani ya siku sitini (60) kuwanzia tarehe ya malalamiko hayo kupokewa.

Katika kipindi cha mwaka 2014/2015, EWURA imepokea kiasi cha malamiko 80 kutoka katika sekta tatu inayozisimamia, Mafuta ya petroli (16), umeme (48), maji safi na majitaka (16). Kati ya malalamiko hayo 80 ni malamiko 50 sawa na asilimia 62 yalitatuliwa. Menejimenti ilitoa taarifa kwamba mashauri yaliyobakia yapo katika hatua ya upatanishi na usikilizaji wa kesi. Pia kifungu 35(5) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ambacho kimeweka muda wa siku 60 kwa shauri kuwa imetatuliwa haifafanui kwa zaidi muda utakaotumika kuhitimisha shauri la malalamiko.
Hali hii inaleta shaka juu ya muda unaotumika kushughulikia malalamiko kwani unazidi muda wa miezi sita ambao umewekwa na Bodi ya Mamlaka kuwanzia siku ya kupokelewa kwake.

Mapendekezo

i. Menejimenti ya Mamlaka inapaswa kutekeleza uanzishaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi ikiwemo kuwanzisha rejista ya vihatarishi pamoja na kamati ya kusimamia vihatarishi ili kuhakikisha shughuli zote za Mamlaka zinafanya kazi na vihatarishi vinadhibitiwa.

ii. Menejimenti ya Mamlaka inapaswa kuwandaa, kuendeleza na kutathmini utaratibu wa kuwatambua

wasambazaji ambao wanakiuka taratibu za uendeshaji wa shughuli za mafuta.

iii. Menejimenti inashauriwa kuwanzisha na kuendeleza kwa mapana mpango unaopimika, unaotekelezeka na unaoendana na wakati. Mpango huo unapaswa kuelezea malengo muhimu ya Mamlaka na pia uhakikishe kwamba ripoti za utendaji kwa sekta zote zinazomimiwa na Mamlaka zinaandaliwa.

iv. Menejimenti inatakiwa kuhakikisha kuna utaratibu maalumu wa kuhakikisha kwamba malalamiko ya wateja yanatatuliwa ndani ya muda maalumu bila ucheleweshaji.

5.3 Kituo cha uwekezaji Tanzania (TIC)

Kituo cha uwekezaji Tanzania (TIC) ni taasisi ya muhimu inayoisaidia Serikali kuratibu, kuhamasisha, kutangaza, kusimamia na kusaidia shughuli za uwekezaji Tanzania. Pia ni kituo chenye jukumu la kuishauri serikali kuhusiana na shughuli zote za uwekezaji. Kituo hiki kinachukuliwa kuwa kitovu cha uwekezaji na wawekezaji wote ambapo wawekezaji wanaweza kupata huduma na taarifa muhimu zinazohusiana na uwekezaji nchini. Katika ukaguzi wa ufanisi katika utendaji wa kituo hiki nilibaini yafuatayo;

5.3.1 Tathmini na Ufuatiliaji wa Mfumo wa Uwekezeja Usiokuwa wa Ufanisi

Wakati wa ukaguzi tulifanya mapitio ya wawekezaji 45 ambao walikuwa wamepewa cheti cha uwekezaji na Kituo hiki. Lengo la kufanya mapitio hayo lilikuwa ni kukadiria na kupima kama Kituo kinatekeleza jukumu la kutathmini na kufuatilia uwekezaji na wawekezaji kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 17(10) cha Sheria ya Uwekezaji Tanzania ya Mwaka 1997. Nilibaini kwamba wawekezaji wanne (4) kati ya arobaini na tano (45) sawa na asilimia tisa (9) ndio waliotoa taarifa kwa kituo kuhusu viwanda vyao baada ya kuanza kufanya kazi. Hii inamaanisha kwamba wawekezaji 41 sawa na asilimia 91 hawakutoa taarifa kwa Kituo kuhusu

kuanza kwa shughuli zao za uwekezaji. Aidha niligundua kwamba Kituo hakikuchukuwa jukumu la kufuatilia ili kuhakikisha kwamba wawekezaji hao wanatoa taarifa hizo kwa kituo. Pia nilibaini kwamba Kituo cha Uwekezaji hakiwatembelei mara kwa mara wawekezaji ili kujiridhisha kama cheti cha uwekezaji kinatumika kama ilivyokubaliwa katika leseni zao. Sheria ya uwekezaji inamuagiza mmiliki wa cheti cha uwekezaji kutoa taarifa ya maandishi kwa Kituo pale anapoanza uwekezaji na baada ya hapo Kituo kitakuwa na jukumu la kutembelea na kuthibitisha uwekezaji huo. Kwa mujibu wa Menejimenti, mapungufu haya yalisababishwa na uhaba wa wafanyakazi katika kitengo cha kuwahudumia wawekezaji ndani ya Kituo.

Kutokana kushindwa kuwatembelea wawekezaji Kituo kinapata ugumu wa kuthibitisha kama misamaha yote inayotolewa na Kituo inatumika kama inavyotakiwa kwa mujibu wa leseni. Kulingana na sheria, mmiliki wa cheti anatakiwa kukijulisha Kituo kwa maandishi tarehe ya kuanza kwa uwekezaji na Kituo kuthibitisha kuanza kwa kazi.

Pia kituo kinashindwa kujua iwapo wawekezaji wanafanya shughuli zao za uwekezaji kama Kituo kilivyoruhusu na kulingana na mashartu ya lesseni zao za uwekezaji.

5.3.2 Ukosefu wa Mawasiliano Katika Taarifa za Kielektroniki Kati ya Kituo cha Uwekezaji(TIC) na Mamlaka ya Mapato(TRA)

Katika ukaguzi wa kazi zinazoendeshwa na Kituo cha Uwekezaji nilibaini kwamba kila mwekezaji ana jukumu la kupeleka orodha ya Vifaa vya Mradi ambavyo angeomba kupewa msamaha wa kodi na serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji ambapo Kituo kitawasilisha orodha hiyo kwa Mamlaka ya Mapato. Kwa kipindi cha Julai 2012 mpaka Juni 2015 Kituo klifanikiwa kuwandikisha miradi 2,095 ambayo yote ilipitishwa na Mamlaka ya Mapato kwa ajili ya kupata msamaha.

Nilibaini kwamba kituo hakina mfumo wa kielektroniki uliounganishwa moja kwa moja na Mamlaka ya Mapato. Hali hii inasababisha kushindwa kuwangalia na kuhakiki misamaha ya wawekezaji ili kujiridhisha kama misamaha hiyo imetolewa kwa usahihi kama ilivyowasilishwa na kituo kwa Mamlaka ya Mapato. Pia kituo kinashindwa kutathmini jinsi misamaha hiyo ilivyotumiwa na wawekezaji.

Hali hii ilisababishwa na kukosekana kwa randama ya makubaliano kati ya Kituo cha Uwekezaji na Mamlaka ya Mapato inayoelekezwa na maongozo wa mawasiliano kati ya taasisi hizi mbili za serikali.

Ukosefu wa muunganisho mawasiliano ya taarifa za kielektroniki kati ya kituo cha uwekezaji na Mamlaka ya Mapato kunaleta ugumu kwa kituo kufanya usawazishaji wa taarifa za misamaha waliyopewa wawekezaji.

5.3.3 Kutowasilisha Ripoti na Mapato ya Wawekezaji kwa Kituo cha Uwekezaji

Katika ukaguzi wangu nilibaini kwamba hakuna ripoti ya nusu mwaka ambayo mwekezaji yoyote aliwasilisha kwa Kituo kama ilivyoainishwa katika barua ya awali ya kupitisha mradi anayopewa mwekezaji kabla ya kupewa cheti cha uwekezaji. Barua ya awali ya kupitisha mradi inamtaka mwekezaji kuhakikisha anatuma ripoti ya maendeleo ambayo itatoa taarifa ya uwekezaji na utekelezaji kila baada ya miezi sita. Kati ya wawekezaji wote 45 tuliopitia taarifa zao hakukuwa na mwekezaji yeyote aliyepeleka taarifa hizo kwa Kituo. Hii ilisababishwa na wawekezaji kutotilia maanani jukumu lao la kupeleka ripoti hizo na Kituo cha Uwekezaji kutofuatilia na kuhimiza wawekezaji kupeleka taarifa husika.

Hali hii ya kutopeleka taarifa za utendaji inasababisha kituo cha uwekezaji kushindwa kutekeleza jukumu lake la kufuatilia kwa ufanisi shughuli zote zinazohusiana na uwekezaji

5.3.4 Ufahamu Mdogo wa Wawekezaji Juu ya Majukumu na Kazi Zinazofanywa na Kituo cha Uwekezaji.

Katika ukaguzi huu nilifanikiwa kutemebelea wawekezaji 29 ambao wamepokea misamaha ya uwekezaji kutoka Serikalini kupita Kituo cha Uwekezaji. Katika mahojiano yangu nilibaini kwamba wawekezaji hao hawana uelewa kuhusu kazi mbalimbali zinazofanywa na kituo cha uwekezaji. Nilibaini kwamba wawekezaji hawa wanashindwa kukitumia Kituo hiki kama inavyotakiwa kuratibu, kuhamasisha, kutangaza, kusimamia na kusaidia shughuli za uwekezaji Tanzania kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 5 cha Sheria ya ya Uwekezaji Tanzania ya Mwaka 1997.

Mbali na kazi zilizoonyeshwa katika kifungu cha 6 cha Sheria hiyo, Kituo kinatakiwa kuhamasisha kusaidia shughuli zote za kukusanya, kuchambua, kusambaza taarifa zote muhimu zinazohusiana na uwekezaji. Hii ni pamoja na kutangaza fursa mbalimbali zilizomo ndani ya nchi, kuwasaidia wawekezaji kupata leseni na vibali mbalimbali na kujiandikisha sehemu mbalimbali kama inavyotakiwa na sheria.

Hali hii inasababishwa na Kituo kutokuwa na matangazo kuhusu vivutio vinayotolewa na Kituo kwa wawekezaji waliopo na wawekezaji wapya ambao wanatamani kufanya uwekezaji nchini Tanzania.

Hali hii inaweza kusababisha Kituo kushindwa kufikia malengo yake makuu ambayo ni kuhakikisha huduma za uwekezaji zinapatikana pamoja na kuwa taasisi ya msingi inayoisaidia Serikali kuratibu, kuhamasisha, kutangaza, kusimamia na kusaidia shughuli za uwekezaji Tanzania. Pia, kituo kina jukumu la kuishauri Serikali kuhusiana na shughuli zote za uwekezaji.

Mapendekezo

I. Ninapendekeza Kituo cha Uwekezaji Tanzania kifanye yafuatayo

a. Kuwanzisha mfumo imara ili kuhakikisha wawekezaji wote wanatoa taarifa pindi wanapoanza shughuli zao. Pia, Kituo kinapaswa kihakiki miradi hiyo kabla ya kuanza shughuli.
b. Kujenga uwezo wa ndani ili kuweza kutembelea miradi na kuhakikisha misamaha iliyotolewa inatumika kulingana na kusudio lililopangwa.

II. Kituo kiwasiliane na Mamlaka ya Mapato kwa ajili ya kupata taarifa kamili za wawekezaji kwenye miradi ambayo kituo kinaweza kutumia wakati wa ufuatiliaji wa miradi hiyo.
III. Kituo kichukuwe hatua madhubuti dhidi ya wawekezaji wote watakaoshindwa kuwasilisha ripoti ya mwaka. Pia kiwape adhabu na vikwazo vingine wawekezaji hao.
IV. Kituo kinashauriwa kuelimisha jamii shughuli kinazozifanya kwa kutoa taarifa kamili kwa wawekezaji na kuwajulisha vivutio vyote vinavyopatikana nchini.

5.4 Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli

Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 4 ya Mwaka 2002. Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli ilichukuwa kazi, mali, na madeni ya lililokuwa Shirika la Reli la Tanzania. Kampuni hii inamilikiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Menejimenti na uendeshaji wa Kampuni hii unafuata randama ya Kampuni, sheria ya kampuni, na Sheria za Tanzania. Kampuni hii ilisajiliwa mnamo tarehe 3i Mei 2007 chini ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 na kupewa hati ya usajili namba 60587.

5.4.1 Mapungufu ya Mpango wa Utekelezaji wa Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli

Katika kipindi cha mwaka 2012/13 - 2014/15 Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli Tanzania ilikuwa na malengo yafuatayo.

I. Kufuatilia vizuizi vya mwendokasi kwa kilometa.

II. Kuongeza ukubwa/urefu wa mkongo wa taifa wa mawasiliano
III. Kuondoa reli za zamani na zilizoharibika na kuweka reli mpya ili kuongeza ufanisi.
IV. Kutumia mtaji unaotosheleza ili kuboresha miundombinu.

Katika kupitia repoti ya utendaji ya Kampuni kwa mwaka 2014/15 iliyokuwa imeelezea kwa kina shughuli zilizofanyika na mafanikio ya malengo yaliyowekwa tulibaini vitu yafuatayo.

Kampuni ilibainisha viashiria vine (4) vya utendaji ili kupima shughuli nne zinazoendana malengo ya kimkakati. Viashiria vya utendaji havikulenga namna matokeo tarajiwa yatakavyopimwa, bali vilikuwa ni maelezo ya jumla yanayofafanua malengo lakini havikueleza kwa kina jinsi malengo hayo yatakavyo fikiwa. Malengo ya Kampuni kwa kila kiashiria cha utendaji yalitelekezwa kwa kiwango Fulani kama inavyoelezwaa hapa chini;

Kampuni ililenga kuondoa vikwazo vilivyosababishwa na miundombinu mibovu pembezoni mwa njia ya reli. Hata hivyo, kampuni ilifanikiwa idadi ya kilometa zenye vikwazo vya kasi kutoka kilometa 139.2 mwezi Juni 2014 hadi kilometa 94.8 tu kufikia Juni 2015. Kwa kipindi cha miaka mitatu (2013-2015) kampuni haikuwa na lengo mahsusi.

Nilishindwa kuelewa namna gani Kampuni inaweza kufikia malengo yake wakati haikuwa imejiwekea malengo hayo. Pia, sikuelewa ni kwa jinsi gani viashiria vya kiutendaji vitapimwa wakati hakukuwa na malengo yeyote yaliyopangwa.

Pamoja na hayo, Kampuni ilidhamiria kubadilisha kutoka mkongo wa shaba kwenda mkongo wa taifa wa kioo ambao si rahisi kuharibiwa. Hata hivyo hapakuwa na mwendelezo wowote kuhusu uboreshaji wa kilometa za mkongo wa taifa. Tulibaini kuwa Kampuni iliweka malengo ya mwaka

2013 kufikia kilometa 120; 2014 kufikia kilometa 150 na 2015 kufikia kilometa 170 za mkongo wa taifa ulioboreshwa. Hata hivyo malengo hayo hayakufanikiwa katika miaka hiyo yote mitatu.

Kampuni ilikuwa na malengo ya kuondoa reli chakavu na zilizoharibika na kuweka reli mpya ili kuongeza ufanisi. Katika mwaka 2013, Kampuni ilikuwa na malengo ya kuweka reli yenye urefu wa kilometa 29, na mwaka 2014 reli yenye urefu wa kilometa 100. Hata hivyo Kampuni haikufanikiwa kuweka reli hizo.

Kampuni pia ilipanga kutumia kiasi cha mtaji wa Shilingi billioni 60.7 kwa ajili ya kuboresha miundo mbinu. Hata hivyo tulibaini kuwa mtaji kwa ajili ya matumizi hayo ulipungua kutoka kiasi cha Shilingi bilioni 29.4 kwa mwaka 2013 /2014 hadi Shilingi bilioni 11.2 kwa mwaka 2014/2015

Menejimenti ya Kampuni ilisema mapungufu hayo yametokana na upungufu wa ruzuku kutoka serikalini.

Mapungufu yaliyojitokeza wakati wa kupanga malengo ya kampuni na viashiria hafifu vya utendaji vinaweza kuwathiri uwezo wa kampuni kupima kwa ufanisi utekelezwaji wa malengo yake iliyojiwekea.

5.4.2 Kushindwa Kutekeleza Malengo ya Maendeleo

Kampuni ilikuwa na malengo ya kufanikisha maendeleo ya kiuchumi ambayo yalikuwa kwenye kanda tatu ambazo ni Kanda ya Kusini (Kanda ya Mtwara) ambayo inajumuisha Mtwara–Songea-Mbamba Bay (Liganga na Mchuchuma) kwa ajili ya Maendeleo ya makaa ya mawe; Kanda ya Kaskazini; Tanga-Musoma ikijumuisha Engaruka na Mradi wa reli Minjingu na Kuboresha ujenzi wa reli ya kati (Kanda ya Kati)

Tuligundua kuwa Kampuni ilikuwa inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kushindwa kwa Shirika la Reli Tanzania kulipa ada ya ardhi na malipo mengine

yanayo takiwa kulipwa kisheria; Mfuko wa miundombinu haukuwa ukifanya kazi; uwezo mdogo wa Kampuni Hodhi kujumuisha mipango mingine ya ziada; Kiasi kikubwa kuhitajika kwa ajili ya miundombinu ya reli. Pia Kampuni haikuwandaa mipango kwa ajili ya kutatua matatizo mbalimbali inayokabiliana nayo kwa ajili ya kutekeleza mpango kazi wa mwaka.

Kutokana na changamoto hizo, Kampuni ilishindwa kufikia malengo yake.Niliguswa na utendaji wa Kampuni kwa sababu changamoto hizi zinazuia utendaji wa kila siku wa kampuni katika kufikia malengo yake.

Nyaraka mbalimbali za Mamlaka ya Bandari Tanzania, zilionyesha kwamba pungufu ya asilimia moja (1%) ya mizigo ilikuwa inasafirishwa kupitia reli. Hii inaonyesha uwezo mdogo wa ufanyaji kazi wa Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli na Kampuni ya Reli kwenye kufanikisha malengo ya mda mrefu ya kuifanya reli iwe njia ya kuwaminika ya usafirishaji mizigo.

Mapendekezo

I. Menejimenti ihakikishe kuwa inatekeleza shughuli ilizozipanga kutokana na mpango wa kazi wa mwaka mzima na bajeti

II. Menejimenti ihakikishe inapima utendaji wake kwa kuwangalia changamoto zilizopo kwa wakati husika. Pia iandae malengo yanayojitosheleza, yanayopimika, ya muda maalumu, yanayofikika, pia yawe kwa ajili ya kufikia lengo la maendeleo yaliyokusudiwa.

5.5 Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)

5.5.1 Shirika Kutofanya Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Rasilimali kwenye Miradi Linayosimamia

Ukaguzi wa jumla wa michakato na uendeshaji wa miradi iliyo chini ya Shirika ulibainisha kwamba upembuzi yakinifu na tathmini ya rasilimali ya miradi minne (4) kati ya mitano (5) ilifanywa na makampuni ya ubia ambayo kwa kiwango

kikubwa yanamilikiwa na washirika binafsi. Gharama zote zinazohusiana na tafiti hizo hugharamiwa na wawekezaji binafsi kupitia makampuni ya ubia ambayo kwa kiwango kikubwa Shirika ina umiliki mdogo wa hisa.

Niligundua pia kuwa gharama za upembuzi yakinifu wa miradi minne (4) kati ya mitano (5) ambayo ni Makaa ya Mawe ya Mchuchuma & Chuma cha Liganga; Makaa ya Mawe ya Mhukuru na Ngaka Kusini; Makaa ya Mawe ya Maganga Matitu, na Mradi wa Kilimo cha Mchikichi na Uzalishaji wa Mafuta ya Mawese hazikuweza kupatikana kutokana na Shirika kutokuwa na utaratibu mzuri wa ufuatiliaji na uthaminishaji wa gharama za kampuni ubia. Kwa upande mwingine, mradi wa uzalishaji wa magadi wa Engaruka ulihitaji bajeti ya Shilingi bilioni 1.0 ili kugharamia upembuzi yakinifu na tathmini ya athari za kimazingira na kijamii ambazo Shirika halikuweza kugharamia.

Ni maoni yangu kuwa programu ya Ubia wa Umma na Sekta Binafsi ya Shirika haina kumbukumbu ya tafiti za upembuzi yakinifu wa maeneo mbalimbali ambayo miradi ya maendeleo inakusudiwa kuwepo ambayo ingeweza kutumika kama chanzo cha mapato, kivutio cha wawekezaji wanapokuja na kuongeza uwezo na ushawishi wa serikali kwenye nafasi ya uwekezaji.

Kukosekana kwa kumbukumbu za utafiti wa pembuzi yakinifu unalifanya Shirika la Maendeleo la Taifa kuwa na nafasi ndogo kwenye majadiliano ya mgawanyo wa rasilimali hivyo kusababisha miradi isitekelezeke bila kugharamiwa na wawekezaji binafsi.

5.5.2 Upungufu wa Fedha za Miradi

Kwa kipindi cha miaka minne (4) iliyopita Shirika la Maendeleo la Taifa limekuwa na nakisi ya bajeti ya Shilingi bilioni 109.5 ikilinganishwa na mahitaji yake kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:

Jedwali 11: Ulinganifu wa Bajeti na Kiasi Halisi cha Fedha kwa Kipindi cha Miaka Minne Iliyopita

Mwaka	Bajeti Iliyotakiwa	Bajeti Iliyopitishwa	Kiasi kilichopokelewa	Nakisi ya Bajeti
2011/12	33,758,000,000	7,063,835,401	2,900,000,000	30,858,000,000
2012/13	28,967,000,000	7,960,000,000	6,738,373,750	22,228,626,250
2013/14	49,141,800,000	19,900,000,000	13,128,180,000	36,013,620,000
2014/15	24,253,000,000	8,896,000,000	3,890,000,000	20,363,000,000
Jumla				**109,463,246,250**

Tathmini ya ufanisi wa bajeti na shughuli ya shirika umebaini kuwa licha ya miradi kadhaa kutekelezwa chini ya usimamizi wa NDC, hisa za serikali kwa sehemu kubwa zimebaki katika mfumo wa rasilimali zilizopo kwa ajili ya uwekezaji. Mchango mkubwa wa fedha za uwekezaji unafanywa na wawekezaji binafsi ambao kwa kiwango kikubwa wanabaki kuwa wamiliki wakubwa wa hisa za ubia za kampuni.

Mahojiano na uongozi wa Shirika yalibainisha ukosefu wa fedha kuwa chanzo cha Shirika kushindwa kuwa na hisa nyingi zaidi kwenye miradi mbalimbali kwa sababu hakuna fedha zinazotengwa kwa ajili ya uwekezaji wa moja kwa moja kwenye miradi husika.

Ninaamini, sekta binafsi inategemea taasisi za kifedha kupata fedha za kugharamia miradi ya Ubia wa umma na sekta binafsi. Kugharamia miradi hii kwa fedha za mkopo ni ghali kwasababu ya kiwango cha riba kinachowekwa na hivyo hupunguza ushiriki wa moja kwa moja wa serikali kwenye miradi ya ubia.

5.5.3 Kutotumika Kikamilifu kwa Kiwanda cha Vipuri cha Kilimanjaro (KMTC)

Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali namba 237 la tarehe 24 Aprili 2009, mali za Kampuni ya Magari (TAMCO) na Kiwanda cha Zana cha Kilimanjaro (KMTC) ziliwekwa chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa. Kiwanda kimekuwa

kikifanya kazi chini ya uwezo hivyo kufanya malengo husika kutofikiwa.

Ripoti za maendeleo ya Kiwanda zinaonyesha uwezo mdogo wa uzalishaji ambapo kutoka Julai 2014 hadi Novemba 2015 jumla ya mapato yaliyokusanywa yalikuwa Shilingi 77,198,032.22 ambayo ni kidogo ikilinganishwa na mpango wa kurejesha Shirika katika uzalishaji wa tija na faida wenye makadirio ya mapato ya jumla ya Shilingi 500,000,000 kwa mwaka.

Tarehe 16 Januari 2013, Shirika la Maendeleo la Taifa liliingia mkataba na mshauri Jackson G Majura kwa Shilingi 36,795,000 kwa ajili ya kuwandaa utafiti kabla ya upembuzi yakinifu na mpango wa kujerejesha kiwanda katika uzalishaji. Pamoja na mambo mengine, utafiti ulionyesha kuwa Shirika linahitaji kiasi cha Shilingi 3,100,000,000 ili kufanikisha uwekaji wa mashine ambayo ingetumika kuyeyusha vyuma ili kuweza kurahisisha utengenezaji wa vipuri mbalimbali. Uwekwaji wa mashine hii ungesaidia kuongezeka kwa uzalishaji na mauzo yatokanayo na uuzaji wa vipuri hivyo. Hata hivyo, hadi sasa hakuna fedha zilizopatikana na kutengwa kwa ajili ya ununuzi wa mashine hiyo.

Hadi mwisho wa zoezi la ukaguzi, jumla ya kiasi cha Shilingi 187,544,480 kilikuwa kimetumika kwa ukarabati wa majengo ya kiwanda kwa kuingia mkataba na kampuni ya G.E Engineering Co.LTD kwa mujibu wa mkataba uliosainiwa tarehe 26.08.2013.

Pia, hakuna mwekezaji aliyeonesha nia ya kuingia ubia na Shirika kwa ajili ya kuwekeza katika kiwanda hicho.

Upembuzi yakinifu wa kina unahitaji kufanyika kutathmini matarajio na mahitaji ya soko ili kuhakikisha ongezeko la thamani ya uwekezaji ambayo Shirika linauweka.

5.5.4 Kukosekana kwa Utaratibu wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Gharama za Ubia

Kanuni namba 46 (2) ya Sheria ya Ushirikiano wa Umma na Sekta binafsi ya Mwaka 2011 inaitaka mamlaka ya umma inayotafuta mbia kwenye mradi husika kuwandaa utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini ya gharama za ubia ambao unaundwa na mpango wa usimamizi wa mradi, vigezo vya utendaji, utaratibu wa kuripoti ukaguzi wa nje, uwasilishaji wa ripoti za taarifa za maendeleo, pamoja na uhakiki wa mali za miradi na mawasiliano na wadau.

Tathmini ya utaratibu wa miundo ya miradi inayotekelezwa chini ya ubia umebaini kuwa, ili kuhakikisha zoezi zima la ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo ya miradi inafanyika kwa wakati, Shirika ina muundo wa utawala wa makampuni ya ubia. Hata hivyo miongozo yake haitekelezwi na hivyo kudhoofisha jitihada za ufuatiliaji.

Aidha, muundo wa utawala hauakisi matakwa ya kanuni namba 46(2) ya sheria ya Ubia wa Umma na Sekta Binafsi ya Mwaka 2011. Pia,hakukuwa na mpango wa ufuatiliaji na tathmini wa gharama za ubia sambamba na majibu ya uongozi wa kampuni ya ubia kuonyesha zoezi la ufuatiliaji na tathmini ya gharama zilifanywa na Shirika.

Uongozi ulibainisha kuwa ukiacha miradi ya Liganga na Mchuchuma ambayo uongozi wa kampuni ya ubia ya Tanzania China International Mineral Resources Limited (TCIMRL) una muundo wa uongozi unaoruhusu Shirika kuwa na uwakilishi, Shirika la Maendeleo la Taifa linatumia taarifa za ukaguzi wa fedha na mkutano mkuu wa mwaka katika kufuatilia utendaji kazi wa makampuni ya ubia.

Ninaamini uwepo wa mpango wa ufuatiliaji na tathmini utawezesha kuboresha mipango kazi, gharama na mapato yaliyokusanywa ambavyo kwa ujumla wake yana nafasi muhimu katika kusimamia maendeleo ya miradi iliyopo na kwa ajili ya uboreshaji wa miradi ijayo.

Kutokuwepo kwa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kunasababisha kutokuwa na taarifa sahihi za maendeleo ya miradi ili kuhakikisha miradi inaendelea. Pia, mapato na matumizi ya mradi husika hayawezi kuthibitishwa na serikali kwa wakati. Hali hii inalifanya Shirika kutegemea taarifa zote zitoke kwa mbia mkubwa kupitia kampuni ya ubia ambayo kwa kiwango kikubwa inamilikiwa na mbia mkubwa. Hii inaathiri muda wa mrejesho wa mradi kabla ya kukabidhiwa kwa serikali.

5.5.5 Mapungufu katika Ununuzi wa Hisa za General Tyre (EA)

Vifungu No.2 (5) na 9 (14) vya makubaliano yaliyofikiwa tarehe 30 Aprili 2015 kati ya Serikali na Kampuni ya Continental AG kwa ajili ya ununuzi wa asilimia 26 ya hisa za Kiwanda cha General Tyre East Africa (GTEA) inazitaka pande husika kutoingia katika majadiliano yoyote mapya kuhusu mauzo ya hisa za Kiwanda ndani ya siku 90 baada ya tarehe ya mkataba. Aidha kama upande wowote hautalipa kwa wakati deni litaongezeka kwa riba kuwanzia tarehe ya malipo hayo yalipotakiwa kulipwa hadi tarehe ya malipo.

Ili malipo ya ununuzi wa hisa yenye thamani ya Dola za Marekani 1,000,000 yalipwe bila ongezeko la riba, yalitakiwa kufanyika si zaidi ya tarehe 30 Julai 2015.

Mnamo Julai 2015, Wizara ya Viwanda na Biashara na Msajili wa Hazina waliliruhusu Shirika kupata mkopo kupitia benki binafsi ili kufanikisha ununuzi wa hisa zilizokuwa zinamilikiwa na Continental AG. Baada ya mawasiliano na mabenki kadhaa ilibainika kuwa kama mkopo huo utatolewa, riba itakayoambatana na malipo hayo haitapungua Dola za Marekani 60,000 ikiwa malipo hayo yatalipwa kwa wakati. Kuchelewa zaidi kungesababisha ongezeko la kiasi cha riba. Ili kufanikisha mkopo huu, dhamana ya serikali pia ilihitajika.

Kutokana na muda wa kulipa bila riba kukaribia, ilikubaliwa malipo yatoke katika sehemu ya fedha za zuio la mradi wa viuatilifu vya Malaria lenye thamani ya Pauni za Uingereza

16,832,377.52 ambazo zilitarajiwa kurejeshwa kutoka Wizara ya Fedha kupitia bajeti ya mwaka. Jumla ya Dola za Marekani 1,000,000 ilihamishiwa kampuni ya Continental AG mnamo tarehe 30 Julai 2015 toka FDR No.13200236008 iliyofunguliwa na Shirika katika Bank ya Afrika (BOA).

Ukaguzi wangu umebainisha kuwa malipo hayo hayakurejeshwa licha ya juhudi za Wizara ya Viwanda na Biashara kuikumbushia Wizara ya Fedha kwa barua yenye kumbukumbu namba 111/188/01/82 ya tarehe 20 Agosti, 2015.

5.5.6 Mlolongo wa Maamuzi ya Serikali Unaochelewesha Uanzishwaji wa Miradi

a) Ucheleweshaji wa Tangazo la Serikali Linalokabidhi Mali za GTEA kwa Shirika la Maendeleo la Taifa

Kwa mujibu wa barua yenye kumbkumbu namba CAC 315/406/01 ya tarehe 28/5/2012 toka Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, umiliki wa Kiwanda cha General Tyre East Africa Limited (GTEA) ulihamishiwa katika Shirika la Maendeleo la Taifa kwa lengo la kukifufua na kukifanya kiendelee na uzalishaji.

Mapitio ya taratibu na mchakato uliopitiwa hadi kufanikisha mali za GTEA kuwekwa chini ya Shirika ulibainisha mapungufu ambayo yanatakiwa kushughulikiwa kabla ya kutafuta mwekezaji mpya.

Wakati wa ukaguzi, hakuna taarifa ya upembuzi yakinifu, tathmini ya mali wala thamani ya mali zilizopo zilizowasilishwa. Pia hadi ukaguzi unaisha, hakuna mwekezaji aliyeonyesha nia ya kuweka ubia na Shirika licha ya GTEA kuwa chini ya usimamizi wake tangu mwaka 2012.

Hata hivyo, hadi muda wa ukaguzi unaisha hakukuwa na tangazo rasmi la Serikali linalothibitisha umiliki kamili wa mali za GTEA kwa Shirika licha ya kiwanda kuwa chini yake kwa zaidi ya miaka mitatu (3). Hadi sasa, jumla ya Shilingi 380,666,820 zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa jengo la

kiwanda, ujenzi wa uzio na ukarabati wa vyoo kwa kuingia mkataba na kampuni ya Concrete Design LTD kufuatia mkataba wa tarehe 28/08/2012. Pia, jumla ya Shilingi 662,936,482 zilitumika kwa ajili ya usambazaji wa vifaa vya umeme kwa mujibu wa mkataba wa tarehe 28.06.2013 kati ya Shirika na Kampuni ya Urban and Rural Engineering Service LTD.

Taarifa ya tathmini ya masoko, mpango wa biashara, mapitio ya mali na utafiti wa ukarabati wa kiufundi vilifanyika ili kiwanda kiweze kuanza kazi mwaka 2017. Jumla ya Shilingi 23,445,797,000 zilihitajika ambazo hadi ukaguzi unakamilika Shirika lilikuwa bado inatafuta.

Kuchelewa utekelezaji wa miradi kunasababisha ongezeko la gharama za uzalishaji na kutofikiwa kwa malengo ya mradi husika kama ilivyopangwa.

b) Uchelewaji wa Uwekezaji Katika Shamba la Mpira kwa Zaidi ya Miaka Saba

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba CCB 63/406/01 ya tarehe 27 Machi 2009, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ilihamishia umiliki wa mashamba ya mpira ya Kalunga yaliyopo wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro na Kihuhwi yaliyopo wilayani Muheza mkoani Tanga kwa Shirika la Maendeleo la Taifa. Tangazo la Serikali namba 266 la tarehe 17.07.2015 lilitoka miaka takirbani saba (7) tangu mashamba husika yawekwe chini ya uangalizi wa Shirika. Shirika halikuwa na uwezo wa kisheria kutumia mashamba hayo kwa ajili ya uwekezaji hadi umiliki kamili ukamilike kupitia tangazo la serikali.

Aidha, hakuna upembuzi yakinifu uliofanywa kwa mashamba yote ya mpira yaliyo chini ya Shirika ulilowasilishwa wakati wa ukaguzi. Kwa mujibu wa ripoti ya tarehe 01/03/2013 ya uthaminishaji ardhi na mimea ilikadiria mpira kuishi miaka 32 ambayo inaundwa na miaka 7 ya kutozalisha na miaka 25 ya uzalishaji.

Hadi ukaguzi unakamilika, hakuna mwekezaji aliyepatikana kwenye mashamba yote, huku Shamba la Kalunga likiwa halina hati ya umiliki ardhi, Shamba la Kihuhwi lipo chini ya mwangalizi.

Kwa mujibu wa uongozi, uchelewaji wa tangazo la serikali, kutokuwepo kwa hati ya umiliki ardhi na uhaba wa fedha kufanya upembuzi yakinifu ni sababu zilizopelekea kuchelewa upatikanaji wa mwekezaji.

c) Kuchelewa kwa Miaka Mitatu Kuthibitisha Umiliki wa Ekari 4000 Inayopelekea Kutoanza kwa Mradi wa Uzalishaji wa Mafuta ya Mawese

Mradi wa uzalishaji wa mafuta ya mawese unahusisha ubia kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa na Kampuni ya NAVA Bharat Singapore PTY LTD, ambapo ununuzi wa ardhi ya ukubwa wa hekta 10,000 ulitirajiwa kufanywa na Shirika. Ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha mafuta ya mawese na uzalishaji wa megawati 10 za umeme wa mimea ulitazamiwa kufanywa na mbia binafsi, ambapo kwa ujumla wake upatikanaji wa lita milioni 58 za mafuta ya mawese zilitarajiwa baada ya mradi kuanza uzalishaji.

Hata hivyo, hadi ukaguzi unakamilika mradi ulikuwa haujaanza kufanya kazi kwa sababu ya urasimu wa taratibu za serikali zilizosababisha uchelewaji wa karibia miaka mitatu (3). Barua ya tarehe 06/12/2015 yenye kumbukumbu namba KSW/130/Vol III/1 toka Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe kwenda Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliyohusu ombi la kuhamisha ardhi yenye ukubwa wa hekta 4000 (kati ya hekta 10,000 zinazohitajika) katika eneo la Kijiji cha Kimala Misale kwenda Shirika la Maendeleo la Taifa. Ilichukuwa mwaka mzima kwa barua hii kujibiwa kwa mradi husika kukubaliwa na maombi hayo kupelekwa rasmi kwa Ofisi ya Raisi kwa barua yenye kumbukumbu namba LD/314579/21 kwa uthibitisho wa mwisho.

Sambamba na hilo, Shirika lilipokea barua yenye kumbukumbu Na. CEA 110/302/V/01/32 ya tarehe 29/12/2015 kutoka Ofisi ya Raisi ikilitaarifu kwamba barua imetumwa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe ili kupata taarifa sahihi kabla ardhi haijamilikishwa kwa mmiliki mpya kwa mujibu wa kifungu namba 114 (1) cha Sheria ya Ardhi na Vijiji inayoruhusu umilikishaji ardhi ya kijiji kwa matumizi ya umma.

Karibu miaka mitatu (3) imepita lakini Shirika bado halijapata uthibitisho wa umiliki wa ardhi ya ukubwa wa hekta 4000 liliyoomba hivyo kuongeza sintofahamu kwenye utekelezaji wa mradi. Taratibu za uombaji wa ardhi ya nyongeza ya hekta 6000 katika vijiji vya Dutumu na Madege haziwezi kuanza bila ombi lililopita la hekta 4000 kufanyiwa kazi ikiwamo ulipwaji wa fidia kwa wamiliki husika.

Ucheleweshaji wa umilikaji wa ardhi unasababisha gharama za fidia kuongezeka, na ucheleweshaji wa faida za mradi husika.

d) Uchelewaji wa Miaka Minne wa Maamumuzi ya Kudhamini Mkopo wa Mradi wa Uzalishaji wa Umeme wa Upepo

Tarehe 07 Februari 2013, Shirika la Maendeleo la Taifa, TANESCO na kampuni ya Power Pool East Africa walisaini mkataba wa ubia ulioanzisha kampuni ya Geo Wind Power Tanzania Limited kwa umiliki wa asilimia 60 kwa Shirika, asilimia 20 kwa TANESCO , na asilimia 20 kwa Power Pool East Africa kwa ajili ya uzalishaji wa umeme wa megawati 50.

Baada ya mafanikio ya upembuzi yakinifu na tathmini ya athari za kimazingira iliyofanywa na Power Pool East Africa, ombi kwa ajili ya mkopo wenye masharti nafuu wa dola milioni 136 kutoka Benki ya Exim ya China kufadhili mradi huo ulitolewa na Serikali kupitia Wizara ya Nishati na

Madini kama barua husika ya tarehe 16 Desemba 2011 inavyoelezea.

Mwaka mmoja baadaye, tarehe 19 Desemba 2012 Wizara ya Fedha ilikubali ombi na iliandika barua yenye kumbukumbu namba TYC/N/40/6 kwenda Exim Bank kuomba kupewa mkopo ambao ulikubaliwa kwa kiwango cha riba ya asilimia 1 na kulipwa ndani ya miaka 25.

Baada ya mchakato kuchelewa kwa miaka 3, Waziri Mkuu kupitia barua yenye kumbukumbu namba PM/P/1/569/31 ya tarehe 28 Machi 2015 alielekeza Wizara ya Fedha kukamilisha taratibu za mkopo haraka iwezekanavyo.

Hata hivyo, kutokana na kuchelewa kwa michakato ya Serikali na hasa udhamini wa Serikali, mnamo tarehe 26 Agosti 2015 Benki ya Exim (China) aliiandikia barua Wizara ya Fedha kuwainisha marekebisho mapya ya masharti ya mkopo kuwa na riba ya asilimia 2 na kulipwa ndani ya miaka 20.

Tarehe 5 Januari 2016, ikiwa ni miaka minne (4) tangu ombi la awali la Wizara ya Nishati na Madini kwenda Wizara ya Fedha, ilijibiwa kwa barua yenye kumbukumbu namba CEA 228/476 /V/4/1 kwa kuwajulisha wadau mbalimbali kwamba Serikali iliamua kutodhamini mradi huo hivyo Shirika ilitakiwa kutafuta vyanzo vingine vya fedha kwa ajili ya mradi huo. Kuchelewa kwa maamuzi haya kumesababisha kuongezeka kwa gharama za mkopo na kuchelewa kwa faida tarajiwa mbazo zingetokana na kukamilika mapema kwa mradi huo.

Uamuzi wa Serikali kuudhamini au kutoudhamini mradi ulitakiwa kufanywa mapema ili kupunguza ongezeko la gharama za mradi na hivyo kuboresha mahusiano baina ya sekta binafsi na umma hivyo kurahisisha utekelezaji wa miradi.

5.5.7 Utaratibu Usio Sahihi katika Kuwekeza Yuro Milioni 16.8 Kwenye Mradi wa Malaria

Tarehe 29 Aprili 2010 Shirika liliingia mkataba wa kubuni, kusambaza, kufunga, kupima na kuweka kiwanda cha uzalishaji wa viwatilifu na Maabara ya Kibaolojia na Kifamasia (LABIOFAM) wenye thamani ya Yuro 16,832,377.52. Lengo likiwa ni kupunguza malaria kufikia kiwango cha chini na hivyo kupunguza matumizi ya serikali kwenye ununuzi wa madawa na gharama nyingine zinatokana na mapambano dhidi ya malaria. Baada ya kukamilika kwa mradi wa LABIOFAM itatakiwa kuhamisha teknolojia na maarifa kwa Watanzania kwa miaka 10.

Ukaguzi ulibainisha kuwa, kabla ya mradi kuanza, Shirika la Maendeleo la Taifa halikufanya upembuzi yakinifu wala tathmini ya athari za mazingira ambapo tafiti hizo mbili zilifanywa mwaka 2010 na 2011 baada ya makubaliano ya awali na LABIOFAM kusainiwa.

Ukaguzi ulibainisha kuwa Shirika lilihamishia asilimia 90 ya fedha za mkataba kwa LABIOFAM bila dhamana ya usalama au utendaji kazi kama fidia ya mkataba ikitokea ukiukwaji wa vipengele vya mkataba husika. Asilimia 75 ya thamani ya mkataba kiasi cha Yuro 12,624,283.21 kilitumwa kupitia Benki Kuu ya Tanzania tarehe 15 Julai 2010. Asilimia 15 iliyobaki sawa na kiasi cha Yuro 2,524,856.63 kilihamishwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha kwenda LABIOFAM. Malipo yote yalihamishwa kupitia benki ya BICSA, ya Ayestaran y20 de Mayo, Havana, 10600, Cuba, kwa Swift code namba BIDCCUHHXXX kwenda akaunti namba 43323020024003 inayomilikiwa na LABIOFAM.

Pamoja na ufunguzi rasmi wa kiwanda uliofanyika tarehe 2 Julai 2015, hadi sasa kiwanda bado hakijaanza uzalishaji kutokana na hitilafu ya kiufundi iliyobainika wakati wa majaribio ya mitambo siku chache kabla ya ufunguzi rasmi.

Sambamba na gharama za matumizi mengine, Shirika bado inalipa mshahara kwa meneja wa mradi ambaye yupo

kwenye eneo la ujenzi wa kiwanda. Shirika pia lilianzisha kampuni ya Tanzania Biotech Products ambayo imeajiri wafanyakazi zaidi ya 130 ambao wanalipwa mshahara kila mwezi licha ya mradi kuchelewa kuanza uzalishaji.

Kwa mujibu wa makubaliano ya kukopeshana kati ya Serikali na Shirika yaliyosainiwa tarehe 9 Julai 2010, Shirika linatakiwa kulipa mkopo kwa mikupuo miwili kwa mwaka ili kufidia kiasi kilichokopwa pamoja na riba ya asilimia 11.7935 kwa mwaka kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 4.01 cha makubaliano. Pia, kwa mujibu wa kifungu cha 4.03 cha mkataba huo, malipo yote yalikuwa na kipindi cha msamaha cha miaka miwili (2) na malipo yote kwa ujumla yalitakiwa kufanyika ndani ya miaka kumi (10). Mkataba wa ujenzi ulitakiwa kukamilika ndani ya miezi kumi na tisa (19). Hata hivyo, hadi sasa miaka sita (6) imepita na hakuna malipo yoyote ya mkopo yaliyofanywa.

Kwa hali iliyopo hadi namaliza ukaguzi, mkandarasi ameshalipwa zaidi ya asilimia 90 ya gharama za mkataba, huku Shirika ikibaki na asilimia 10 tu ambayo ni fedha za zuio la mkataba.

Barua ya tarehe 20 Januari 2016 yenye kumbukumbu CA/137/339/08 inaonesha kuwa kuna hali ya kutokubaliana kati LABIOFAM na Shirika ambapo mkandarasi anadai matumizi yake kuongezeka hadi Dola za Marekani milioni 10 kitu ambacho hakikuthibitishwa na kupitishwa na Shirika licha ya kiwango cha juu cha gharama za ziada kwa mujibu wa mkataba kutotakiwa kuzidi asilimia 10 ya thamani ya mkataba ambayo ni Yuro 2,230,768.2.

Uongozi wa Shirika uliandika barua kwa Wizara ya Fedha kuomba kuongezewa muda wa ulipaji wa mkopo lakini hakuna jibu lililopatikana. Kwa mujibu wa Shirika, tangu Julai 2015 gharama zinazoendelea kutumika na makadirio ya mapato yaliyotarajiwa kupatikana na Shirika kipindi ambacho kiwanda hakijaanza kufanya kazi kumesababisha hasara ya zaidi ya Shilingi milioni 230 kwa mwezi tangu

Julai 2015. Hadi tarehe 31 Desemba 2015, kiasi cha Shilingi Bilioni 1.5 kinakadiriwa kupotea. Licha ya kutokubaliana kati ya Shirika na LABIOFAM, majadiliano bado yanaendelea ili kuhakikisha makubaliano yanafikiwa.

Kuchelewa kuanza uzalishaji wa kiwanda kunasababisha Shirika kulimbikiza gharama za riba ya mkopo, ambapo sambamba na kuendelea kudhoofika kwa Shilingi dhidi ya fedha nyingine za kigeni ikiwa ni pamoja na Yuro ambayo mkopo unatakiwa kulipwa, jumla ya gharama zitazidi kuongezeka. Pia, kuchelewa kiwanda kuanza uzalishaji kunasababisha ongezeko la madai ya wafanyakazi ambao wanalipwa bila uzalishaji wa kiwanda. Hii pia inasababisha kuchelewa kwa faida inayotarajiwa kutokana na kukamilika kwa mradi husika, ambayo inaweza kusababisha kupungua thamani ya mitambo au kupitwa na teknolojia.

5.5.8 Mapungufu katika Utekelezaji wa Mradi wa Mchuchuma na Liganga.

a) Uchangiaji wa fedha katika mradi wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 2.4.

Mnamo tarehe 21 Septemba, 2011, Shirika, Kampuni ya Sichuan Hongda (Group) Company Limited na Kampuni ya Tanzania China International Mineral Resources LTD (TCIMRL) zilisaini mkataba wa ubia wa kuendesha Kampuni ya Tanzania China International Mineral Resources LTD, ikiwa ni kampuni iliyoanzishwa kwa kusudi la utekelezaji wa miradi ya Mchuchuma na Liganga.

Kwa mujibu wa aya ya 2.9 ya mkataba, Sichuan Hongda (Group) Company Limited ilikubali kuchangia kiasi cha pesa kisichozidi Dola za Marekani milioni 600 ikiwa ni mtaji kwa TCIMRL, ili zitumike kulingana na maendeleo ya utekelezaji wa mradi. Kwa kuongezea kampuni itatafuta mkopo wa kuweza kufikisha makusanyo ya Dola za Marekani bilioni 2.4, utakaodhaminiwa na mali za kampuni ya ubia zitazojumuisha haki za uchimbaji zinazomilikiwa na

kampuni ya ubia zenye uhusiano na mradi na udhamini wa Hongda.

Baada ya kupitia mchakato na usimamizi wa uendeshaji wa shughuli za Shirika imebainika kwamba hakuna utaratibu uliowekwa wa kuhakiki na kuthibitisha kiasi cha pesa kilichotolewa na Hongda hadi sasa kama sehemu ya mtaji iliyokubali kutoa wa Dola za Marekani milioni 600 kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa mradi. Namna pekee ya kupata taarifa ni kwa kuhudhuria mkutano mkuu wa mwaka na ripoti ya ukaguzi wa hesabu ya mwaka ambayo inakuja baada ya mwaka kuisha na miamala imeishafanyika. Ripoti hizi haziwezi kulihakikishia na kulithibitishia Shirika kwamba miamala iliyofanyika inakubalika kwa mujibu wa mkataba wa ubia ulioingiwa na ambayo ni sehemu ya mtaji ulioingizwa.

Kwa kuongezea, baada ya kupitia mkataba wa ubia imebainika kwamba, Sichuan Hongda (Group) Company Limited inamiliki asilimia 80 ya hisa za TCIML wakati asilimia 20 inamilikiwa na Shirika. Uchangiaji wa ziada wa kiasi kisichozidi Dola za Marekani bilioni 2.4 utadhaminiwa na mali za kampumi ya ubia zikijumuisha haki za uchimbaji za mradi badala ya rasilimali za Hongda Sichuan (Group).

Ni maoni yangu kuwa, mgawanyo wa hisa unahusisha wajibu wa masuala ya kifedha. Hivyo, kama mkopo unadhaminiwa kwa rasilimali za Tanzania, Shirika kwa niaba ya serikali lilipaswa kuwa mwanahisa mkuu wa TCIMRL kulingana na thamani ya rasilimali ambazo hazijatumika zenye thamani zaidi ya kiasi cha fedha ambayoo ilikubaliwa Hongda Sichuan (Group) achangie.

Kukosekana kwa utaratibu wa kuhakiki na kuthibitisha gharama za matumizi ya mwekezaji wa mradi, kuna matokeo hasi kwenye muda wa marejesho pamoja na gharama ambazo Shirika lilizitumia kwa kuzingatia gharama zote zilizotumika na mwekezaji huchukuliwa kama gharama

anazotakiwa kurejeshewa kutokana mapato yatokanayo na uzalishaji.

b) Kazi Ambazo Hazijatekelezwa za Mradi wa Mchuchuma na Ligannga.

Baada ya kupitia kazi zinazotakiwa kutekelezwa na pande zote mbili za ubia katika kufanikisha utekelezaji wa miradi ya Mchuchuma na Liganga kama ilivyoelekezwa katika mkataba wa ubia, tulibaini mapungufu yafuatayo:

i. Kutolipwa Faidia ya Shilingi bilioni 13.31 kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Mchuchuma na Liganga ya Umeme wa Makaa ya Mawe na Liganga.

Katika mapitio yetu tumebaini kwamba fidia na ripoti ya uthamini iliyofanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa (Idara ya Uthaminishaji) ya mwezi wa nane, 2015 ya mradi wa umeme wa makaa ya mawe wa Mchuchuma ya Shilingi bilioni 4.472 na mradi wa chuma wa Liganga wa Shilingi bilioni 8.836 kwa lengo la kufidia wakazi wa eneo linalozunguka mradi iliwasilishwa Shirikani kwa ajili ya utekelezaji.

Hata hivyo, mpaka sasa ni miezi sita toka ripoti ya uthamini imewasilishwa na Shirika halijaanda utaratibu wa kulipa fidia. Ucheleweshaji huo unapelekea kuongezeka kwa gharama za fidia kuendana na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Umiliki wa Ardhi Na. 47 ya mwaka 1967.

ii. Ucheleweshaji wa Kutia Saini Randama ya Makubaliano na Mkataba wa Manunuzi ya Umeme Kati ya Shirika la Umeme Tanzania, Shirika la Maendeleo la Taifa na Kampuni ya Ubia.

Katika mapitio ya mradi wa Mchuchuma na Liganga ilibainika kwamba hapakuwa na makubaliano yaliyofikiwa kati ya Shirika la umeme Tanzania, Shirika la Maendeleo la taifa na Kampuni ya Ubia kuhusiana na randama ya makubaliano na mkataba wa manunuzi ya umeme wa megawati 600.

Majadiliano yamesitishwa mpaka hapo TANESCO itakapofanya Uchunguzi wa kina juu ya Hongda Sichuan (Group) ingawa uchunguzi kama huo ulishafanywa na Shirika la Maendeleo la Taifa katika michakato yake ya mwanzo ya mradi.

Mbali na hayo, imegundulika kwamba TANESCO imependekeza majadiliano ya mkataba wa manunuzi yaanze mwezi Januari, 2017 baada ya kukamiilisha upembuzi yakinifu wa njia ya kusafirisha umeme ya kuwanzia Mchuchuma mpaka Makambako. Kama ratiba iliyopendekezwa itafuatwa, itapelekea ucheleweshwaji wa utekelezaji wa mradi na hivyo kuongeza gharama za mradi.

Kuwepo kwa vizingiti visivyo vya lazima kunapelekea kuwepo kwa ucheleweshwaji wa utekelezaji wa mradi usioendana na mpango kazi uliopo kwenye mkataba hivyo kuongeza gharama. Urasimu uliopitiliza katika mchakato mzima wa utekelezaji wa mradi unaweza kuongeza gharama kwa serikali.

Mapendekezo

I. Menejimenti inashauriwa kutafuta njia mbadala za kupata fedha za kuweza kuendesha stadi zake katika nyanja mbalimbali. Kuwa na taarifa za awali za akiba ya rasilimali kutaongeza nguvu ya majadiliano na umiliki wa hisa kwa serikali katika makubaliano ya mikataba ya ubia.

II. Ili Shirika la Maendeleo la Taifa liweze kuvutia wawekezaji na serikali kupata nafasi katika miradi ya ubia wa umma na sekta binafsi, ni lazima kiasi cha fedha kitengwe na kushiriki katika shughuli za utekelezaji wa miradi katika mkataba wa ubia ili kuongeza ushiriki wa serikali na umiliki wa hisa katika miradi husika.

III. Shirika la Maendeleo ya Taifa linatakiwa kutafuta fedha za kununua mashine ya Foundry ambayo itakiwezesha kiwanda kuzalisha kwa ufanisi.

IV. Menejimenti inashauriwa kutengeneza sera ambayo itatoa mwongozo katika zoezi zima la ufuatiliaji na tathmini ya miradi kama inavyotakiwa na Kanuni na. 46 (2) ya Kanuni za Manunuzi za Mwaka 2013.
V. Shirika la Maendeleo la Taifa lazima liimarishe mchakato mzima wa ufatiliaji na uthaminishaji kwa kuongeza kifungu ambacho bila kujali idadi ya hisa ambazo Shirika linamiliki katika mikataba ya ubia, mara kwa mara lazima kupitia na kupitisha ripoti za mapato na matumizi ya kampuni ya ubia ili kuhakikisha hakuna ongezeko la gharama na kupunguza mapato kwa ajili ya malipo ya mrahaba, kodi na mgawanyo wa gawio.
VI. Serikali inashauriwa kutoa fedha zinazohitajika kuwezesha Shirika la Maendeleo la Taifa kupata umiliki wa uendeshaji wa Kiwanda cha Tairi cha General Tyre (EA).
VII. Serikali inashuriwa kuongeza kasi katika mchakato wa Kiwanda cha Tairi cha General Tyre (EA) ilikuwa kwenye nafasi nzuri ya kuvutia wawekezaji.
VIII. Stadi za upembuzi yakinifu na upatikanaji wa rasilimali pamoja na tathmini ya mali ni muhimu zifanyike ili kubaini masoko, mwekezaji na mahitaji ya rasilimali za kufufua kiwanda.
IX. Serikali inashauriwa kufuatilia kwa haraka mchakato wa kumilikisha mashamba makubwa ya mpira kwa Shirika la Maendeleo la Taifa ili kuiwezesha kuvutia wawekezaji.
X. Serikali inashauriwa kuratibu shughuli zote za wizara ili kuepusha ucheleshwaji usio wa lazima, Kama ilivyo sasa mwekezaji kulipia gharama zote za mradi, hatua madhubuti zichukuliwe kabla mwekezaji hajajitoa katika mradi kama inavyoweza kuwa ngumu katika suala la muda na kutenga kiasi cha pesa cha kumpata mwekezaji mwingine mwenye nia ya kuwekeza.
XI. Serikali inashauriwa kufanya maamuzi kwa wakati muafaka ili kuepukana na ongezeko la gharama za

miradi zisizo za lazima na hivyo kuchelewa kupata manufaa yaliyotarajiwa katika miradi.

XII. Kama Shirika la Maendeleo la Taifaa bado inaona mradi una manufaa, inabidi kushirikiana na wanahisa wengine kwa kuwangalia vyanzo vya nje vya fedha kabla ongezeko la gharama halijakwamisha mradi.

XIII. Menejimenti inashauriwa kuikumbusha serikali kupitia Wzara ya Mambo ya Nje kufanya mawasiliano na serikali ya Cuba kuona namna ya kutekeleza mradi bila ya kuongeza gharama nyingine.

XIV. Menejimeti inashauriwa kuwasiliana na serikali na kukubaliana juu ya masuala ya malipo ya mkopo baada ya kuanza kwa uendeshaji wa mradi.

XV. Tathmini inapaswa kufanyika ili kubaini fursa, hali ya soko ili kutambua iwapo mradi una manufaa ili kuweka utaratibu mzuri wa kurejesha mkopo.

XVI. Menejimenti inashauriwa kuchukuwa hatua za haraka kwa kuweka utaratibu madhubuti wa kusaidia uthaminishaji na ufuatiliaji wa gharama zilizotumika katika mradi na mapato yanayotarajiwa.

XVII. Menejimenti inashauriwa kufanya tathmini ya uwezekano wa kuhakikisha kuwa serikali haipo katika hatari kwa kuingia makubaliano na washirika wa sekta binafsi. Iwapo hakuna njia mbadala ya kudhamini mkopo zaidi ya hati za uchimbaji za mradi kama ilivyopendekezwa katika mkataba, basi asilimia za umiliki zinapaswa kubadilika.

XVIII. Menejimenti inashauriwa kutafuta fedha na kuwalipa mara moja fidia raia wote waliohamishwa ili kuepuka madai yoyote hapo baadaye.

XIX. Tunapendekeza kuwa Shirika la Maendeleo la Taifa iwasiliane na menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania ili kuweza kuwanzisha mjadala ambao utasaidia pande zote mbili za ubia kufikia muafaka mzuri wa mkataba wa manunuzi ya umeme.

5.6 Shirika la Ugavi wa Umeme (TANESCO)

5.6.1 Mapitio ya faida ya kampuni na ufanisi katika uendeshaji.

Nimebaini kuwa kampuni haijaandikisha faida halisi licha ya kurekodi maboresho katika maeneo mengine wakati wa kipindi cha sasa kama ifuatavyo:

Kiasi	Miezi 18 kufikia 30.06.2015	Miezi 12 kufikia 31.12.2013	Miezi 12 kufikia 31.12.2012
	Shilingi 'Milioni	Shilingi 'Milioni	Shilingi 'Milioni
Mauzo	1,957,756	993,525	820,436
Faida /(hasara)	186,414*	(483,990)	(342,001)
Faida ya uendeshaji/(Hasara)	263,462*	(386,653)	(175,568)
Hasara	(35,123)	(467,704)	(178,454)
Hasara ya Jumla	(1,573,476)	(1,450,380)	(982,676)
Viashiria vya Utendaji			
Ongezeko la mapato kwa mwaka	40%*	13.80%	50.40%
Uwiano uliopo	0.81*	0.66	0.48
Uwiano wa madeni na mtaji	1.40*	1.51	0.6

Nilitaarifiwa na menejimenti kuwa, Shirika limekuwa ikipata hasara itokanayo na gharama za uzalishaji kuwa kubwa ikilinganishwa na bei ya mauzo ya umeme unaozalishwa na wazalishaji binafsi na wazalishaji wa umeme wa dharura.

Menejimenti imekiri kwamba, Shirika lipo kwenye mchakato wa kuhama kutoka uzalishaji unaotumia mafuta kwenda unaotumia gesi zaidi katika mitambo yake. Pia mitambo mipya ya uzalishaji wa umeme inayotumia gesi kama Mtambo wa Gesi Ubungo I, Mtambo wa Gesi Ubungo II na Mtambo wa Gesi Kinyerezi ipo katika jitihada za kuiokoa Kampuni kutoka kwenye gharama za mafuta.

Kwa mujibu wa maelezo ya menejimenti, Shirika llimetekeleza miradi mbalimbali iliyogawanywa katika

makundi ya muda mfupi na muda wa kati ili kuboresha utendaji kama ifuatavyo:

I. Ujenzi wa mtambo wa uzalishaji wa umeme wa megawati 150 unaotumia gesi, utakao simikwa Kinyerezi I;

II. Ujenzi wa mtambo wa uzalishaji wa umeme wa megawati 240 unaotumia gesi, utakao simikwa Kinyerezi II;

III. Ujenzi wa awamu ya kwanza ya mtambo wa uzalishaji wa umeme wa megawati 300 unaotumia gesi, utakaosimikwa Kinyerezi III;

IV. Utekelezaji wa mradi wa kusafirisha umeme (Backbone Transmission Investment Project- (BTIP)) unaoendelea. Hasa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa kilovoti 400 na kituo kidogo cha kupooza umeme kutoka Iringa hadi Shinyanga.

V. Ukarabati wa kituo kidogo cha kupooza umeme na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na kituo kidogo cha kupooza umeme kilichopo Dar-es-salaam ambacho kinafadhiliwa na serikali ya Japani kupitia Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japani; na

VI. Mpango wa kuongeza idadi ya wateja ili kuongeza mapato ya mwaka

Kwa mujibu wa maelezo ya menejimenti, miradi iliyotajwa hapo juu hususani kwa mitambo mipya itaongeza kiwango cha umeme kwa ajili ya mauzo na kuongeza mapato, kupunguza utegemezi wa wakopeshaji, kuwa na umeme wa uhakika. Kwa kuongezea, Shirika linatarajia kupunguza madeni kupitia akaunti maalumu ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya muda mrefu na kuwachana na uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta badala yake kuzalisha umeme kwa kutumia gesi.

Kwa hali hiyo, hasara zinazidi kutafuna mtaji wa Shirika na kupelekea ongezeko la vihatarishi vya ukwasi katika Shirika na kupunguza uwezo wake kutekeleza kazi zake kwa ufanisi. Pia suala hili lina matokeo hasi kwa uwezo wa Shirika kukopa katika soko.

Menejimenti inatakiwa kuendelea kuchukuwa hatua stahiki za mda mfupi na mrefu katika kuhakikisha kwamba uwezo wa kifedha wa Shirika unaboreshwa kwa kutambua vikwazo vinavyorudisha nyuma ufanisi wake.

5.7 Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA)

Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania imepewa majukumu ya kusimamia watu na taasisi ambazo zinafanya shughuli ya utoaji wa huduma za usafiri wa anga, elimu ya masuala ya usafiri wa anga katika viwanja vya ndege na uongozaji wa anga na vilevile kutoa huduma ya uongozaji Ndege katika anga la Tanzania.

Katika mapitio ya utendaji wa kiufanisi wa Mamlaka nilibani kuwa kulikuwa na mapungufu yafuatayo ambayo yanahitaji kuzingatiwa na Mamlaka katika utendaji wa majukumu na kufikia malengo yake kikamilifu.

5.7.1 Ukosefu wa Mpango Mkuu (Master Plan) wa Anga ya Nchi

Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO) linasimamia utekelezaji ulimwenguni katika mawasiliano, uongozaji vyombo vya anga, uchunguzi wa anga na usimamizi wa mwenendo wa ndege angani. Katika mahojiano na utawala wa Mamlaka, ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) haina Mapango Mkuu. Kuwepo kwa Mpango Mkuu kungewezesha Mamlaka kufahamu mabadiliko ya kiteknolojia yatokanayo na mikakati ya kiuwekazaji katika Mamlaka ya Anga. Hivyo, ukosefu wa Mpango Mkuu wa kunaifanya Mamlaka kukabiliwa na athari zifuatazo;

i. Mamlaka kutoweza kusimamia utekelezaji wa mawasiliano, uongozaji wa ndege angani, na uchunguzi wa anga na mfumo wa usimamizi wa mienendoya

ndege angani katika eneo la Afrika Masharika na kwa nchi zinazopakana nazo.

ii. Mapungufu katika usimikaji wa "Automatic Dependent Surveillance Broadcast" iliyosababishwa na mpango mbovu katika ushughulikiaji wa mradi ikiwemo upembuzi yakinifu na uchunguzi wa awali na vile vile katika kufanya mchanganuo wa gharama za mradi.

iii. Ugumu wa kupata miundombinu ya kisasa ya CNC/ATM. Pia ili kufanikisha malengo katika usalama na uongozaji ndege, miundombinu na uwezo ikilinganishwa na mifumo iliyopo.

5.7.2 Mapitio ya Mipango na Utendaji wa Menejimenti katika Mradi

Mamalaka ya Usafiri wa Anga ina jukumu la kulinda matumizi ya anga la Tanzaniaa kwa madhumini ya kuongoza Ndege. Mamlaka inapata asilimia 51 ya mapato yake kutokana na huduma za uongozaji ndege. Mapitio ya uwezo wa Mamlaka hivi sasa katika kutoa huduma za uongozaji ndege na juhudi zinazofanyika na Mamlaka katika kuboresha uwezo wake wa utoaji huduma yamebaini kuwa kuna umuhimu wa utoaji huduma za uongozaji ndege kwa mdhibiti nyendo za ndege ambaye anapaswa kuwa na uwezo wa kuwasiliana na marubani katika ndege ambazo zinahitaji huduma ya uongozaji ndege. Pia nilifahamishwa na Mamlaka kuwa kutokana na ukosefu wa uwezo wa kutosha, miundombinu ya mawasiliano ya redio iliyotumika itawekwa ili kuwezesha mawasiliano kati ya mdhibiti wa mienendo ya ndege na marubani.

Mamlaka ya Usafiri wa Anga iliingia mkataba na Kampuni ya Ujeruman COMSOFT GmbH kuleta mfumo wa Kuratibu na Kuongozea Ndege (Automatic Dependency Surveillance Broadcast) katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ingeleta mfumo wa ADSB katika tasnia ya mashariki na awamu wa pili ingeleta mfumo wa ADSB katika tasnia ya magharibi. Awamu ya kwanza ya mfumo wa ADSB ilimalizika lakini ikiwa na mapungufu katika utoaji wa huduma.

Zaidi ya hayo muuzaji na mkandarasi wa mfumo huu wa ADSB hivi karibuni alitangaza kufilisika. Kwahiyo, baadaye Kampuni haitokuwa na uwezo wa kutoa msaada katika mfumo huo na kuufanya mfumo kuwa wa kizamani kama ilivyo kwa mfumo wa rada Mfumo huo haujaweza kupitishwa katika uendeshaji wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga wa Tanzania.

Zaidi niliweza kubaini kwamba mchakato wa kuwanzisha, kutekeleza, na ufungaji wa mradi ulifanyika katika msingi wa dharula na hivyo kukosekana kwa kumbukumbu za awali za hitaji la kuwanzishwa kwa mradi huo ambao umepitishwa na Menejimenti kwa ajili ya kuwanzishwa kwake.

Mapungufu yaliyobainishwa yanayopatikana na kukosekana kwa utawala na usimamizi wa utendaji wa miradi katika mamlaka. Pamoja na uwezo duni wa Mamlaka kuhusiana na mipango ya teknonlojia.

Mapendekezo

i. Menejimenti inashauriwa kufanya mapitio ya faida ya mradi wa ADSB na kuzingatia athari za kufilisika kwa muuzaji wa mfumo huo na gharama kamili zinazohitajika kuleta rada zenye uwezo kwa kutumia mfumo wa ADSB
ii. Uongozi pia unashauriwa kutengeneza mipango ya teknolojia ambayo itawajibika kwa uchunguzi na kipimo cha faida ya teknolojia kabla ya teknolojia mpya haijaweza kutumia na Mamlaka ya Usafiri wa Anga.

5.7.3 Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania

Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania ni Mamlaka inayojitegemea yenye wajibu wa kusimamia sekta ya mawasiliano na utangazaji Tanzania. Mamlaka ni taasisi iliyoanzishwa kisheria ikiwa ni sehemu ya sera ya mageuzi katika sekta ya mawasiliano ikiwa ni lengo la kuboresha upatikanaji wa taarifa za huduma za mawasiliano kwa

umma. Lengo linguine la uanzishaji kuruhusu wadau wapya kuingia katika soko.

Katika mapitio ya mpango kazi na ripoti za ufanisi za Mamlaka kwa mwaka 2014/2015 imebainika kuwa baadhi ya kazi ambazo zilizowekwa katika mpango kazi zilikuwa hazijatekelezwa au kufanyika kama zilivyopangwa. Pia, nimebaini kuwa baadhi ya shughuli ambazo zilikuwa zitekelezwe na Mamlaka zilikosa viashiria vya ufanisi, msingi na malengo.

Vilevile tulibaini kuwa, Mamlaka haikuwandaa mpango kazi kwa kuwanisha changamoto ambazo inakumbana nazo na jinsi ufanisi wa kazi utakavyopimwa.

Kutotimiza mpango kazi uliotakiwa kutekelezwa katika mwaka husika kunaweza pelekea kuzuia Mamlaka kutimiza mikakati ya malengo yake muhimu. Pia, kukosekana kwa viashiria vya ufanisi, msingi na shabaha kwa kazi zilizotakiwa kutekelezwa, Mamlaka inaweza kutokuwa katika nafasi ya kupima ufanisi halisi wa kazi zilizotekelezwa kulingana na malengo. Hivyo Mamlaka inaweza kushindwa kupata mafanikio ya malengo yaliyokusudiwa.

5.7.4 Kushindwa Kufanya Upembuzi Yakinifu Kabla ya Utekelezaji wa Mradi wa TTMS

Umbembuzi yakinifu unalenga katika mantiki na malengo ya kuvumbua faida na hasara, fursa na hatari zilizomo katika mzingira ya mradi uliopendekezwa, mahitaji ya rasilimali katika uendeshaji wa mradi; na matarajio ya mafanikio ya mradi.

Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania imeingia katika makubaliano na Kampuni ya Societe Generale de Surveillance (SGS) kuendesha Mradi wa Mfumo wa Usimamizi wa Nyendo za Mawasiliano ya Simu (TTMS) kwa utaratibu wa kujenga, kuendesha na kuhamisha.

Kiambatanisho Na. VII cha mkataba kinaelezea gharama ya uwekezaji za mradi zilizonyesha kuwa upembuzi yakinifu na utafiti wa mazingira zilikuwa ni sehemu ya gharama za mradi yenye thamani ya Dola za Marekani 100,000. Hata hivyo, sikuweza kupewa ripoti iliyotolewa kuthibitisha kuwa umbembuzi yakinifu na utafiti wa mazingira ulifanyika kabla ya mradi kutekelezwa.

Vilevile, sikuweza kupata ushahidi kuthibitisha kuwa hitaji la kuwanzishwa kwa mradi iliandaliwa kwa ajili maamuzi ya kutekeleza mradi husika. Bila kuwa na upembuzi yakinifu kuna hatari kuwa mradi ulitekelezwa bila kuwangalia mahitaji ya Mamlaka na wadau wengine.

5.7.5 Kuwanzisha Mpango wa Ufuatilia Mauzo ya Muda wa Mawasiliano (ARMS)

Mpango wa ufuatiliaji wa mauzo ya muda wa mawasiliano unaruhusu uanzishaji wa mfumo wa kutambua mapato yanayotokana na matumizi ya mawasiliano kwa wateja. Katika kipindi cha mwaka 2014 iliundwa kamati ya kutoa mapendekezo na kufanya vikao vya majadiliano na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Mawasilaino Tanzania (TCRA), Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, pamoja na Wizara ya Fedha ili kukubaliana kwa pamoja namna ya uanzishaji wa mfumo huo.

Katika kupitia mapendekezo yaliotolewa na kamati, nilibaini kuwa mapendekezo hayo yanatilia msisitizo ushirikishwaji kamili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika makubaliano ya Mfumo wa Ufuatiliaji Mwenendo wa Mawasiliano ya Simu (TTMS) kama mdau muhimu na kuchukuwa jukumu la manunuzi ya mfumo huo na kuingia mkataba na mshauri wa mfumo. Yafuatayo ni mapendekezo halisi yaliyototolewa na kamati:

- Kwakuwa Mamlaka ya Mapato ni mlengwa wa mfumo (ARMS) iangalie uwezekano wa kuwa katika sehemu ya mkataba wa TTMS.

- Mamlaka iingie mkataba na mtengenezaji mfumo wa ARMS ili kutoa huduma za mfumo huo.

- Mamlaka inaweza kutaka kuwa na teknolojia ya juu ambayo itaiwezesha kupata taarifa kutoka katika waendesha mawasiliano. Baadhi ya fulsa kwa Mamlaka zitakuwa ni:

  a) Mamlaka inaweza kupata taarifa moja kwa moja kutoka kwa waendesha mawasiliano kwa kutumia mfumo wa Mamlaka ya Mawasiliano ambao upo kwenye makampuni ya simu. Hii itahusisha kuweka kiungo kati ya makampuni ya simu na tovuti kuu ya Mamlaka ya Mapato.

  b) Mamlaka inaweza kutumia mfumo wa mawasilaono kutoka Mamlaka ya Mawasiliano, ambao utahusisha kupata taarifa zote kutoka makao makuu ya Mamlaka ya Mawasiliano.

- Mamlaka ya Mawasiliano kuipa Mamlaka ya Mapato taarifa zote za TTMS ili Mamlaka ya Mapato iweze kufahamu jinsi TTMS inavyofanya kazi. Hii itasaidia Mamlaka ya Mapato kuwandaa mahitaji ya mfumo wa ARMS.

- Mamlaka ya Mawasiliano kumwita mtaalamu wa TTMS kwa ufafanuzi zaidi juu ya mkataba wa utengenezaji wa mfumo wa ARMS ndani ya mfumo wa TTMS.

- Iwapo Mamlaka ya Mapato itakuwa ni sehemu ya mkataba wa TTMS, Mamlaka ya Mawasiliano na Mamlaka ya Mapato itapaswa ikubaliane na taratibu sahihi za manunuzi za mfumo wa ARMS.

Tamthmini ya mapendekezo ya kamati ilidhihirisha kwamba, kamati haikuzingatia vipengele vya utawala na usimamizi vya mradi wa ARMS kwakuwa mradi huu unahusisha taasisi mbalimbali zenye uongozi na utawala tofauti.

5.7.6 Haja ya Matumizi Bora ya Moduli za TTMS

Mamlaka ya Mawasiliano inaendesha mfumo wa kudhibiti mawasiliano ya simu (TTMS) ambao unafuatilia mwenendo wa mawasiliano ya simu za kimataifa kutoka kwa waendesha mawasiliano waliopewa leseni. Mfumo huu umezingatia moduli tano ambazo ni mfumo unayofutilia mwenendo wa mawasiliano ndani na nje ya nchi; mfumo wa usimamizi wa udanganyifu katika mawasiliano; mfumo wa usimamizi wa ubora wa mawasilaino; mfumo wa kufuatilia uhamishaji wa pesa kwa njia ya simu; pamoja na mfumo wa uchunguzi yaani Regista ya Kumtambua Mpiga Simu (CEIR) . Mapitio yangu juu ya matumizi ya moduli hizo yaligundua kwamba baadhi ya moduli zinatumiwa vizuri Zaidi. Kwa mfano, mfumo unaofuatilia mwenendo wa mawasiliano ndani na nje ya nchi ni moduli yenye thamani ndani ya Mamlaka kuliko mamlaka zingine. Hata hivyo, bado kuna uwezekano wa kuongeza matumizi ya moduli hii kwa Mamlaka ya Mapato kwa ajili ya uhakika wa mapato ya waendesha mawasiliano ndani na nje ya nchi.

Mfumo wa kubaini udanganyifu katika mawasiliano unafanya kazi kwa karibu na kwa kutegemeana na mfumo wa wa ufuatiliaj mwenendo wa mawasiliano ndani na nje ya nchi. Kwahiyo matumizi yake yapo katika kiwango kinachokubalika. Mfumo wa usimamizi wa ubora wa mawasiliano unafaa katika shughuli za msingi za Mamlaka ya Mawasiliano, hata hivyo tunaamini bado kuna nafasi zaidi ya kuuboresha mfumo huu kwakuzingatia kanuni zinazosimamia ubora wa mawasiliano yanayotolewa na watoahuduma wa mawasiliano na uwezo wa kiufundi wa Mfumo huu. Mfumo wa kufuatilia uhamishaji wa pesa utatoa uwezo wa kufanya miamala ya simu kwa muda.

Ninaamini Benki Kuu ya Tanzania itakuwa ni taasisi muhimu ya kutumia mfumo huu, kwa kuwa utatoa uwezo wa kuifundi unaoweza kudhibiti uhamishaji wa pesa kutoka benki kwa njia ya simu. Kama uchambuzi wa taarifa za kibiashara utajengwa ndani ya ufumo huu, baadhi ya

masuala muhimu kuhusu mzunguko wa pesa kwa njia ya simu yataratibiwa vema na masuala hayo ni pamoja na kiwango cha pesa, athari inayotokana na kushindwa kwa mfumo wa pesa kwa njia ya simu ambao unasimamiwa na makampuni ya simu na athari ya thamani ya kubadilisha pesa kutokana na miamala ya pesa kwa njia ya simu kutoka nje ya nchi. Masuala mengine ni kuchunguzwa kirahisi pesa chafu pamoja na miamala ya pesa haramu kupitia simu na usafirishaji wa pesa kutoka nje unaweza kuchunguzwa kirahisi.

Pia nilibaini kuwa, Mamlaka ya Mapato haitumii moduli hii kikamilifu ili kujua kiasi cha kodi kutoka katika gharama za simu zinazotozwa na makampuni ya simu. Mfumo wa uchunguzi (CEIR) unatoa uwezo wa kufanya tamthmini ya vifaa vya simu vinavyotumiwa na mtandao wa makampuni ya simu. Mfumo huu unafaa sana katika shughuli muhimu za Mamlaka ya Mawasiliano. Hata hivyo, mafanikio ya uanzishaji wa mfumo huu unahitaji ushiriki mpana wa wadau wengine wa mfumo kutoka katika sekta ya mawasiliano kama vile wateja wa simu na makampuni ya simu.

Ni maoni yaangu kuwa matumizi ya mfumo wa TTMS yanaweza kuongezwa zaidi kwa watumiaji wengine kama Benki Kuu ya Tanzania na Mamlaka ya Mapato, pamoja na kujenga uwezo wa kibiashara kupitia marekebisho ya kanuni na taratibu za Mamlaka ya Mawasiliano.

5.7.7 Ukosefu wa Mawasiliano Miongoni mwa Wadau Muhimu wa Mradi

Mapitio ya utekelezaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Mwenendo wa Mawasiliano ya Simu (TTMS) yalibaini kuwa kuna baadhi ya mapungufu ambayo ni pamoja na ukosefu wa mawasiliano mazuri miongoni mwa wadau katika sekta ya umma kama vile: Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Mapata Tanzania na Kampuni ya Simu Tanzania.

Matokeo ya udhaifu huu ni mkataba wa TTMS kutojumuishwa katika Waraka wa Zabuni baadhi ya moduli muhimu zihusuzo na uhakiki wa mapato kama vile Mfumo wa Kusimamia Mapato ya Muda wa Hewani (ARMS). Hivyo Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania na Mamlaka ya Mapato Tanzania zimepanga kuwa na makubaliano zaidi na Mshauri wa TTMS kwa ajili ya kujumuisha moduli hii kwenye Mfumo wa Kudhibiti Mawasiliano ya Simu (TTMS). Vilevile zimepanga kuongeza baadhi ya vitendea kazi ili kuuwezesha Mfumo kuhakiki mapato katika mawasiliano ya simu jambo ambalo litapelekea kuongezeka kwa gharama.

Ni maoni yangu kuwa, gharama hizi zingeshuka endapo moduli hii ingewekwa kwa pamoja na hizi moduli tano zilizopo hivi sasa.

Kwa mujibu wa kifungu B. (vii) cha masharti maalumu ya mkataba, miongoni mwa maeneo ambayo Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania ilikubaliana na Mshauri ni kuongeza moduli ili kuweza kupata maelezo ya kumbukumbu za miito ya muda halisi uliotumika kwa lengo la kukokotoa jumla ya mapato yatokanayo na muda wa hewani kwa makampuni ya simu kwa simu za ndani ya nchi na kimataifa.

Hata hivyo, nimebaini hadi sasa Mshauri bado hajapachika kiwambo ambacho kitaweza kunasa malimbikizo ya mapato ya ndani ya nchi katika kampuni za simu. Pia, kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba, moja ya lengo ilikuwa ni kusaidia na kurahisha utekelezaji wa mchakato kwa kuhakikisha utaratibu unafuatwa katika utoaji wa taarifa za mapato, utoaji wa huduma bora na kutekeleza masharti ikiwa ni sehemu ya kibali cha mwendeshaji kufuatana na makubaliano na masharti ya kibali.

Aidha nilibaini kuwa moja ya malengo ya makubaliano ilikuwa ni kuondoa na kuzuia upotevu wa mapato kwa makampuni ya mitandao na Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Hivyo nimeshindwa kubaini kwa jinsi gani Mshauri alishughulikia lengo hili kupitia mfumo uliopo.

Miongoni mwa wajibu wa Mshauri ilikuwa ni kufanya kazi zote kama inavyotakiwa na Mwenendo wa Uhakiki wa Mapato Kimataifa, Usimamizi wa Mwenendo wa Ubora wa Huduma, Kufuatilia na Kubaini ubadhilifu, Kusimamia Miamala ya Simu, Kuhakikisha Kunakuwa na usawa miongoni mwa Waendeshaji Mtandao na kubaini taarifa za mtumiaji wa kadi ya simu na kutambua taarifa ya simu husika.

Kiambatanisho na. VII cha makubaliano kulingana na mkataba kinataka kuwepo kwa mchanganuo wa gharama za uwekezaji ambapo moja ya programu ilikuwa ni kwa ajili ya tozo (Mwenendo wa mawasiliano wa ndani ya nchi na kimataifa) ambayo imekadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 2.722.

Hivyo, nimeshindwa kubaini iwapo sehemu hii ya tozo itatumika kubaini kiasi cha malimbikizo ya mapato kwa Mamlaka kutokana na miito ya ndani na miito ya kimataifa. Pia nilibaini Mamlaka imeweka mfumo mmoja tu wa kusimamia uhakiki wa mwenendo wa mapato kimataifa huku ikiiacha sehemu ya ndani ya nchi kwa ajili ya kuhakiki mapato.

Ni dhairi kuwa Mamlaka ya Usimamizi ya Mawasiliano Tanzania imeshindwa kubainisha kilichotakiwa na mradi tangu awali. Mamlaka ilijikita zaidi katika uwekezaji na ufundi wa mradi. Kwa hali hiyo, kasoro hizi zinapelekea kuwa na vihatarishi kwa wadau wa sekta ya umma na Serikali kutofikia malengo vilevile mahitaji halisi ya mradi kutozingatiwa.

5.7.8 Kutofanya Tathmini ya Vihatarishi vya Mradi

Mgawanyo sahihi wa vihatarishi kati ya sekta ya umma na binafsi ni hitaji muhimu iwapo njia ya makubaliano kati ya

sekta ya umma au binafsi ya tozo na ukodishaji itahitaji kupata thamani ya fedha katika mradi.

Katika mahojiano na Menejimenti ya Mamlaka, nilishindwa kuthibitisha kuwa Mamlaka ya Mawasiliano ilifanya tathmini ya vihatarishi vinavyoweza kuwathiri mradi ikiwa ni pamoja na kufanya mgawanyo sahihi wa vihatarishi hivyo katika mradi wa TTMS baina ya pande zote mbili. Hivyo, ukaguzi haukuweza kuthibitisha endapo Menejimenti ya Mamlaka ilifanya Tathmini ya vihatarishi katika kipindi chote cha uwepo wa mradi.

Nimeshindwa kuthibitisha iwapo Mamlaka ya Mawasiliano iliweza kuhamisha vihatarishi vya mradi baada ya kutathmini gharama za uhamishaji kwenda sekta binafsi badala ya Mamlaka kubeba vihatarishi hivyo. Baada ya kutathmini ingekuwa njia bora ya kusimamia mradi, ikizigatiwa kuwa, mmbia wa sekta binafsi atatoza malipo ya kiwango cha juu cha mapato yatakayotokana na mradi kwa kukubali kubeba vihatarishi vya mradi huo.

Kifungu Na.22 (a) cha Mkataba wa makubaliano ya jumla wa TTMS kinatoa maelezo ya malipo kwa washauri SGS/GVG. Malipo ya washauri yamefafanuliwa zaidi kwenye mkataba katika kiambatanisho X, kuwa washauri wanatakiwa kulipwa malipo ya awali ya Matumizi Katika Vitu Vinavyodumu Muda Mrefu (CAPEX) ya kiasi cha Dola za Marekani 48,000,000. Malipo ya mwisho ya Matumizi Katika Vitu Vinavyodumu Muda Mrefu ya kiasi cha Dola za Marekani 20,655,839.24; pamoja na malipo ya mwenzi yenye dhamani ya Dola za Marekani 0.04/dakika kwa dakika 0-32, 500,000 kwa mwezi na Dola za Marekani 0.02/Dakika kwa dakika inapozidi 32,500,000 kwa mwezi.

Gharama ya mradi baada ya kutoa punguzo ni Dola za Marekani 20,655,839.24. Gharama hiyo ni pamoja na matumizi ya dharura ya Dola za Marekani 300,000 ambayo pia ni sehemu ya malipo ya mwisho ya mkataba.

Hakukuwa na ushahidi madhubuti wa kuthibitisha jinsi viwango vya malipo hayo vilivyopatikana na kama tathmini ya manufaa na gharama ilifanyika kupata kiasi cha gharama ambacho kila upande ungepata. Pia hakuna ushahidi kuwa kulikuwa na matumizi ya dharura katika uendeshaji wa mradi.

Mapendekezo

i. Menejimenti ya Mamlaka inapaswa kuwandaa mpango wa utekelezaji na kuendelea na ufuatiliaji wake katika mwaka mzima wa uendeshaji wa shuguli za mamlaka ili kupata mafanikio na kufikia lengo la mkakati huo.

ii. Mamlaka ya Mawasiliano inatakiwa kuhakikisha kuwa uandaaji wa mpango wa utekelezaji unaimarika ikiwa ni pamoja na kujumuisha viashiria na malengo katika kila shughuli inayotekelezwa.

iii. Menejimenti inapaswa kubaini masuala ya muundo wa usimamizi na utawala bora katika kuimarisha mradi na kufanya tathmini ya vihatarishi vya mradi mzima ili kuongeza udhibiti wa kukusanya kodi ya mapato;

iv. Menejimenti inapaswa kuwandaa mpango wa utekelezaji utakaoziwezesha mamlaka kufanya upanuzi wa matumizi ya moduli ya TTMS kwa ngazi ya juu kwa kuwashirikisha wadau wengine kama makampuni ya simu, Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania.

v. Ni muhimu kuhakikisha kuwa mawasiliano kati ya wadau muhimu yanaimarishwa ili kuhakikisha kwamba mahitaji yote maalamu yanabainika na kufanyiwa kazi toka mwanzo wa mradi ili kuepuka kuwa na mradi usiokidhi mahitaji yao.

vi. Taasisi za umma zinapaswa kushirikiana na wadau husika ili kuhakikisha kwamba miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa ubia wa sekta ya umma na sekta binafsi inalenga katika kupata thamani ya fedha.

vii. Ni muhimu sana upembuzi yakinifu na wa kina ufanyike kabla ya uamuzi wa utekelezaji wa mradi wowote mkubwa ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa

mafanikio, faida inapatikana na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

viii. Menejimenti ya Mamlaka inapaswa mara kwa mara kutathmini na kugawanya vihatarishi vyote kwa kuzingatia uwezo wa kila upande kuvimudu na kuvidhibiti. Pia, menejimenti inapaswa kuhakikisha kuwa mgawanyo wa vihatarishi unabakia katika kiwango ambacho Mamlaka ya Mawasiliano inaweza kudhibiti.

5.7.9 Mamlaka ya Bandari Tanzania

Mamlaka ya Bandari Tanzania ilianzishwa kwa Sheria ya Bandari Na.17 ya mwaka 2004 ili kuchukuwa majukumu ya iliyokuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania (Tanzania Harbours Authority) ambayo majukumu yake yalifikia ukomo tarehe 14 Aprili, 2005. Mamlaka ya Bandari inamilikiwa na serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia mia moja na sehemu kubwa ya mtaji wake unachangiwa na mapato ya shughuli za Mamlaka, Serikali na misaada kutoka kwa wadau mbalimbali

5.7.10 Kutofikia malengo ya viashiria muhimu vya ufanisi

Mamlaka ya Bandari ilijiwekea viashiria vya ufanisi ili kuweza kusimamia na kupima ufanisi wa kazi mbalimbali za miradi yake kama ifuatavyo:

“Panamax Ships” kushughulikiwa katika Gati 13 na 14 kabla ya mwaka 2016

a. Sehemu ndogondogo zilizoongezwa kwenye DMGP ni kama ifuatavyo:
   - Kuendeleza Gati 13 – 14;
   - Kuhamisha Gati ya Kupakulia Mafuta ya Kurasini (KOJ);
   - Kuimarisha Gati 8 – 11;
   - Kujenga na kukamilisha gati ya kupokea meli za magari (RoRo) kabla ya mwaka 2014;
   - Kuongeza ujenzi wa Gati nne. Gati mbili kati ya hizo zijengwe na kukamilika katika Bandari ya Mtwara kabla ya Juni, 2016;

- Kutoa taka zilizoko chini ya maji kwenye mkondo wa kuingilia kwenye CD 13 ifikapo 2015;
- Kuboresha Gati 1 -7 ili kumudu meli kubwa. Gati 1 – 7 ziwe zimeboreshwa kufikia 2016;
- Kufupisha Gati ya Kupakulia Mafuta ya Kurasini ili kuwezesha meli kubwa kupita kupitia Gati 13 na 14 ifikapo 2014;
- Kuongeza uwezo wa mita za Gati ya Kupakulia Mafuta ya Kurasini kutoka mita za ujazo 740 kwa saa hadi kufikia mita za ujazo 1,500 kwa saa ifikapo 2013;
- Kuongeza uwezo wa kumudu mbolea, nafaka na masalia ya makaa ya mawe ifikapo mwaka 2015;
- Kuweka barabara nzuri kwenye mageti ifikapo mwaka 2013;
- Kutengeneza Gati za kuelea katika Bandari ya Dar es Salaam ifikapo mwaka 2013 na;
- Sera ya uwekezaji iwe imepitiwa upya kabla mwezi Disemba 2011

Mapitio yangu ya utekelezaji wa mpango mkuu wa Mamlaka na viashiria vyake vya ufanisi yalibaini kuwa viashiria vingi vya ufanisi havikufikiwa kama ilivyoainishwa kwenye Kiambatisho VI. Nina shaka kutofikiwa kwa malengo hayo kumeathiri uwezo wa Mamlaka kufikia malengo yaliyoainishwa kwenye mpango mkuu wa Mamlaka ya Bandari.

5.7.11 Mapungufu Katika Uendeshaji na Udhibiti wa Karakana ya Meli ya Gati ndogo ya Nchi Kavu Dar Es Salaam

Katika ripoti ya mwaka 2011, niliripoti juu ya kuchakaa kwa Gati ndogo ya nchi kavu ambayo ilijengwa tangu miaka ya 1950 na kushauri kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Bandari iweke mikakati ya kuijenga upya Gati hiyo kwa hatua ili kuongeza ufanisi.

Katika ukaguzi wa mwaka huu, nimebaini kuwa, Karakana hii haifanyi kazi kwa kuwa miundombinu yake imechakaa

na haiwezi kutengenezeka na baadhi ya vifaa vilitolewa kufuatia uendelezaji wa gati namba 13 na 14. Pia nilibaini kwamba matengenezo ya matishari (TPA marine crafts) yamekuwa yakifanyikia katika Bandari ya Mombasa ambapo kiasi cha Shilingi milioni 1,327.14 kilitumika.

Ni maoni yangu kuwa kuwepo kwa karakana ya meli ya kisasa kutawezesha ufanisi wa vifaa kwa kiwango cha juu. Uwepo wa matishari kutaongeza ufanisi wa kazi za Mamlaka pamoja na kupunguza gharama za matengenezo ya kila mwaka zinazotokana na huduma hiyo kutolewa nje ya nchi.

Kutokuwepo kwa karakana ya meli inayofanya kazi kunaikosesha Mamlaka mapato na kuongeza gharama za matengenezo kutokana na matishari ya mamlaka kukarabatiwa nje ya nchi yanapoharibika.

5.7.12 Kuwepo kwa Bajeti ya Maendeleo Isiyo Halisi.

Mpango Mkuu wa Bandari (Port Master Plan) ni wa miaka 18 na ni sehemu ya Mpango Mkakati wa Mamlaka. Muundo wa bajeti wa Mamlaka ya Bandari unaakisi Mpango Mkuu na ulizingatia Mpango Mkakati wa Mamlaka wa Miaka mitano (5) wa mwaka 2011/21 – 2015/2016 ukijumuisha bandari zote na makao makuu.

Baada ya kupitia Mpango na muundo wa bajeti na utekelezaji wa Mpango Mkakati ilibainika kuwa kila lengo lilikuwa na chanzo cha fedha kilichohitajika ili kutekeleza malengo yaliyo katika Mpango Mkakati. Nilibaini pia kuwa asilimia 85 (Dola za Marekani milioni 2,020.45 sawa na Shilingi trilioni 4.24) zilizokadiriwa zinahitajika kutoka vyanzo vya nje. Asilimia 15 tu ndicho kiasi kinachotokana na vyanzo vya ndani.

Pia, nilipitia Mpango Mkakati wa kati wa Mamlaka na kubaini kuwa makadirio ya fedha zinazohitajika kutekeleza kazi zilizoainishwa kwenye mpango ni Dola za Marekani milioni 475.4 ambapo asilimia 15 ya fedha hizo

zimeainishwa kuwa zitatokana na vyanzo vya ndani na asilimia 85 zitatokana na vyanzo vya nje kupitia mpango wa ubia wa umma na sekta binafsi.

Hali hii inaonyesha kuwa bajeti ya mwaka ya Mamlaka ya Bandari ilitengenezwa bila kuzingatia vya kutosha changamoto zitokanazo na kupata fedha kutoka vyanzo vya nje. Pia haikuzingatia kiwango cha wataalamu kinachohitajika kutekeleza malengo ya kimkakati ili kufikia malengo yaliyoainishwa kwenye mpango mkuu wa Mamlaka ya Bandari.

Ninaonelea kwamba vigezo vya mgawanyo wa bajeti si halisi hali inayoweza kusababisha mipango yenye matarajio makubwa na kuwathiri usahihi wa makadirio ya bajeti ya mtaji wa maendeleo.

Mamlaka inashauriwa, kwa kutumia Idara ya Mipango, kuwanzisha mpango mkakati wa utafutaji na ukusanyaji wa rasilimali ambao ni mahususi kwa ajili ya kupanua wigo wa wakopeshaji na kuboresha uwezo wa kutafuta na kukusanya rasilimali baina ya Mamlaka na kuweka mahusiano mazuri na wakopeshaji.

5.7.13 Kusuasua kwa utekelezaji wa miradi iliyoainishwa kwenye Mpango Mkuu wa Bandari wa 2028

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilianza kutekeleza mpango mkuu wake mwaka 2010 ikiwa ni sehemu muhimu ya programu yake ya mabadiliko makubwa ya kuboresha usimamizi na udhibiti wa kazi zake na uandaaji wa taarifa za ufanisi pamoja na kuongeza ufanisi wa kazi za Bandari.

Nilipitia hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Mamlaka hususani miradi iliyoainishwa. Ilibainika kuwa, jitihada za kutekeleza Mpango Mkuu wa Mamlaka unakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinathibitishwa na miradi minane (8) ambayo utekelezaji wake ama uko nyuma, umeahirishwa au umesimamishwa kwa miezi kadhaa. Hali hii inaathiri kufikiwa kwa malengo

yaliyokusudiwa kama yalivyoainishwa kwenye Mpango Mkuu wa Mamlaka.

Maelezo ya miradi hiyo na vikwazo vilivyoikumba vimeelezewa kama ifuatavyo:

a) Ujenzi wa Gati 13 na 14

Mpango Mkuu wa Bandari umeainisha hatua za utekelezaji wa ujenzi wa Gati mpya za 13 na 14 katika Bandari ya Dar es Salaam. Kwa mujibu wa Mpango Mkuu huo, ujenzi wa Gati hizo mpya ulitakiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miaka mitano (5) kuwanzia mwaka 2010 hadi mwaka 2016 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 524. Hata hivyo, utekelezaji wake uliahirishwa kwa kipindi cha miaka minne kutokana na sababu zifuatazo:

i. Kubatilishwa kwa uhalali wa Kampuni ya Kichina CCCC iliyozuiwa kujihusisha na shughuli za manunuzi (tendering) na Benki ya Dunia Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) mwaka 2010. Kampuni hiyo haikufuata mwongozo wa Benki ya Dunia kifungu namba 1.14(a)(ii) kwa kufanya udanganyifu kwa kudanganya au kuondoa taarifa muhimu ili kushawishi maamuzi ya kimanunuzi au utekelezaji wa mkataba.

ii. Pia, mwezi Mei 2013, kampuni nyingine ya Kichina CHEC ilichukuwa zabuni hiyo ili kuendeleza mradi huo kwa muundo wa "EPC". Lakini, makubaliano ya kisheria na CHEC hayakukamilishwa kwa sababu ilikuja kugundulika kwamba CHEC ilikuwa ni kampuni tanzu ya Kampuni ya Kichina CCCC ambayo ndio iliyofungiwa na Benki ya Dunia.

Ilibainika kuwa Mamlaka ilifanya jitihada za kutekeleza ujenzi wa Gati 13 na 14 kwa ubia na sekta binafsi chini ya muundo wa Buni, Jenga, Endesha kontena rejesha (DBOT). Hata hivyo mradi haukuanza kwa kuwa Mamlaka iliamua kusitisha taratibu za manunuzi kutokana na maswali mengi kutoka kwa waombaji kutaka kupata maelezo ya kina ya

mradi kwenya masuala ya kitaalamu juu ya kuhamishwa kwa Gati ya Kupakulia Mafuta ya Kurasini.

Ninaonelea kuwa Mamlaka haikuhusisha wataalamu wa kutosha wakati wa hatua za usanifu na pia Mamlaka haikufanya kwa kina upembuzi yakinifu kama ushahidi na uthibitisho wa mahitaji ya waombaji ambapo yangebainika mapema wakati wa upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kwa mchakato wa manunuzi.

b) Ujenzi wa Sehemu Kubwa ya kuhifadhia vimiminika (Construction of CUSTODY Transfer Tank Farm Project)

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilipanga kutekeleza kwa ukamilifu mradi huu mwaka 2015 kwa makadirio ya Dola za Marekani milioni 20 kwa lengo la kuboresha udhibiti wa mfumo wa uhifadhi wa mafuta kutoka kwa makampuni ya uagizaji wa mafuta. Hata hivyo mradi huu haukutekelezwa kutokana na kufutwa na kusimamishwa kwa mchakato wa manunuzi ili kupisha na kuwezesha kufanyika kwa upembuzi yakinifu na kutathmini kazi za kukamilishwa kwenye usanifu wa kina cha bahari, nguvu ya maji ya bahari na udongo wa sakafu ya bahari (bathymetric, hydrodynamic and geotechnical designs).

Hii inaonesha kuwa Mamlaka ilianza mchakato wa manunuzi bila kufanya upembuzi yakinifu wa kina wa mradi huo na kusababisha kusimamishwa kwa utekelezaji wa mradi huo na hivyo malengo yaliyokusudiwa kutopatikana kwa wakati.

c) Kuendeleza Sehemu ya Kuegesha Malori Nje ya Bandari

Mpango Mkuu wa Bandari wa hadi 2028 unaitaka Mamlaka kuendeleza sehemu ya maegesho ya malori nje ya bandari ili pamoja na mambo mengine, kuwezesha uhifadhi wa mizigo mingi zaidi. Kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Mamlaka kwa mwaka 2011/12–2015/16, jumla ya Dola za

Marekani milioni 55 zilikasimiwa na ilitarajiwa mradi huu uwe umekamilika kufikia mwaka 2014.

Nilibaini kuwa mradi huo haukutekelezwa kutokana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kukataa ombi la Mamlaka la utekelezaji wa mradi huo katika eneo la Manispaa kwa kuwa hapakuwepo na makubaliano yoyote kati ya Mamlaka na Manispaa hiyo.

Ninaonelea kuwa Mamlaka ya Bandari ilianza mchakato wa manunuzi bila kufanya mazungumzo wala kuweka makubaliano na Manispaa ya Temeke juu ya uwekazaji huo. Hii inaashiria kuwa kuna uwezekano wa Mamlaka kushindwa kutekeleza mradi huo na hivyo kuwathiri mipango na malengo ya kimkakati ya Mamlaka.

d) Mradi wa ujenzi wa Gati moja kwa ajili ya samaki nje ya bandari ya Dar es Salaam

Mpango Mkakati wa Mamlaka umeonesha hatua za utekelezaji wa ujenzi wa Gati ya Samaki moja ambayo ilitarajiwa kukamilika mwaka 2015 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 21. Mradi huo unahusisha kuhamishwa kwa soko la samaki la sasa kwa ajili ya usalama wa Bandari.

Hata hivyo, hadi wakati ukaguzi unafanyika mwezi Februari, 2016 mradi ulikuwa haujaanza kutokana na mazungumzo yaliyokuwa yakiendelea na wadau wengine mbalimbali ambao hawakuhusishwa kabla ya mchakato wa manunuzi.

Ninaonelea kuwa utekelezaji wa mradi usingechelewa kama mazungumzo na wadau wote yangefanyika kwa umakini na kwa ukamilifu kabla ya hatua za mwanzo za utekelezaji wa mradi hali ambayo ingewezesha urahisi wa utekelezaji wa mradi.

e) Kuboresha mradi wa "Lighter Quay"

Mamlaka ilipanga mradi huu uwe umekamilika ifikapo mwaka 2015. Hata hivyo utekelezaji wa mradi uliahirishwa

kutokana na ukamilishwaji wa mradi wa Programu ya Maboresho ya Bandari (DMGP). Ninaonelea kuwa kutohusishwa kwa wataalamu katika hatua za awali za upangaji na usanifu wa mradi kumesababisha kushindwa kutekeleza mradi huo na hivyo kusababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kutohusishwa kwa wataalamu katika hatua za awali za usanifu wa mradi ndiko kulikosababisha kutozingatiwa kwa kazi za miradi mingine ambazo zilizokwishaanza na ambazo zilikuwa zinaathiri utekelezaji wa mradi huu. Pia, Mamlaka haikufanya tathmini ya kina juu ya vihatarishi vinavyoweza kukwamisha utekelezaji wakati wa usanifu wa mradi huu. Tathmini hii ni muhimu na ingetoa njia za kukabiliana na vikwazo vinavyojitokeza.

Mpango Mkakati wa Mamlaka unaonesha shauku kubwa ya Mamlaka ya kutekeleza miradi inayohitaji utaalamu wa hali ya juu na rasilimali nyingi kuliko uwezo wa Mamlaka. Wakati huo huo hakuna uratibu mzuri wa mawasiliano kati ya Mamlaka ya Udhibiti wa Bandari na wadau wengine katika kutekeleza miradi ya Mamlaka.

Kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi ya uendelezaji wa mitaji kwa Mamlaka kunaathiri kufikiwa kwa malengo ya Mamlaka kwa wakati na inaathiri ufanisi wa utekelezaji wa kazi za Mamlaka kwa ujumla. Uratibu na mawasiliano hafifu kati ya Mamlaka ya Bandari na wadau wengine wa utekelezaji, unaathiri utekelezaji wa miradi ya Mamlaka kama inavyothibitishwa na mradi wa Soko la Samaki na Mradi wa Maegesho ya Malori Temeke. Pia, kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi kunaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama za miradi hiyo na kushusha imani ya wafadhili kwa Mamlaka.

5.7.14 Mapungufu Kwenye Mkataba Baina ya TICTS na Mamlaka ya Bandari

Mnamo tarehe 5 Mei 2000, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Tume ya Kurekebisha Mashirika ya

Umma (PSRC), Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa upande mmoja na Kampuni ya Huduma za Makontena ya Kimataifa (ICTASI) na Kampuni ya Kimataifa ya Huduma za Makontena Tanzania (TICTS)" kwa upande mwingine iliingia mkataba wa miaka kumi(10) ya uendeshaji na usimamizi wa kitengo cha makontena na ghala la makontena liliyopo Kurasini Dar es Salaam.

Mkataba huo wa upangishaji ulihusisha pia usimamizi wa gati namba 9-11. Eneo hilo lilikabidhiwa kwa TICTS pamoja na vifaa vyake na Mamlaka ya Bandari mnamo tarehe 10 Septemba 2000, ambapo ndio tarehe rasmi ya kuanza utekelezaji wa mkataba wa upangishaji. Kwenye mkataba huo, TICTS ilitakiwa kuilipa Mamlaka ya Bandari kiasi cha Dola za Marekani 3,680,000 ambazo zingelipwa kwa siku ya kwanza ya miezi kumi na mbili itakayofuata.

Mapitio ya Mkataba huo yaligundua mapungufu yafuatayo:

a) Kutokuwepo kwa Uangalizi wa Makontena Yanashughulikiwa na TICTS

TICT iliingia mkataba na Mamlaka ya Bandari Tanzania ambao unawapa mamlaka TICTS ya kutoa huduma za kupokea makontena kwa niaba ya Mamlaka ya Bandari. Kutokana na mkataba huo, TICTS ingelipa mrabaha na tozo ya matumizi ya bandari kwa kila kontena litakalopokelewa TICTS.

Niligundua kwamba Mamlaka ya Bandari haikuwa na chombo chochote kilichowawezesha kusimamia na kufahamu idadi ya makontena ambayo yalipokelewa na kuhifadhiwa na TICTS. Mamlaka ya Bandari inategemea taarifa kutoka TICTS. Pia haifanyi usawazishaji (reconciliation) wa taarifa halisi za makontena yanayotunzwa na kusimamiwa na TICTS mara baada ya kupata taarifa hizo.

Baada ya timu ya ukaguzi kuihoji menejimenti ya TPA kuhusu ulinganishaji wa taarifa za makontena

yanayopokelewa na TICTS, Menejimenti ilisema kwamba Mamlaka haina haki ya jumla ya kuingia kwenye mfumo wa kompyuta wa TANCIS ambao ndio mtandao wa usimamizi wa makontena wa Mamlaka. Pamoja na hayo, kutokana na Mamlaka kuomba ruhusa ya kuingia kwenye mtandao huo mara kwa mara kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya kuongezewa wigo kwenye TANCIS, Mamlaka ya Bandari Tanzania haijapewa haki ya kuingia kwenye mtandao huo wa TANCIS hadi ninaandika taarifa hii.

Hii imekuwa ngumu kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania kuweza kusimamia ipasavyo mapato yatokanayo na kitengo cha makontena cha TICTS ambayo huwa yanakusanywa na kitengo hicho kila siku na kulipwa kwa Mamlaka ya Bandari kila mwezi.

Mamlaka ya Bandari Tanzania ilipeleka tena maombi Mamlaka ya Mapato kwa ajili ya kupewa uwezo wa kuingia kwenye mtandao wao wa TANCIS mnamo mwezi Disemba 2015. Mamlaka ya Bandari imeendelea kutumia taarifa za mapato kutoka TICTS.

Kutokana na kutegemea taarifa kutoka TICTS tu, kuna uwezekano wa Mamlaka ya Bandari kupoteza kiasi kikubwa cha mapato.

b) Kubadilika kwa Umiliki pamoja na kubadilka kwa kipindi cha upangishwaji

Mnamo tarehe 31 Oktoba, 2001, ikiwa ni siku ya 20 baada ya kusainiwa mkataba wa upangishaji wa kitengo cha makontena, niligundua kwamba hati ya mabadiliko (Addendum) Namba 1 ilitiwa saini kubadili umiliki wa mkataba wa upangishaji kutoka ICTSI ili kuhamishia asilimia 51 ya hisa za TICTS kwa kampuni ya Hutchison International Port Holding.

Vilevile niligundua kwamba, mnamo tarehe 30 Disemba 2005 miaka mitano kabla ya kukamilika kwa mkataba wa upangishaji, Mabadiliko Namba 2 yalitiwa saini. Mabadiliko

namba 2 ya mkataba wa upangishaji ulianza kutumika ambapo kipindi cha upangishaji kiliongezwa kutoka miaka 10 ya mwanzo na kuwa miaka 25. TICTS ilipewa ongezeko la eneo ambapo ilikuwa inachukuwa gati namba 8 na maeneo yote yanayolizunguka na eneo la kuhifadhia makontena la Ubungo ambalo hapo mwanzoni halikuwepo kwenye mkataba wa upangishaji.

Kutokana na kifungu cha 9.1 cha mkataba wa upangishaji mabadiliko ya muda wa mkataba wa upangishaji hayaruhusiwi.

Moja ya madhumuni ya ubinafsishaji wa mashirika ya umma ilikuwa ni kwa Serikali kuingia ubia na makampuni binafsi kwa makampuni na mashirika yote ya umma ambayo yalikuwa yakijiendesha kwa hasara ili kuyaongezea ufanisi. Kinyume cha madhumuni hayo, mkataba wa upangishaji wa gati namba 8-11 ulijumuisha hifadhi za makontena za Kurasini na Ubungo ambazo zilikuwa zikifanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

Pia, niligundua kwamba Mamlaka ya Bandari iliishauri Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kumhusisha mshauri muelekezi ili kuweza kutoa mapendekezo kwenye mfumo mzima wa ubinafsishaji na muundo wa mkataba mpya wa upangishwaji. Mshauri mwelekezi alitoa mapendekezo kuwa kwenye eneo hilo jipya la gati namba 8-11 liwe la makontena 500,000 ya urefu wa futi ishirini. Kutokana na ushauri wa Mshauri Mwelekezi, eneo hilo lilionekana lenye faida Zaidi. Hivyo Serikali inatakiwa kulipa Dola za Marekani milioni 50-100 kama gharama za upanuzi.

Hata hivyo, kiasi hicho cha fedha hakikulipwa na Serikali kwa ajili ya upanuzi huo.

Nimethibisha kwamba ubinafsishaji wa eneo hili la uzalishaji haukuzingatia madhumuni ya ubinafsishaji kama ilivyokuwa kwenye Sera ya Ubinafshishaji ya Sekta ya Mashirika ya Umma.

c) **Kushuka kwa kiwango cha ufanyaji kazi cha mpangaji chini ya makubaliano.**

Kifungu cha 7.4.2(2) cha mkataba wa upangishaji kinaeleza kwamba Mkataba wa upangishaji unaweza kutenguliwa endapo kiwango cha ufanyaji kazi kwa mwaka kitashuka kwa zaidi ya asilimia 25.

Niligundua pia kwamba kwa mwaka 2007, Mamlaka ya Bandari ilifanya tathmini ya ufanisi wa TICTS tangu mwaka 2000 na ikagundua kuwa kiwango cha ufanyaji kazi kilishuka sana, Mamlaka iliwasilisha ripoti hiyo TICTS. TICTS ilikiri kwamba ufanyaji wao wa kazi ulikuwa chini ya kiwango ambacho walikubaliana kwenye mkataba wa upangishwaji.

Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Bandari iliwasilisha mapendekezo Wizara ya Miundombinu mwezi Septemba 2007 ikipendekeza mapitio ya mkataba wa upangishaji ikiwepo, kuondolewa kwa kipengele cha upekee, kuongeza kiwango cha ufanyaji kazi, kuongeza kiwango cha malipo ya mrabaha, kuitaka TICTS kuwasilisha mpango wa uwekezaji ambao utajumuisha manunuzi ya vifaa vipya vya kufanyia kazi, na pia kuongezea kipengele cha mapitio ya mkataba ya upangishaji kila baada ya miaka mitano (5).

Mnamo mwaka 2008, TICTS ilipewa notisi ya nia ya kuvunja mkataba wa upangishaji kutokana na kuvunja kipengele cha 7.4.2(2) kilichotokana na ufanyaji kazi usioridhisha ambapo ilipelekea lengo kushuka kwa asilimia 26. Kutokana na kifungu 7.4.2(2), mkataba wa upangishaji unaweza kuvunjwa kama ufanisi utashuka kwa kiwango cha asilimia 25 kwa mwaka.

Hata hivyo, Serikali ilitoa maelekezo kwa Mamlaka ya Bandari isiitoe hiyo notisi kwanza kwa TICTS ili kupisha majadiliano kati ya pande hizo mbili. Majadiliano yalifanyika ambayo yalipelekea kupitiwa kwa mkataba mwaka 2009, ambapo masuala ya kujadiliana yalitimia

baada ya kusaini randama ya makubaliano (MoU) tarehe 5 Octoba 2009 kama mpango kazi wa kuongeza ufanisi.

d) Kushindwa kupanua umiliki wa TICTS kwa kuuza hisa kwa Wananchi

Kifungu cha 6.1.6 cha mabadiliko namba 2 ya mkataba kinamtaka mpangaji kupanua umiliki wa TICTS kwa kuuza hisa kwa wanachi. Kutokana na mkataba wa upangishaji, mpangishaji alitakiwa kuongeza umiliki wa kampuni ya TICTS ifikapo tarehe 31 Disemba 2011 ili Watanzania waweze kumiliki hadi asilimia 40 ya hisa za kampuni hiyo. Ili kuondoa mkanganyiko kwa kuongezeka umiliki wa hisa kwa Watanzania kwa asilimia 40, majukumu ya mkataba wa upangishaji yalipaswa yawe yamefikiwa kwa ujumla.

Hata hivyo hadi ninakamilisha ripoti hii, mwezi February 2016, sikuweza kupata uthibitisho iwapo hisa za TICTS zimeuzwa kwenye soko la hisa kwa Watanzania kama ilivyotakiwa na mkataba wa upangishaji.

5.7.15 Matengenezo ya Eneo la Kuhifadhia Mizigo la Kisarawe

Eneo la kuhifadhia mizigo la Kisarawe ni eneo la bandari kavu ya Kisarawe Kaskazini (km 35 kutoka Dar es Salaam). Eneo hili litakuwa ni upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam ili kukidhi hifadhi ya makontena na magari yanayotoka na kwenda nje ya jiji na nchi jirani.

Mradi huu wa Kisarawe unahusisha ujenzi wa njia ya reli; ujenzi wa; kuunganisha yadi ya makontena ya Bandari ya Dar es Salaam, kiwanja kipya cha kuhifadhia mizigo, barabara mpya za maunganisho; kituo cha kuhifadhia mizigo; jengo la mawakala wa kutoa mizigo bandarini na sehemu ya kuhifadhia magari. Gharama za mradi huu zilikadiriwa kuwa kiasi cha Dola za Marekani milioni 280. Katika kipindi cha ukaguzi, niligundua kwamba, pamoja na mradi kuwa kwenye hatua ya pili ya utekelezaji, ulisimamishwa na Serikali.

Wizara ya Uchukuzi ilitoa maelekzo kwa Mamlaka ya Bandari kuusimamisha mradi huo kwa sababu kampuni binafsi ijulikanayo kama BlackIvy kutoka Marekani ilikuwa tayari kutekeleza mradi kama huo maeneo ya Soga Bagamoyo mkoani Pwani kwa gharama zake yenyewe. Hatukuweza kupatiwa uthibisho kuwa ni kwa vipi kampuni hii iliweza kupatikana na endapo ilipatikana kwa kushindanishwa.

Mradi huu upo kwenye mpango wa uendelezaji wa Bandari na ulikuwa ukipewa fedha kutoka Benki ya Dunia. Kwa kuongezea, fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa awali ilikuwa imeshalipwa na Benki ya Dunia. Upembuzi yakinifu ulishafanyika na eneo la mradi lilikwishafahamika. Kuusimamisha mradi huu na kuipa sekta binafsi mradi ambao Benki ya Dunia kupitia Mamlaka ya Bandari ilishawekeza fedha haikuwa maamuzi ya kimsingi na iliweza kuwathiri utekelezaji wa mpango wa uendelezaji wa Bandari.

Fedha za mradi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu zilikuwa zimeshalipwa kwa mshauri mwelekezi ambapo baada ya kuusimamisha haijaweza kuzaa matunda kwa Mamlaka ya Bandari.

Mapendekezo kwa Menejementi ya Bandari:-

i. Kuwanzisha chombo cha kusimamia miradi ili kuhakikisha na upembuzi yakinifu unafanyika kikamilifu kabla ya utekelezaji wa miradi.
ii. Kuhakikisha kwamba kunakuwa na muunganisho na ushirikishaji wa wadau wote wa Bandari kama vile Wizara ya Fedha, Msajili wa Hazina, Wizara ya Uchukuzi na vyombo vingine vya utekelezaji kwenye kipindi cha mipango ya miradi, na pia katika kipindi cha utekelezaji wa miradi husika.
iii. Menejimenti inashauriwa kufuata malengo ya Mamalaka kwa kuwezesha kufuata Mpango Mkuu wa

Bandari au kufanyia marekebisho Malengo ya mamlaka ili yaweze kutekelezeka.

iv. Kuhakikisha ujenzi wa gati 13 & 14 unakamilika mapema iwezekanavyo kwani kwa kutokamilika kunaathiri utekelezaji wa malengo ambayo Mamlaka imejiwekea Malengo mengi yanategemea kukamilika kwa gati namba 13 & 14.

v. Mamlaka ya Bandari kuupa kipaumbele ukarabati wa bandari ya Dar es Salaam ili kuiweka kwenye ushindani kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

vi. Mamlaka ya Bandari ikusanye maelezo kutoka kwenye mfumo wa kompyuta wa TANCIS ambayo yataionyesha makontena yaliyopokelewa na TICTS na kuyalinganisha na idadi halisi yaliyopokelewa na TICTS.

vii. Serikali ipitie upya mkataba wa upangishaji wa TICTS ili kuona ni jinsi gani matakwa ya jamii yametekelezwa kwa kupitia mkataba huu. Pia matakwa ya kisheria ya kuongezea muda mkataba huu kabla ya kuisha kwa muda kwa mkataba wa kwanza. Kutathmini na kuona kama kulikuwa na manufaa na pia kuwangalia kama kuna uwezekano wa kuuvunja mkataba huu.

viii. Menejiment ya Mamlaka ya Bandari ifuatilie kwa karibu masuala ya TICTS na kuhakikisha inafuata vigezo na masharti ya mkataba wa upangishaji.

ix. Pia, Serikali ipitie upya maamuzi ya kuusimamisha mradi wa kujenga sehemu ya kuhifadhi mizigo ya Kisarawe ili kuhakikisha Mamlaka ya Bandari inatekeleza majukumu yake kwa upana ili kuongeza ufanisi.

SURA YA SITA

UFUATILIAJI NA UTATHIMINISHAJI WA UBINAFSISHAJI

6.0 UTANGULIZI

Serikali ilisitisha shughuli za Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC) tarehe 30 Juni 2014 na kuhamisha shughuli zilizobaki kwa Msajili wa Hazina kuwanzia tarehe 1 Julai, 2014. Katibu Mkuu Wizara ya Fedha alimuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalumu wa Shirika Hodhi la Mali za Serikali ili kuthibitisha hali ya kifedha ya Shirika ikiwa ni pamoja na mali, madeni, na shughuli zote zilizobaki ili kubaini mapungufu na athari zake katika shughuli za Shirika. Ukaguzi ulilenga katika kumwezesha Msajili wa Hazina kufuatilia na kuchukuwa hatua zinazohitajika kuhusu masuala ya uendeshaji na ukamilishaji wa shughuli zilizobaki toka Shirika Hodhi la Mali za Serikali.

6.1 Matokeo Muhimu na Mapendekezo

6.1.1 Ufuatiliaji wa Maendeleo ya ubinafsishaji wa Mashirika

Ufuatiliaji na tathmini ya mali za mashirika yaliyobinafsishwa ni muhimu katika kupima matokeo tarajiwa ya ubinafsishaji na kuhakikisha vifungu muhimu vya mkataba wa mauzo vinafuatwa.

Utekelezaji wa mpango wa uwekezaji katika kalenda maalumu ni moja ya vifungu muhimu katika mkataba wa mauzo. Mwekezaji asipozingatia mpango wa uwekezaji, husababisha uvunjaji wa mkataba ambayo inaweza kusababisha muuzaji kusitisha mkataba.

Kufikia tarehe 30 Juni, 2014,makampuni 331 kati ya 360 yalikuwa yamebinafsishwa na makampuni 29 yalikuwa katika hatua mbalimbali za ubinafsishaji. Japokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali lilikuwa na Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini yenye jukumu la kufuatilia uendeshaji na utendaji wa mashirika yaliyobinafsishwa, mashirika 180 tu kati ya 331 (sawa na asilimia 54) yalifanyiwa tathmini ya utendaji hadi kufikia tarehe ya ukaguzi huu.

Kulingana na Menejimenti ya lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali, kushindwa kufuatilia utendaji na maendeleo ya mashirika yaliyobinafsishwa kulitokana na kutokuwa na rasilimali-watu ya kutosha.

Tulibaini utekelezaji mbovu wa mpango wa uwekezaji ambapo wawekezaji walitakiwa kuwekeza katika mali kama ilivyo kwenye makubaliano ya mauzo.

Napendekeza Serikali ihakikishe rasilimali za kutosha zinakuwepo kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini mashirika yaliyobinafishwa. Vinginevyo, serikali inapaswa kufikiria kutumia kampuni binafsi katika kufanya shughuli hii.

6.1.2 Kutokamilika kwa Uhamisho wa Viwanja vya Mamlaka ya Tumbaku Viliyobinafsishwa

Mamlaka ya Tumbaku ilikuwa na viwanja vitatu katika vitalu namba 346, 347 na 348 vilivyoko Kurasini kabla ya ubinafsishaji kwa kampuni ya Tanzania Leaf Tobacco Company (TLTC) ambayo ilikuwa si sehemu ya makubaliano ya mauzo na mnunuzi ambaye ni TLTC. TLTC aliendelea kumiliki viwanja viwili namba 346 na 347 huku kitalu namba 348 kikivamiwa na watu kinyume cha sheria.

Tume ya kurekebisha mashirika ya Umma/Shirika Hodhi la Mali za Serikali liliingia katika mgogoro wa kisheria na Msajili wa Hati za viwanja katika harakati za kumiliki tena viwanja hivi vitatu na kesi zingine tano za viwanja zenye namba 241/2004 PSRC. Mahakama kuu ilitoa uamuzi wa kesi mnamo tarehe 8 Novemba, 2007 kwamba viwanja viwili vyenye namba 346 na 347 havina mzozo wowote na hivyo kutolewa na kuhamishiwa pamoja na hati kwa Mamlaka ya Tumbaku. Hata hivyo hali ya mzozo kuhusiana na kiwanja katika kitalu namba 348 haikuweza kuwekewa misingi na hali ya uhamishaji wa vitalu namba 346 na 347 bado haijafahamika. Ninashauri Serikali kupitia Msajili wa Hazina kufuatilia na kuchukuwa hatua zinazohitajika kuhusu vitalu hivyo.

6.1.3 Kukosekana kwa hati Miliki na Kutokuwepo kwa Kumbukumbu kwa Mali Zinazotarajiwa Kuuzwa

Iliyokuwa Simu 2000 ilikabidhi hatimiliki 32 kwa lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali. Kati ya hizo, ni hati 25 tu ndizo zilizopitiwa na kuthibitishwa. Hati 7 hazikuonekana na zilidaiwa kukabidhiwa kwa wamiliki husika. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi wa kukabidhiwa kwa wamiliki husika. Nashauri Msajili wa Hazina kufuatilia hati 7 zilizokosekana ambazo inasemekana zilirudishwa kwa wamiliki ili kujiridhisha kwamba hazijatumiwa tofauti na malengo yake. Kuhusu vitalu 25 ambavyo vimehifadhiwa, kuna haja ya kujiridhisha iwapo ni vile vilivyouzwa lakini bado hati hazijachukuliwa na wamiliki.

6.1.4 Kuhakiki Dhamana na Hatimiliki

Uhakiki wa iliyokuwa benki ya Taifa ya Biashara, na madeni pamoja na mali na dhamana/hatimiliki umebaini masuala mbalimbali kwa ajili ya Msajili wa Hazina kufuatilia. Masuala hayo ni kama yanavyooneshwa hapa chini.

- Baadhi ya wateja hawana habari kuhusu madeni wanayodaiwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali. Baadhi yao wapo tayari kulipa madeni hayo.
- Baadhi ya wadaiwa ambao dhamana zao zimethibitishwa si rahisi kuwapata na hakuna taarifa yoyote kuhusu mahala walipo.
- Baadhi ya wadaiwa wanalalamika kuwa wameshalipa madeni yao kikamilifu lakini hati zao bado zimeshikiliwa na Shirika Hodhi la Mali za Serikali.
- Kuna baadhi ya wadaiwa wameweka ardhi kama dhamana ambazo zina hatimiliki za jadi.
- Kuna baadhi ya wadaiwa ambao hawajawahi kutembelewa na wafanyakazi wa Shirika Hodhi la Mali za Serikali au wakusanya madeni wa Shirika Hodhi la Mali za Serikali tangu kubadilishwa kwa iliyokuwa benki ya Taifa ya Biashara.
- Baadhi ya wateja wanalalamika kuwa wamelipa madeni yao yote ama kwa wafanyakazi wa Shirika

Hodhi la Mali za Serikali au kwa wakusanya madeni wake.

- Kuna wateja ambao walidai kwamba wamenunua mali hizo na wanazimiliki kihalali.

Nashauri Msajili wa Hazina kufuatilia masuala ya dhamana na hatimiliki na kusuluhisha masuala ambayo hayajakamilika ikiwemo madeni na pia kuthibitisha na kurekebisha taarifa za wadaiwa.

6.1.5 Wadaiwa katika Mashirika ya Umma ambayo Yamebinafsishwa

Wadaiwa wa kiasi cha shilingi milioni 328 chini ya Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa hawakuingizwa katika vitabu vya lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali. Wadaiwa hawa walikabidhiwa kwa Mfuko wa Pensheni kwa wafanyakazi wa Serikali za mitaa kwa hatua zaidi baada ya mfilisi kushindwa kukusanya madeni kutokana na ugumu wa upatikanaji wa wadaiwa hao. Inawezekana wadaiwa walifutwa kiudanganyifu na wafanyakazi wasio waaminifu.
Hakuna ushahidi juu ya hadhi ya wadaiwa waliowasilishwa kwa Mfuko wa Pensheni kwa wafanyakazi wa Serikali za mitaa kwa hatua zaidi ambao kwa upande mwingine walipaswa kukabidhiwa kwa lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali. Ufuatiliaji wa wadaiwa unapaswa kuimarishwa. Taarifa sahihi za wadaiwa pamoja na ukusanyaji wa madeni vinatakiwa kuwanzishwa.

6.1.6 Mapato ambayo Hayajarekodiwa Yaliyotokana na Mashirika Yaliyobinafsishwa

Tulibaini kuwa taarifa za kifedha za mashirika mawili ya umma yanayotakiwa kufilisiwa ambayo ni BASOTU Plantation na Kampuni ya Taifa ya Ufugaji wa Kuku hazikuingizwa kwenye taarifa za kihesabu za ufilisi za lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali mnamo tarehe 30 Juni, 2014. Ufilisi wa BASOTU umehitimishwa lakini ufilisi wa Kampuni ya Taifa ya Ufugaji wa Kuku haujahitimishwa

kutokana na kutokuwepo kwa ushirikiano wa mfilisi. Ilikuwa vigumu kujua hali ya kifedha ya BASOTU na Kampuni ya Taifa ya Ufugaji wa Kuku kutokana na kutowasilishwa kwa taarifa zake kwa mashirika hayo. Ninashauri Serikali kupitia Msajili wa Hazina kuhakikisha kwamba mizania ya mali na madeni ya BASOTU na Kampuni ya Taifa ya Ufugaji wa Kuku inatengenezwa ili kuingizwa katika taarifa za fedha za lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali. Ofisi ya Msajili wa Hazina inatakiwa kuhimiza utaratibu wa kisheria ili kuwataka wafilisi wa Kampuni ya Taifa ya Ufugaji wa Kuku na BASOTU kufuata sheria za ufilisi.

6.1.7 Kutopatana Hesabu za lililokuwa Shirika Hodhi la Mali ya Serikali na Taarifa za Kihesabu za wafilisi

Tumebaini kuwa taarifa za mapato yatokanayo na uuzaji wa mali za mashirika yaliyobinafsishwa katika vitabu vya lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali vilivyokaguliwa haziendani na kiwango cha mauzo kilichopo katika taarifa za ufilisi wa shirika. Taarifa za ufilisi katika Idara Ufilisi ya Shirika Hodhi la Mali za Serikali na Idara ya fedha hazipo katika mtiririko unaoendana. Kutofanyika kwa usawazishaji wa taarifa ya ufilisi kati ya Kitengo cha fedha na Idara ya Ufilisi kinaweza kupelekea makosa katika taarifa muhimu katika vitabu vya hesabu vilivyokaguliwa.

Ninashauri Msajili wa Hazina afanye usahihishaji wa taarifa za kifedha kati ya Shirika la Umma linalotarajiwa kufisiliwa na taarifa za mali zake ili kuepuka uwezekano wa kutowekwa au upotoshaji wa taarifa za fedha.

6.1.8 Serikali kuingilia utendaji wa Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma/ Shirika Hodhi ya Mali za Serikali kwa Mashirika Yanayobinafsishwa

Serikali kupitia wizara husika iliongoza machakato wa ubinafsishaji wa mgodi wa makaa ya mawe wa Kiwira na Hoteli ya Kilimanjaro kinyume cha sheria ya iliyokuwa Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma/lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali. Hatua hiyo inakinzana na jukumu la Serikali la uangalizi kupitia sheria ya iliyokuwa Tume ya

kurekebisha mashirika ya umma/lililokuwa Shirika Hodhi la Mali ya Serikali.

Zaidi ya hayo, jukumu la usimamiaji wa iliyokuwa Tume ya kurekebisha mashirika ya umma/lililokuwa Shirika Hodhi la Mali ya Serikali juu ya Bodi na Menejimenti za makampuni maalum halijawekwa vizuri katika sheria ya Mashirika ya Umma (na marekebisho yake) ya mwaka 1993, na kuwacha lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali katika nafasi dhaifu ya kuweka usimamizi wa maamuzi ya menejimenti ambayo yangeathiri shughuli za ubinafsishaji. Ninashauri Serikali ipitie upya sheria ya Mashirika ya Umma (na marekebisho yake) ya mwaka 1993, ili kuhakikisha kunakuwa na usimamizi maalumu na wenye tija wa mashirika ya Umma. Kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu ya Msajili wa Hazina ikiwa ni pamoja na mwendelezo na ukamilishaji wa shughuli zilizobakia za Shirika Hodhi la Mali za Serikali, Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa Msajili wa Hazina anatumia mamlaka yake kwa uhuru kwa mujibu wa madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 10 (2) cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu) ya mwaka 2002 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2010).

6.1.9 Ukosefu wa udhibiti sahihi wa mapato ya kodi na nyaraka nyingine za mpangaji

Tulibaini nyumba 3 ambazo hazijauzwa za lililokuwa Shirika la Biashara la Mkoa wa Mwanza zilibinafsishwa kwa MZARTC na kwa sasa zimekodishwa kwa wapangaji mbalimbali bila ya mkataba wa kupangisha kati ya lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali na MZARTC. Pia, sehemu ya pato la kodi hutumiwa kwa ajili ya kulipa kodi ya Serikali na gharama za utengenezaji wa nyumba. Bila kuwepo kwa mkataba wa upangishaji, lililokuwa Shirika Hodhi la Mali ya Serikali ipo kwenye hatari ya kupoteza mapato ya kodi au kuwepo kwa matumizi mabaya ya nyumba. Pia, tulibaini ankara za umeme ambazo hazijalipwa zenye thamani ya shilingi milioni 19 za sehemu ya jengo la Samora ambazo EDC Polytechnical ilikuwa inadaiwa kutoka mwezi Aprili 2011

hadi Juni 2014. Kuna haja ya kuingia mkataba wa kukodisha kati ya Serikali na kampuni ya MZARTC wa majengo 3 ya lililokuwa Shirika la Biashara la Mkoa wa Mwanza ambayo hayajauzwa ili kuhakikisha kwamba mapato ya kukodisha yanatokana na Kampuni ya nyumba hizo yanahesabiwa vizuri. Kuna haja ya kuishinikiza zaidi EDC Polytechnic ili kuhakikisha malipo kamili ya umeme yanalipwa.

6.1.10 Mkakati wa ubinafsishaji na uchaguzi wa njia ya mauzo

Tumegundua kutowepo kwa mkakati wa ubinafsishaji na uchaguzi wa njia ya mauzo kwa Mashirika ya Umma yaliyo katika mpango wa ubinafsishwaji. Vigezo vinavyotumiwa na muuzaji katika kuwamua njia ya ubinafsishaji, ikiwa ni pamoja na kufikia malengo mapana ya mkakati wa ubinafsishaji haviko bayana. Hii inaweza kushababisha maamuzi ambayo si sahihi na makini kwenye malengo ya sera muhimu ya Mageuzi ya Sekta ya Mashirika ya Umma. Serikali inatakiwa ihakikishe kuwa kuna kumbukumbu kamili za mikakati ya ubinafsishaji kwa kila Shirika. Mikakati hiyo lazima ioneshe uchambuzi wa faida na gharama ya uchaguzi wa ubinafsishaji na uchaguzi wa njia sahihi za ubinafsishaji zinazoshughulikia sera muhimu za ubinafsishaji na jinsi zitakavyo fuatiliwa na kutathiminiwa.

6.1.11 Umiliki na Usimamizi wa Mashirika Yaliyobinafsishwa

Iliyokuwa Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma/lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali lilikuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba Watanzania wenye uwezo wa usimamizi na ujasiriamali wanafanikiwa katika kushiriki kumiliki Mashirika yaliyobinafsishwa kwa kushawishi uchaguzi wa mashirika ya kubinafsisha, aina ya ubinafsishaji na muda wa kubinafsisha.
Tathmini ya muundo wa umiliki wa mashirika yaliyobinafsishwa ulibaini kwamba baadhi ya mashirika yaliyobinafsishwa yanamilikiwa kwa asilimia 100 na wageni kinyume na mkakati wa ubinafsishaji wa mashirika ya umma.

Serikali inapaswa kuhakikisha kwamba sera ya Mashirika ya Umma inatoa kipaumbele kwa wazawa na kudhibiti ubinafsishaji kwa wageni bila idhini maalumu.

6.1.12 Ukusanyaji na Kuweka Benki Mapato ya Mauzo ya Ubinafsishaji

Tulibaini kwamba lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali haikufungua na kuendesha akaunti maalumu ya makusanyo ya mauzo kinyume cha kifungu cha 34 (2) cha Sheria ya Mashirika ya Umma Namba 16 ya Mwaka 1993 (kama ilivyorekebishwa). Badala yake, mapato yaliyotokana na mauzo ya Mashirika ya Umma yalikuwa yanaingizwa katika akaunti ya jumla. Ninashauri kwamba kwa mauzo yajayo, mapato yote yapelekwe kwenye akaunti maalumu kulingana na Sheria ya Mashirika ya Umma na kisha zipelekwe Hazina kama Sheria Namba 16 ya Mwaka 1993 ya Mashirika ya Umma inavyotaka.

6.1.13 Mauzo ya Shamba kwa bei Pungufu

Ofa ya mauzo ya shamba la Gombe ilitakiwa kuwa na idhini ya Serikali lakini hakuna ushahidi wa idhini ya Serikali uliopatikana. Menejimenti ya lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Serikali haikuwasilisha suala hilo katika Bodi ya Wakurugenzi pindi walipolifahamu tarehe 19 Mei, 2010. Bei ya punguzo iliyotolewa ya shilingi milioni 83.7 milioni mwaka 2013 ilizingatia bei ya mnunuaji ya mwaka 2007 ya Dola za Marekani 30,000 ambayo ilikwishapitwa na wakati ambayo ndiyo iliyoweka thamani ya shamba kuwa ni milioni 152. Hakukuwa na ushahidi uliothibitisha kuwa Menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi iliidhinisha mauzo kupitia barua ya Mkurugenzi wa Ubinafsishaji kwenda shamba la Gombe yenye kumbukumbu namba CHC/DV/1/13/288 ya tarehe 15 Aprili 2013 kwa mauzo ya shamba hilo kwa shilingi milioni 83.7 kama inavyotakiwa na taratibu za ubinafsishaji.

Napendekeza ifanyike tathmini ya matokeo ya kisheria yatakayobadilisha mfumo mzima na kuwanzisha mfumo mpya ambao utafuata taratibu sahihi za mauzo. Hii ni pamoja na vibali vya kuidhinisha na kutoa bei ya mauzo kulingana na thamani iliyopo ya soko iliyofanyiwa tathimini. Vilevile, kwa kufuata utaratibu wa kiushindani, shamba la Gombe lipewe nafasi ya kwanza ya kuwamua kwa bei iliyopo ya soko na kulipa tofauti ya bei.

6.1.14 Mauzo ya Hisa za Shirika la Usafiri Dar es salaam

UDA lilikuwa na uwezo wa kuwa na jumla ya hisa za mtaji 15,000,000 kwa thamani ya shilingi 100 kwa kila hisa. Hisa asilimia 47.5 (sawa na hisa 7,119,697) zilitolewa sokoni, ambapo asimilia 51 ziliuzwa kwa Benki ya Watu wa Dar es Salaam, na asilimia 49 ziliuzwa kwa Serikali ya Tanzania. Asilimia 52.5 zilizobakia ambazo ni 7,880,303 hazikugawiwa. Bodi ya Wakurugenzi iliziuza kwa Kampuni ya Simon Group Limited. Kufuatia maswali bungeni katika mkutano wa mwezi Julai mwaka 2011 kuhusu mauzo ya hisa za UDA ambazo zilikuwa bado hazijagawiwa, nilitakiwa kuchunguza muamala huo na tulibaini yafuatayo:

- Bodi ya Wakurgenzi ya UDA haikuwa na mamlaka ya kuuza hisa za UDA. Bodi ilipuuza ushauri wa Shirika Hodhi la Mali za Serikali wa kuuza hisa katika soko la ushindani. Badala yake hisa ziliuzwa kwa Kampuni ya Simon Group Limited kwa bei ya shilingi 298 kwa hisa, ambayo ni asilimia arobaini ya bei ya hisa iliyopo kwenye ripoti ya tathmini ya mwezi Oktoba mwaka 2009 (bei ya shilingi 744.79 kwa hisa mwezi Oktoba na shilingi 656.15 kwa hisa ya mwezi Novemba). Mwisho, Simon Group ililipa shilingi 145 kwa hisa (jumla shilingi milioni 285).
- Serikali haikuwa na mwakilishi katika Bodi ya Wakurugenzi ya UDA licha kwamba inamiliki asilimia 49 ya hisa za UDA. Hakuna ushahidi kwamba Msajili

wa Hazina na Shirika Hodhi la Mali za Serikali liidhinisha mauzo ya hisa za UDA.

- Hisa za UDA ambazo hazikugawiwa ziliuzwa kwa Kampuni ya Simon Group kwa shilingi bilioni 1.14. Kampuni ya Simon Group ililipa asilimia 24.9 tu ya bei ya makubaliano (shilingi milioni 285) na kuweka fedha kwenye akaunti ya CRDB namba 01J1021393700. Hakuna ushahidi kwamba kiasi cha asilimia 75.1 (shilingi milioni 858) kilichobaki kililipwa.
- Mwenyekiti wa UDA alipokea shilingi milioni 320 kupitia akaunti yake binafsi ikiwa ni malipo ya huduma ya ushauri (consultancy service) kwa Kampuni ya Simon Group Limited. Malipo hayo yanadaiwa na Simon Group Limited kuwa ni sehemu ya malipo ya hisa za UDA. Ninashauri Msajili wa Hazina kutambua na kufuatilia iwapo kiasi cha hisa cha asilimia 75.1 ambacho hakijalipwa kama kimelipwa kikamilifu.

SURA YA SABA

MASUALA MENGINEYO MUHIMU

7.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha masuala mengineyo muhimu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine yakiwa na Mapendekezo ya nini kifanyike ili kutoa ufumbuzi wa masuala hayo. Masuala hayo yamewekwa katika jedwali kama ifuatavyo:

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
1.	**MFUKO WA PENSHENI WA LAPF**	**Madeni ya wafanyakazi wasiokatwa kodi**	
		Riba iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania kwa mujibu wa sheria katika kipindi cha mwaka 2015 ni asilimia 16. Aidha, kifungu 27(1)(b)(ii) cha sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 kinamtaka mwajiri anayetoa mikopo kwa waajiriwa kwa riba iliyo chini ya kiwango cha riba kilichotolewa kisheria, tofauti itakuwa ni faida na ni lazima iwekwe katika mahesabu ya kutafuta kodi ya mwajiriwa katika mapato ya mwajiriwa. Katika mwaka huu wa ukaguzi, mfuko ulitoa mikopo kwa waajiriwa wake yenye thamani ya Shilingi bilioni 11 ukilinganishwa na mikopo ya mwaka yenye thamani ya bilioni 9 ambayo ilitolewa kwa riba ya	Menejimenti ya mfuko wa pensheni wa LAPF inawajibu wa kufanya hesabu na kuhakikisha faida inayopatikana kutokana na Mfuko kutoa riba ndogo kuliko iliyotolewa na Benki Kuu kisheria zinaingizwa katika hesabu ya kodi ya mapato inayotokana na mapato. Pia, Mamlaka ya Mapato ina wajibu wa kutoa faini pamoja na adhabu kwa wale wote ambao

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		asilimia 5. Tofauti ya asilimia 11 haikuingizwa katika hesabu za kodi ya mwajiriwa ili kutimiza wajibu wake wa kulipa kodi. Faida ya riba iliyotolewa chini ya kiwango cha riba kilichothibitiswa na Benki kuu ya Tanzania ni shilingi bilioni 1.21 (shilingi bilioni 11 * asilimia 11) ambayo haikulipiwa kodi. Hali hii hupelekea ukwepaji wa kodi ambao utausababishia Mfuko kupigwa faini na adhabu kama ilivyoainishwa katika sheria ya mapato ya mwaka 2004 chini ya kifungu cha 100.	wanavunja sheria pindi wanapokwepa kodi.
2.	**Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kigoma (KUWASA)**	**Wadaiwa wasiokuwa na nyaraka za uthibitisho-Shilingi 952.15milioni.**	
		Mamlaka imetoa ripoti ya madeni yenye thamani ya shilingi bilioni1.88 kutoka kwa wateja wake. Hata hivyo, nyaraka zilizopo zinatosha kuthibitisha madeni yenye thamani ya shilingi milioni 925.63 na kufanya wadaiwa wenye madeni yenye thamani ya shilingi milioni 952.15 kutokuwa	Menejimenti ya KUWASA inabidi ithibitishe uhalali wa waidaiwa kwakuwa na nyaraka za ukweli, ulinganishi, kuhakiki na kuchambua madeni. Pia,

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		na nyaraka za uthibitisho wa madeni. Mamlaka ilishindwa kuthibitisha kuwepo kwa wadaiwa hao.	menejimenti inashauriwa kuwasiliana mara kwa mara na Bodi yake kabla ya kufanya maamuzi na kuripotiwa madeni vizuri katika hesabu.
3.	**TAASISI YA SARATANI OCEAN ROAD**	**Upungufu mkubwa wa madawa**	
		Katika mwaka huu wa ukaguzi Taasisi ya Saratani ya Ocean Road iliomba Serikali kupitia Bohari ya Dawa kiwango cha aina 54 za dawa za saratani. Hadi tarehe 30 mwezi wa sita mwaka 2015, taasisi ilipokea aina 19 za dawa zilizotimia (asilimia 35). Aina 8 za tiba hazikupokelewa zote (asilimia 15 ya maombi yaliyowasilishwa) na aina 27 zilizobaki (asilimia 50) hazikupokelewa kabisa.	Kwakuwa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ni taasisi pekee iliyobobea kwa uchunguzi na matibabu ya Saratani nchini Tanzania, Menejimenti inahimizwa kuendelea kufuatilia upatikanaji wa dawa ili kuhakikisha zinapatikana.
4.	**TAASISI YA KITEKNOLOJIA DAR ES SALAAM (DIT)**	**Taasisi haitambuliwi na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)**	
		Kampasi ya Mwanza ya Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam (DIT) ni sehemu pekee ambayo inaweza kutumika kutoa mafunzo ya teknolojia ya ngozi. Kwa sasa kampasi ya Taasisi ya Mwanza imeidhinishwa kutoa	MenejimentI inashauriwa kwenda sambamba na Serikali kubaini njia za kupata fedha za kuendesha mafunzo na

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		mafunzo mafupi tu. Taasisi haijapata idhini ya utambulisho kutoka kwa NACTE. Pia usajili wa muda unaisha mwezi wa tisa mwaka 2016. Ili taasisi ikidhi vigezo vya kutoa mafunzo ya muda mrefu katika mafunzo ya teknolojia ya ngozi, inahitaji kuwa na wafanyakazi waliokidhi viwango vya elimu ya teknologia ya ngozi. Upungufu wa wafanyakazi katika teknolojia ya ngozi unasababisha uchelewaji wa Taasisi kufanikisha mpango mkakati wa kuwa kituo cha mafunzo ya teknolojia ya ngozi kwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi.	kutoa mafunzo kwa wafanyakazi ili kupata vigezo vinavyohitajika katika teknolojia ya ngozi ambapo itasaidia Taasisi kupata vigezo vya kupewa kibali cha utambulisho na NACTE.
5.	**CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA (CBE)**	**Ada ambayo haikupelekwa benki kiasi cha shilingi milioni 251.03**	
		Ofisi ya fedha ya CBE ilitoa risiti kwa wanafunzi zenye thamani ya Shilingi milioni 251.03 bila kuingiza hela hizo kwenye akaunti ya chuo. Kutokana na tukio hilo, wahasibu watatu walifukuzwa kazi na mhasibu mkuu alishushwa cheo na kuhamishiwa kampasi ya Mwanza. Mpaka leo utawala umeweza kukusanya Shilingi milioni 68.29	Menejimeti inashauriwa kujenga na kuwanzisha mkakati wa kuhakikisha mapato yaliyopotea kutokana na ubadhilifu yanarudishwa ndani ya muda muafaka.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		kutoka kwa wanafunzi.	
6.	**Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma**	**Kutokuwa na makabidhiano ya miradi iliyokamilika kwa Halmashauri ya Manispaa.**	
		Bodi ya wakurugenzi iliagiza Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma kukabidhi miradi iliyokamilika na vituo vingine kwa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma katika kikao chao Mawasiliano kati ya Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu na Halmashauri umebaini kwamba, Halmashauri iliiomba Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu kukabidhi vituo 32 na miundombinu iliyokamilika. Hadi ukaguzi unamalizika, Novemba 2015, mchakato wa makabidhiano ya miradi haukuwa umekamilika. Vilevile, orodha na thamani ya miradi iliyokamilika haikuwandaliwa na Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu. Kutokufuata maelekezo ya Bodi kumesababisha mamlaka kuingia gharama za ukarabati wa miradi ambazo zilitakiwa ziwe gharama za Halmashauri	Menejimenti inashauriwa kuzingatia maelekezo ya Bodi na kukabidhi miradi 32 ya vituo viliyokamilika ili kupunguza mzigo wa gharama.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		kama ingekuwa imekabidhi miradi hiyo.	
		Ulipaji wa gharama zote za mkataba kabla ya ukamilikaji wa utekelezaji	
		Kanuni ya manunuzi No.114 ya 2013 inahitaji chombo kinachofanya manunuzi kuwajibika katika ufanisi wa menejimenti ya manunuzi ya bidhaa, huduma na kazi zinazofanywa na Mamlaka. Mamlaka iliingia mkataba na kampuni ya watoa huduma ya ushauri inayojulikana kama M/s Africa Property Ltd kuhusu kutathmini mali zinazomilikiwa na Mamlaka pamoja na kuwandaa rejista ya mali kwa gharama ya mkataba ya Shilingi milioni 33.39. Huduma ilitarajiwa kutolewa Agosti 2015. Hata hivyo, rejista ya mali isiyohamishika na ripoti ya uthaminishaji hazikuw azimekabidhiwa na mshauri huyo mpaka mwezi Oktoba 2015, ingawa asilimia 100 ya malipo ilikuwa imeshalipwa na Mamlaka. Hali hii inaweza kupelekea upotevu wa mali ya umma	Mamlaka inashauriwa kuhakikisha ufuatiliaji mzuri wa mikataba inapoanza hadi inapomalizika na malipo yafanyike kwa kiasi kilichokamilika kulingana na kazi kama mkataba unavyosema.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		kama mtoa huduma asipotimiza wajibu wake.	
7.	**Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati**	**Ucheleweshaji wa malipo ya yatokanayo na ulimbikizaji wa wa riba ya Shilingi milioni 115.97.**	
		Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Babati imekuwa na ulimbikizaji wa riba ya madeni yenye thamani ya Shilingi milioni 115.97 kutokana na kushindwa kulipa hati za malipo ya kazi ya ujenzi kwa muda unaotakiwa. Ulipaji wa riba utaathiri hali ya kifedha na kusababisha kukwamisha ufanisi wa kazi za uzalishaji za Mamlaka.	Menejimenti inashauriwa kufanya na kuhimiza ufuatiliaji kwa Wizara ya Maji ili kuhakikisha kwamba hati ya malipo zinalipwa kwa muda unaotakiwa ili kuzuia ulimbikizaji wa riba.
8.	**MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MUSOMA**	**Kutotimiza malengo**	
		Mamlaka imeshindwa kufikia malengo yake kama yalivyowekwa katika randama ya makubaliano na Wizara ya Maji. Uwiano wa idadi ya watu wanaoishi katika maeneo yenye mtandao wa maji limefikia asilimia 40 ikilinganishwa na malengo ya asimilia 82. Uwiano wa idadi ya watu wanaopata maji umefikia asilimia 76 iikilinganishwa na malengo ya asilimia 78. Uwiano wa	Menejimenti ihakikishe malengo ya shughuli za kazi yanafikiwa kama yalivyowekwa kwenye randama ya makubaliano kati ya Wizara ya Maji na Mamlaka.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		mita umefikia asilimia 76 ikilinganishwa na malengo yaliyowekwa ya asilimia 90.	
9.	**Taasisi ya utafiti ya uvuvi**	**Kutekelezwa kwa maboti yatumikayo kwa uvuvi na utafiti.**	
		Ukaguzi ulibaini kuwa kuna boti ya MV TAFIRI II iliyopo kituo cha Mwanza ambayo haijatumika tangu mwaka 2004 na uongozi haujafanya jitihada zozote za kuifanyia matengenezo. Boti ilikuwa inatumiwa kwenye shughuli za utafiti na uvuvi katika eneo la Ziwa Victoria na hivyo kuwezesha uzalishaji uliopelekea kupata mapato. Injini ya boti imeanza kupata kutu ikiashiria boti ipo kwenye hali mbaya. Kuna hatari ya uchakavu kuongezeka na kupelekea thamani ya chombo kuendelea kupungua kama hatua za haraka hazitachukuliwa.	Menejimenti inatakiwa kuchukuwa hatua za haraka za kukarabati chombo kabla hali ya chombo haijazidi kuwa mbaya.
10.	**TAASISI YA**	**Uchelewaji wa kumaliza ujenzi wa miradi**	

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
	BENJAMINI MKAPA	Katika ukaguzi wa ujenzi wa miradi ya chumba cha upasuaji na wodi za wazazi chini ya MFP II-WAVE I, pamoja na nyumba za wafanyakazi wa Nkasi, Mpanda, Mafia, Bagamoyo, Simanjiro, Kiteto na Hanang na Ngorongoro katika mradi unaofadhiliwa na Global Fund katika awamu ya tisa (9) awamu ya I & II umechelewa kwa miaka mitatu kutokana na mkandarasi wa miradi kutotimiza majukumu yake yaliyowekwa katika mkataba. Miradi kutokamilika kwa wakati kutapelekea kutotimia kwa malengo na kutaongeza gharama ambazo wafadhili hawatakuwa tayari kuufadhili tena.	Utawala unabidi uongeze jitihada za haraka za kumaliza ujenzi wa miradi inayochelewa na kuhakikisha hamna ucheleweshaji.
11.	**MAMLAKA**	**Udhaifu katika ufuatiliaji madeni ya wafanyakazi**	

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
	YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MWANZA	Mapitio ya wadeni na masurufu ya Mamlaka ya Maji nimebaini kuwa Shilingi milioni 64.5 ni madeni yasiyolipika (yamekaa zaidi ya mwaka mmoja). Kati ya Shilingi milioni 64.5 za wadeni, Shilingi milioni 28.09 ni wadeni ambao ni wafanyakazi walioacha kazi kwenye Mamlaka. Katika ukaguzi wa madai nimebaini kuwa, mmoja wa wafanyakazi alipewa masurufu ya Shilingi milioni 12.5 kwa ajili ya kulipa vibarua kwenye mradi wa Lamadi.Kati ya pesa hizo Shilingi milioni 4.09 tu ndizo zililipwa kwa vibarua na salio la Shilingi milioni 8.4 ni hela iliyotoka bila idhini ya msimamizi.	Menejimenti inashauriwa kuhakikisha masurufu yasiyo na marejesho yamerejeshwa.
		Mapungufu kwenye kanuni za manunuzi	
		MWAUWASA imeonyesha mkakati wake wa mwaka wa manunuzi ambao utatumia mfumo wa mkataba kama njia ya manunuzi ya mabomba na vifaa vingine. Katika ukaguzi tumebaini kuwa njia ya vigezo vya awali ilitumika ingawa juu ya kiwango kilichowekwa kwenye kifungu B cha	Menejimenti unashauriwa kuzingatia mfumo wa udhibiti unaoongoza manunuzi ili kuhakikisha ufanisi katika matumizi ya fedha za umma.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		ratiba ya Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2011. Mkakati wa manunuzi ya mwaka wa MWAUWASA upo kati 5 to 10 bilioni ambayo njia ya vigezo vya awali haimruhusu Afisa masuuli kufanya manunuzi kwa zaidi ya kiwango cha Shilingi milioni 500 kwa kutumia LPO. LPO zenye thamani ya Shilingi milioni 955.42 kwa ajili ya mabomba na viambata vya samani ilitolewa kwa msambazaji mmoja katika mwaka huu. Huu ni ukiukaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na inapelekea Mamlaka kutopata utendaji mzuri kwa sababu ya kukiuka kanuni za manunuzi.	
		Manunuzi ya mabomba na vifaa vingine kwa dhaarura	
		Manunuzi ya mabomba na vifaa vingine vya thamani ya Shilingi milioni 528.86 yalifanyika kwa manunuzi ya dharura bila kuwa na vigezo vya kufanya manunuzi ya dharura kulingana na kifungu cha 65 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011. Njia ya manunuzi ya	Menejimenti inashauriwa kufuata mfumo wa mchakato wa manunuzi ya umma ili kuhakikisha fedha za umma zinatumika kama ilivyotakiwa.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		ushindanishi haikufatwa, ambayo inaweza kusababisha kutokuwa na ufanisi katika manunuzi.	
		Ulipaji wa fidia ya manunuzi ya mali maeneo ya mabwawa ya maji machafu ya Butuja	
		MWAUWASA ina wajibu wa kuwalipa fidia wamiliki wa ardhi kwa maeneo walionunua kusaidia uendelezaji wa miundombinu. Kiasi cha Shilingi bilioni 1.18 kilitengwa katika mwaka wa fedha 2014/15 ingawa hakikutumika kwa dhumuni hilo kutokana na Ucheleweshaji ulisababishwa na nakisi ya bajeti. Aidha, ucheleweshaji ulichangiwa na ongezeko la gharama za fidia kwa sababu ya ongezeko ya thamani la ardhi.	Serikali inashauriwa kuweka kipaumbele ulipaji wa fidia ya manunuzi ya eneo la Butuja kwa sababu idadi ya watu wa mji wa Mwanza inaongezeka na uhitaji wa maeneo ya kumwaga maji machafu unaongezeka.
12	**CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**	**Utoaji wa mikopo kwa wafanyakazi bila sera ya utoaji na usimamizi wa mikopo.**	
		Mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 165.45 ilipitishwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa wafanyakazi wake lakini hapakuwa na sera maalumu iliyowekwa kudhibiti utoaji wa mikopo husika. Pia mikopo ya Shilingi milioni 132.68 ilikuwa imeshapita muda	Menejimenti inashauriwa kuwanzisha sera ya utoaji na usimamizi wa mikopo kwa wafanyakazi na kuwekeza nguvu katika kukusanya mikopo iliyofikia muda wa

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		wake wa kulipwa lakini bado wafanyakazi husika hawakurejesha mikopo hiyo. Kutokuwepo kwa sera husika inaashiria usimamizi wa mikopo usioridhisha na kufanya ukusanyaji wa mikopo hiyo kutofanikiwa.	kulipwa.
13	**SHIRIKA LA ELIMU KIBAHA**	**Ukosefu wa makubaliano ya kimkataba wa mkopo kati ya Shirika la Elimu Kibaha na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**	
		Shirika la Elimu Kibaha ilipokea mkopo wa vifaa vya tiba vyenye thamani ya Shilingi milioni 360.7 kutoka kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Hata hivyo, hatukuweza kupata mkataba ulioorodhesha masharti na makubaliano ya mkopo husika.	Menejimenti inashauriwa kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya katika kuwandaa na kusaini mkataba wa mkopo husika.
14	**CHUO KIKUU CHA USHIRIKA MOSHI**	**Madai yamuda mrefu yasiyolipwa**	
		Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kina madai ya kiasi cha Shilingi bilioni 1.93 (baada ya makato ya kisheria). Mchanganuo wa kimiaka inaonesha madai ya kiasi cha Shilingi milioni 755.45 (asilimia 39) yalikuwa yanazidi miezi 12 na bado hayajalipwa ambapo mengi ya madai haya yanatokea Hazina kutokana na stahiki mbalimbali za	Menejimenti inahitaji kukuza mipango endelevu itakayowezesha namna madai yatakavyokusanywa na kuwekeza nguvu zaidi katika ukusanyaji wa madai.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		wafanyakazi. Madai katika kipindi cha ukaguzi yanajumuisha malimbikizo ya kiinua mgongo yanayogharamiwa na Hazina.	
15	**MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA TANZANIA (TCAA)**	**Usalama duni na Hakika ya ubora wa shughuli za Mamlaka**	
		Ukaguzi wa usalama na uhakika wa ubora hakika uligundua kwamba, ukaguzi wa usalama ulikuwa haufanyiki kwa mujibu wa Mpango wa Utekelezaji. Usalama na shughuli 205 zilipangwa lakini ni 166 tu ndizo zilitekelezwa. Shughuli hizo zilikuwa na madhumuni ya kulinda abiria, wafanyakazi na umma kwa ujumla dhidi ya kuingiliwa kwa kuvunja sheria ikizingatia usalama, utaratibu na ufanisi wa ndege kama ilivyoelezwa katika sera ya ICAO. Hii inatokana na kutokufuatwa kwa sera ya ICAO ya usafiri wa anga kwenye usalama na ubora wa viwanja vya ndege, ndege, kampuni za utunzaji na waendeshaji wengine. Utendaji usioridhisha kwenye usalama na ubora utaathiri usalama na ubora wa shughuli za usafiri wa	Ninapendekeza Menejimenti ihakikishe ukaguzi wa ratiba na wa kushtukiza unatekelezwa ili kuhakikisha usalama na ubora wa huduma unaboreshwa.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		anga.	
16	**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)**	**Udhaifu juu ya usimamizi wa madai**	
		Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina wastani wa madai wa Shilingi bilioni 57.53 kwa mwaka unaoishia tarehe 30 mwezi wa sita 2015. Hili ni ongezeko la asilimia 16 kutoka miaka ya nyuma. Katika deni hilo, Shilingi bilioni 31.54 lilikuwa linazidi mwaka mmoja. Hii inaashiria hatari ya kushindwa kukusanya madai husika ya Mamlaka.	Menejimenti inashauriwa kuwanzisha mchakato wa kisayansi juu ya ukusanyaji madai ambayo utasaidia kupata fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za Mamlaka.
		Matumizi hafifu ya Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano	
		Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilifunga Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano (TIMS) kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 20.66. Dhumuni la kufunga mfumo huo ni kusimamia mawasiliano na hasa katika maeneo ya uhakiki wa mapato, ubora wa huduma, usimamizi wa fedha za simu, mpango unaojiendesha kupunguza na kusimamia udanganyifu. Hata hivyo, ukaguzi wangu uligundua kuwa hakuna mfumo wa usimamizi katika mapato ya muda wa maongezi ili kuhakikisha	Menejimenti inashauriwa kuongeza kasi katika kutekeleza mfumo wa kuhakiki wa mapato ili kupata faida ya ongezeko la mapato.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		usahihi wa mapato japokuwa mfumo unaweza kuhimili hilo. Kuchelewa kufunga mfumo huo kuunazuia nguvu ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali.	
17	**HOSPITALI YA TAIFA YA MUHIMBILI**	**Serikali kushindwa kutoa fedha za mradi wa maendeleo zenye thamani ya Shilingi bilioni 9.20**	
		Sehemu ya shughuli muhimu za Hospitali ya Taifa ya Muhimbili zinafadhiliwa na ruzuku ya Serikali. Hospitali ilikuwa na bajeti Shilingi billion 9.20 katika kipindi cha mwaka kwa ajili ya shughuli za kimaendeleo lakini haikupokea fedha zozote kutoka Serikalini. Kutokana na hilo, Hospitali ilishindwa kutekeleza mipango endelevu ya maendeleo.	Serikali inashauriwa kuhakikisha fedha zinatolewa kama zilivyopitishwa katika bajeti. Pia, Menejimenti ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili inashauriwa kuweka nguvu katika kuongeza vitegauchumi vya ndani ili kuendesha miradi ya maendeleo.
		Bidhaa zilizopo njiani zenye thamani ya Shilingi bilioni 2.03	
		Bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 2.03 zilioneshwa kama bidhaa zilizopo njiani kutoka Bohari Kuu ya Dawa tokea Mei 2012. Bidhaa hizo zilikutwa kwenye hati 23 za madai kutoka Bohari	Menejimenti inashauriwa kufanya ulinganisho na Bohari Kuu ya Dawa ili kupata idadi sahihi ya dawa zilizopo

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		Kuu ya Dawa kama bidhaa zilizopo njiani kutoka Bohari Kuu ya Dawa. Hali hii inaonekana si ya kawaida kwani bidhaa hazitegemewi kukaa zaidi ya wiki moja ikizingatiwa Bohari Kuu ya Dawa na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili zote zipo mkoa wa Dar es Salaam. Hali hii pia inaashiria kuwa labda dawa hizo zilipotea au hapakufanyika ulinganisho sahihi. Hii pia inaweza kuwathiri uwezo wa Hospitali katika kujiendesha. Nina shaka dawa hizo muhimu zinaweza kupotea bila ufahamu wa Menejimenti ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.	njiani na kugundua mapungufu.
18	**BOHARI KUU YA DAWA (MSD)**	**Madai ya muda mrefu yasiyolipwa kutoka kwenye miradi inayofadhiliwa**	
		Bohari Kuu ya Dawa ina salio la madai yenye thamani ya Shilingi milioni 453.41 ambayo yamekuwa yakidaiwa kwa zaidi mwaka mmoja. Madai haya yanatokana na huduma zilizotolewa kwa wafadhili wa miradi wa kimataifa kwa miaka ya nyuma. Wafadhili hawa ni pamoja na, *Shirika la* Umoja wa Mataifa *la* Kuhudumia *Watoto* (UNICEF), *Shirika*	Menejimenti inahitaji kuongeza kasi katika mchakato wa kufuatilia na kukusanya madai ya Bohari. Menejimenti pia inashauriwa kuhifadhi vizuri kumbukumbu zote zinazohusiana na miradi ya

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		la Afya Duniani *(*WHO), Jumuiya ya Misaada la Norway (NORWEGIAN PEOPLE AID), Shirika la Kupambana na Malaria la Italia, Shirika *la Umoja wa* Mataifa na Idadi ya Watu (UNFP) na Mradi wa Danida Kagera (DANIDA KAGERA PROJECT). Kuna hatari madai haya yanaweza kutokulipwa kutoka kwa wafadhili hawa ikizingatiwa kuwa yamekaa muda mrefu bila kulipwa na pengine baadhi ya miradi imeshafungwa.	ufadhili kwa ajili ya ulinganisho na ukusanyaji wa mapato ya Bohari Kuu ya Dawa yaliyotumika kwenye miradi husika.
19	**SHIRIKA LA MAGAZETI TANZANIA (TSN)**	**Ukosefu wa viambatisho vya malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa wakala wa forodha**	
		Malipo yenye thamani ya Shilingi milioni 238.02 yalilipwa kwa wakala wa forodha mwenye jina la Walmax Freight Forwaders Co. Limited. Fedha hizi zililipwa kwa kuzingatia hati ya malipo ya kodi kutoka kwa Walmax lakini hapakuwa na ripoti ya tathmini ya kodi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na kumbukumbu ya malipo. Hii inahatarisha uhakika iwapo malipo yaliyolipwa kwa Walmax yalifikishwa kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania au ni ukosefu tu	Menejimenti inashauriwa kuomba viambatisho husika au vinginevyo ikusanye fedha hizo kutoka kwa Wakala wa Forodha.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		wa viambatisho vya nyaraka kwa ajili ya malipo hayo. Hii ni tofauti kabisa na utaratibu wa kawaida katika usimamizi wa fedha kwani nyaraka muhimu kama viambatisho vya malipo ni lazima kuwepo kabla ya malipo.	
20	**SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)**	**Ukosefu wa wigo wakuingia kwenye mfumo wa TANCIS**	
		Ili Shirika la Viwango Tanzania liweze kudhibiti uvushaji wa mali katika mipaka, Shirika litahitaji taarifa zote za mali zinazoingia na kuidhinishwa katika vituo vya mipakani ambazo zinahifadhiwa na mfumo wa TANCIS wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Wakati wa ukaguzi uligundua kwamba taarifa hizi hazikuwepo kwa wafanyakazi wa Shirika la Viiwango japokuwa idhini ya kuingia kwenye mfumo ilishatolewa. Kutokana na hayo, baadhi ya uvushwaji wa mali unaruhusiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania bila taarfia kwa Shirika la Viwango Tanzania.	Menejimenti inashauriwa kuweka nguvu za ziada katika kupata wigo wa kuingia kwenye mfumo huo TANCIS wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa sababu Mamlaka zote ni kwa maslahi ya Taifa.
21	**MAMLAKA YA MAJI SAFI NA**	**Mawando ya Mtandao wa Maji**	
		Wizara ya Maji inatakiwa kutoa fedha kwa ajili ya	Serikali inashauriwa

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
	USAFI WA MAZINGIRASHINYANGA (SHUWASA)	kuongeza mawando ya mtandao wa maji katika Manispaa ya Shinyanga kipitia awamu ya pili (II) ya WSDP. Hata hivyo, fedha hizi hazikutolewa na kusababisha Mamlaka kushindwa kupanua mtandao wa maji. Kwa kupitia vyanzo vya fedha vya ndani, Mamlaka iliweza kuongeza mtandao wa maji kwa kilometa 3.2. Mtandao wa maji kwa sasa umefikia asilimia 61 ya idadi nzima na kubakisha asilimia 39 ya idadi ambayo inatakiwa kufikiwa. Hali hii inapunguza mapato ya Mamlaka na kunyima haki ya msingi ya wananchi kupata maji safi na salama.	kutoa fedha kama zilivyoidhinishwa kwenye bajeti. Menejimenti inashauriwa kuendeleza uwezo wa ndani kwa kuweka nguvu zaidi ili kufikia asilimia 100 ya huduma ya maji kwa wakazi wote.
22	**MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA (LUWASA)**	**Ukosefu wa fedha unaoikabili Mamlaka**	
		Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa MazingiraLindi (LUWASA) inadaiwa madeni ya muda mrefu ikiwa ni pamoja na Shilingi milioni 445.10 ya Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) na Shilingi milioni 901.17 ya mkandarasi. Hii imesababishwa na ukosefu wa fedha unaoikabili Mamlaka kutokana kushindwa kukusanya	Menejimenti inashauriwa kuongeza kasi ya utaratibu wa ukusanyaji wa mapato na madeni kutoka kwa wateja. Pia Serikali inashauriwa kuiwezesha Mamlaka ili iweze kufikisha maji safi na

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		mapato kutoka kwa wateja na ufinyu wa bajeti.	salama kwa wananchi.
23	**MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRAKAHAMA (KUWASA)**	**Udhaifu katika ukusanyaji wa mapato**	
		Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa MazingiraKahama (KUWASA) ina salio la madai ya Shilingi milioni 679.13 ambayo yamekuwa yakidaiwa kwa wateja kwa zaidi ya mwaka mmoja. Hata hivyo, salio la madai hayo yameongezeka kwa asilimia 41 wakati mapato yameongezeka kwa asimilia 27 tu ukilinganisha na mwaka jana. Hii imesababishwa na mbinu dhaifu za Mamlaka za ukusanyaji wa madai na zinazoathiri uwezo wa kifedha.	Menejimenti inahitaji kuharakisha taratibu za ufuatiliaji na ukusanyaji wa madai kutoka kwa wateja.
24	**HIFADHI ZA TAIFA ZA TANZANIA (TANAPA)**	**Malipo ya ziada ya gharama za kukodisha**	
		Waraka namba TNP/HQ/A.10/01 wa Hifadhi za Taifa za Tanzania (TANAPA) unahusiana na posho ya pango iliyoidhinishwa katika kiwango cha Shilingi 600,000 kwa mwezi kulipwa kwa wafanyakazi. Katika ukaguzi wa posho za pango, tuligundua kiwango cha kodi ya pango yenye thamani ya Dola za Marekani 1,120 kwa mwezi sawa na Shilingi million 2.26 ililipwa kwa mmoja wa Wakurugenzi kama	Kuna haja ya kuhakikisha fedha za umma zinatumika vizuri ili zielekezwe katika shughuli zilizopangwa.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		posho ya pango tofauti na Waraka namba TNP/HQ/A.10/01. Kulikuwa na malipo yaliyozidi ya Shilingi milioni 19.48 kwa mwaka.	
25	**CHUO KIKUU CHA DODOMA**	**Utunzaji wa Mikataba ya Nyumba za Kupanga**	
		Chuo Kikuu cha Dodoma kimepanga nyumba kutoka NHC BK A MEDELI na NHC BK B MEDELI. Katika ukaguzi niligundua mapungufu yafuatayo: wapangaji walianza kupanga na kukaa miaka miwili kabla kusaini mikataba ya kukodi na kuongeza muda wa mikataba kabla muda wa mkataba wa kwanza kwisha. Wenye Nyumba wote walikodisha tarehe 27.11.2012 kwa ajili ya kipindi kuwanzia 01.03.2010 hadi 31.03.2013. Mikataba yote ilisainiwa tarehe 18.02.2012 na kuongezewa muda tarehe 18.12.2012 mpaka 30.04.2016. Hali hii inaweka mikataba hiyo kukosa uhalali.	Ninashauri Menejimenti ya Chuo ihakikishe masharti ya mikataba yanafuatwa.
26	**TAASISI YA UTAFITI WA MAGONJWA YA BINADAMU (NIMR)**	**Ulipaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)**	
		Wauzaji walikusanya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya	Serikali inahitaji kuweka hatua za kuhakikisha Kodi ya Ongezeko la

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		Binadamu (NIMR) lakini hawakutoa risiti za kielektroniki; badala yaje walitoa risiti za kuandikwa kwa mkono EFD au ankara ya kodi. Katika hali nyingine, wauzaji walitoa risiti za EFD ziilizoonesha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ni sifuri tofauti na hati ya malipo iliyotolewa. Hati za malipo zinaonesha kodi ya Ongezeko la Thamani ambapo Kodi hiyo iliyolipwa na NIMR kwa wauzaji 53 haikufikishwa kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ni Shilingi 120,169,190.	Thamani zinazolipwa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kwa wauzaji zinalipwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)
27	**SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC)**	**Udhaifu katika Usimamizi wa Madai ya Shirika**	
		Utaratibu ni Mwongozo wa Kifedha wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) unautaka uongozi kupata uthibitisho kutoka kwa wateja kila mwisho wa mwaka. Pia, Sera ya Mikopo ya Shirika inahitaji ufanywaji wa tathmini ya mikopo. Yafuatayo ni udhaifu ulioonekana kuhusiana na madai ya Shirika: • Hakukuwa na vielelezo vya ushahidi vinavyoonesha kuwa uthibitisho wa madai	Menejimenti inashauriwa kuongeza nguvu katika ufuatiliaji wa madai ya muda mrefu. Pia, Menejimenti ihakikishe sera na taratibu zake zinafuatwa.

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		ulifanyika. • Hakukuwa vielelezo vya ushahidi kwamba tathmini ya mikopo ilifanyika. • Madai ya Shilingi bilioni 1.76 ilikuwa yanadaiwa kwa zaidi ya miezi sita. • Ongezeko hatarishi la kushindwa kukusanya madai kutoka kwa wateja husika.	
28	**SHIRIKA LA MAJI SAFI NA MAJI TAKA DAR ES SALAAM**	**Madeni ya muda mrefu ya Shilingi bilioni 29.63**	
		Hadi tarehe 30 June 2015, DAWASCO ilikuwa na madeni yapatayo Shilingi bilioni 51.71, kati ya hayo Shilingi bilioni 29.63 (asilimia 57.10) yalikuwa ni madeni ya zaidi ya miezi 12. Nina shaka iwapo madeni haya yatalipwa kwani yamekaa kipindi kirefu bila kulipwa	Menejimenti inashauriwa iongeze nguvu ya ukusanyaji wa madeni na kuhakikisha masharti magumu yanawekwa kuzuia madeni yasiyolipwa kwa muda mrefu.
		Kutowasilishwa kwa makato ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu	
		DAWASCO imeiarifu bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kuwa ina wafanyakazi sitini na sita (66) wafaidika wa mikopo ya Bodi kwa mujibu wa Kifungu cha 20(1) - (2) cha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu mwaka ya 2004. Hata hivyo, imegundulika	Menejimenti inashauriwa kuhakikisha walengwa wote waliofaidika na mikopo kutoka HESLB wanakatwa madeni yao na kiasi hicho kuwasilishwa

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		kwamba makato yanafanyika kwa wafanyakazi 15 tu kati ya idadi iliyopo. Huu ni ukiukwaji wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya mwaka ya 2004 na inakaribisha faini kama ilivyo kwenye kifungu namba 21.	kwenye Bodi ya Mikopo.
29	**MFUKO WA TAIFA WA HIFADHI YA JAMII(NSSF)**	**Usimamizi wa nyumba za kuuza za Mtoni Kijichi haufati taratibu za uwekezaji za Benki Kuu ya Tanzania na Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**	
		Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii upo katika awamu ya iii ya mradi wa uuzaji wa nyumba za Mtoni Kijichi wenye makadirio ya Shilingi 137.7 bilioni. Tarehe 30 Juni 2015 kiasi cha Shilingi bilioni 79 za Mfuko huo kilitumika katika ujenzi wa nyumba hizo ambazo ziliamuliwa kuuzwa ndani badala ya kufuata maelekezo ya wasimamizi kwa kutumia benki au makampuni ya mikopo kama ilivyoelezwa katika kanuni namba 13 ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na mwongozo wa uwekezaji wa Benki Kuu.	Menejimenti inashauriwa kuzingatia sheria, kanuni na maelekezo yanayotelewa na wasimamizi wake Kitendo chochote cha kutofuata maagizo kinatakiwa kuwasilishwa kwa maandishi kwa mdhibiti wa sekta na kukubaliana muda uliopangwa kwa ajili ya kufuatwa.
		Manunuzi ya ardhi Bila ushindani (Toka kwa	

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		Muuzaji Mmoja) Shilingi bilioni 15.16	
		Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ilibajeti shilingi bilioni 1.6 kwa manunuzi ya kiwanja kupitia zabuni za ushindani. Hata hivyo ilitumiia chanzo kimoja katika manunuzi ya kiwanja kilichogharimu kiasi cha shilingi bilioni 15.16, nimegundua kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma hawakujulishwa kinyume cha kanuni namba 87 ya Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma, 2013 inayohitaji kuwasilishwa kwa taarifa za mkataba wa tuzo kwake Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ndani ya siku saba kuhusu ya mchakato wa manuunuzi endapo chanzo kimoja kilitumika	Menejimenti ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii inatakiwa kuzingatia mpango wake, bajeti na Kanuni za Manunuzi ya umma za Mwaka 2013 kwa ajili ya kuhakikisha manunuzi yanafanyika katika ushindani ili kupata huduma kwa bei nafuu.
30.	**CHUO CHA KUMBUKUMBU CHA MWALIMU NYERERE**	**Uwepo wa wanafunzi wachache kuliko uwezo wa Chuo**	
		Katika mwaka wa ukaguzi, Chuo kilikuwa na jumla ya wanafunzi 1,548 katika kozi zote wakati uwezo wake ni wanafunzi 5,020 kampasi zote za Zanzibar na Kigamboni. Hii ni asilimia 31 ya uwezo kamili wa chuo. Kampasi ya Zanzibar kilikuwa na wanafunzi 150	Chuo kinatakiwa kielekeze nguvu katika kupanua na kuwanzisha kozi mbalimbali kwa kupanga mikakati ya masoko kupitia matangazo katika magazeti ya ndani na

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		hadi kufikia mwisho wa Septemba 2015 dhidi ya uwezo wa wanafunzi wa 2,520. Uandikishaji wa chini unaathiri mapato ya Chuo kupitia fedha zinazokosekana kwenye ada na matumizi hafifu ya miundombinu ya mafunzo na vifaa vingine.	kupitia tovuti ya Chuo.
31.	**MFUKO WA PENSHENI WA UTUMISHI WA UMMA**	**Upungufu wa udhibiti juu ya utambulisho na uthibitisho kwenye Mfumo wa Pensheni kwa Njia ya Mtandao (ePen)**	
		Matokeo ya uchunguzi wa taarifa za wanachama kwenye mfumo wa Mfumo wa Pensheni kwa Njia ya Mtandao yanaonesha wanachama 311 walisajiriwa wakiwa na umri wa chini ya miaka 18, wanachama 2,213 walisajiriwa katika umri wa miaka 60 au zaidi na wanachama 520 walisajiliwa bila uwepo wa taarifa zao kama vile, tarehe za kuzaliwa, wakati wa kustaafu waliwekewa kumbukumbu za tarehe za kuzaliwa za mbele kuliko tarehe walizoajiriwa, wanachama waliingizwa kwenye orodha ya wastaafu wakati walichangia kwa kipindi kisichozidi miezi 180; na wanachama 533 wanalipwa pensheni	Mfuko unapaswa kuwa na mfumo mzuri wa kuhifadhia kumbukumbu za wanachama wa Mfumo wa Pensheni kwa Njia ya Mtandao. Hili linaweza kufanikiwa kwa kufanya ukaguzi ambao utahitajika kufanywa kwa waajiri wa wanachama ili kuepuka uwezekano wa kulipa kiinua mgongo kisicho sahihi au malipo ya pensheni ambayo yanapelekea upotevu wa

Na.	Shirika	Masuala yaliyopewa uzito	Maoni
		baada ya kuwacha kazi wakati walikuwa hawajafikisha miaka 55 kinyume na sera na kanuni za Mfuko.	mapato kutokana na taarifa zisizo sahihi kuingizwa katika mfumo

HITIMISHO

Sehemu hii inahitimisha masuala ambayo yameainishwa katika ripoti hii. Haya masuala yanayohitaji mwitikio kutoka kwa Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi, na Menejimenti za Mashirika husika ya Umma.

Mapendekezo mengi yaliyotolewa katika ripoti hii yametokana na ripoti za ukaguzi za Mashirika ya Umma husika, ambapo mapungufu yaliyojitokeza tayari yalishawasilishwa kwa Bodi zao za Wakurugenzi. Kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma kinampa nguvu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa mapendekezo kwa nia ya kuzuia na kupunguza matumizi yasiyo na tija ya rasilimali za umma, kusimamia ongezeko la pato la taifa na kuondoa upotevu wa rasilimali utokanao na vitendo vya uzembe, wizi, kukosa uaminifu, ufisadi, na rushwa ili kuwezesha utolewaji wa huduma na maisha bora kwa jamii.

Hivyo basi, ili ripoti hii iweze kuleta tija na kuongeza uwajibikaji katika rasilimali za taifa na kuongeza ufanisi katika utendaji wa Mashirika ya Umma, ni muhimu kwa Serikali na Mashirika ya Umma kutengeneza mpango kazi wa mwaka utakao elezea namna ya kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti kwa muda uliopangwa. Kwa mapendekezo niliyoyatoa ambayo hayajatekelezwa kwa muda mrefu, ninaishauri Serikali kuongeza juhudi zitakazopelekea kutekelezwa kwa mapendekezo hayo.

Katika tathmini ya taasisi zilizobinafishwa, ukaguzi ulibaini ukiukwaji wa taratibu katika kubinafsisha Taasisi za Umma. Hivyo basi, ninaishauri Serikali pamoja na Msajili wa Hazina kufanya tathmini ya kutosha kwa taasisi zote za umma zilizobinafsishwa kwa nia ya kufahamu iwapo taasisi husika zinafanya kazi kwa mujibu wa makubaliano ya uuzwaji wake.

Tathimini ya ufanisi katika utendaji wa mashirika mbalimbali ya umma imeonyesha kuwa kumekuwa na mapungufu katika ufuatiliaji na udhibiti wa taasisi hizo katika kutelekeza mipango mikakati yake ikiwa ni pamoja na kukosa usimamizi madhubuti wa taasisi hizi kutoka kwa bodi na viongozi wakuu wa mashirika husika.

Mfano mmojawapo ni Kampuni ya Ndege ya Tanzania na Mamlaka ya Bandari Tanzania. Kampuni ya Ndege Tanzania imekuwa ikipata hasara kwa muda mrefu sasa huku Menejimenti yake ikiwa haina mpango madhubuti wa kuiokoa kampuni hiyo kutoka katika tatizo hili ambalo limedumu kwa muda mrefu sasa.

Ninaishauri Menejimenti kutengeneza mpango madhubuti wa kufufua Kampuni hiyo kwa kutathmini na kufuatilia kiini cha tatizo lililopelekea Kampuni kuwa katika hali mbaya ya kifedha ili kuibadilisha kuwa kampuni inayotengeneza faida.

Mamlaka ya Bandari Tanzania imekuwa na malengo mbalimbali iliyojiwekea ili kutekeleza Mpango Mkakati wake wa Miaka Mitano. Nimebaini kuwa Mamlaka hiyo bado haijatekeleza kikamilifu mipango yake ikiwemo kufanyia mabadiliko makubwa katika gati ya 13 & 14.

Menejimenti ya Bandari inapaswa kuhakikisha inatekeleza shughuli ilizojipangia kuzifanya sambamba na mpango mkakati wake.

Mwisho, usimamizi wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika yote ya umma unapaswa kuimarishwa ili kuhakikisha Taasisi za Umma zinaendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika sheria za kuwanzisha kwake.

VIAMBATISHO

Kiambatanisho Namba I – Mchanganuo wa Hati Zilizotolewa katika mwaka 2014/2015

Na	Shirika la Umma	Hati
1	Chuo Kikuu cha Ardhi	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
2	Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
3	Chuo cha Ufundi Arusha (ATC)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
4	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha	Hati Inayoridhisha
5	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
6	Taasisi ya ukimwi ya Benjamini Mkapa	Hati Inayoridhisha
7	Mamlaka ya Uendelezaji Mji Mkuu Dodoma (CDA)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
8	Mamlaka ya Udhibiti wa Soko la Mtaji (CMSA)	Hati Inayoridhisha
9	Bodi ya Korosho Tanzania	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
10	Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Kijijini (CARMATEC)	Hati Inayoridhisha
11	Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)	Hati Inayoridhisha
12	Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB)	Hati Inayoridhisha
13	Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam (DIT)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
14	Taasisi ya Bahari Dar es Salaam (DMI)	Hati Inayoridhisha
15	Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE)	Hati Inayoridhisha
16	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)	Hati Inayoridhisha
17	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa MazingiraDar es Salaam (DAWASA)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
18	Deposit Insurance Board	Hati Inayoridhisha
19	Mamlaka ya Maji Safi na	Hati Inayoridhisha

Na	Shirika la Umma	Hati
	Usafi wa Mazingira Dodoma	
20	Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA)	Hati Inayoridhisha
21	Baraza la walaji la Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Nishati na Maji	Hati Inayoridhisha
22	Tume ya Ushindani (FCC)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
23	Gaming Board of Tanzania	Hati Inayoridhisha
24	Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi wa Serikali (GEPF)	Hati Inayoridhisha
25	Chuo cha Usimamizi wa Fedha	Hati Inayoridhisha
26	Chuo cha Uhasibu Arusha	Hati Inayoridhisha
27	Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW)	Hati Inayoridhisha
28	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Iringa	Hati Inayoridhisha
29	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama	Hati Inayoridhisha
30	Shirika la Elimu Kibaha (KEC)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
31	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Kigoma	Hati Yenye Shaka
32	Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa	Hati Inayoridhisha
33	Mamlaka ya Maji Lindi	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
34	Marine Parks and Reserves Unit	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
35	Mamlaka ya Maji ya Masasi Nachingwea	Hati Inayoridhisha
36	Mbeya University of Science and Technology	Hati Inayoridhisha
37	Bohari ya Dawa (MSD)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
38	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
39	Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo

Na	Shirika la Umma	Hati
40	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Moshi	Hati Inayoridhisha
41	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
42	Muhimbili University of Health and Allied Sciences (MUHAS)	Hati Inayoridhisha
43	Mamlaka na Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma	Hati Inayoridhisha
44	Mwalimu Nyerere Memorial Academy	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
45	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza	Hati Inayoridhisha
46	Chuo cha Mzumbe	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
47	Baraza la Sanaa la Taifa	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
48	Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA)	Hati Inayoridhisha
49	Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
50	Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
51	Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)	Hati Inayoridhisha
52	Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
53	Chuo cha Usafirishaji (NIT)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
54	Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro	Hati Inayoridhisha
55	NHC-PPF Investment Company	Hati Inayoridhisha
56	Taasisi ya Saratani Ocean Road	Hati Inayoridhisha
57	Mfuko wa Pensheni wa PPF	Hati Inayoridhisha
58	Public Procurement Appeals Authority (PPAA)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
59	Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA)	Hati Inayoridhisha
60	Mfuko wa Pension wa Utumishi wa Umma (PSPF)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo

Na	Shirika la Umma	Hati
61	Rasilimali Ltd	Hati Inayoridhisha
62	Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Same	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
63	Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
64	Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Singida	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
65	Udhibiti ya Mifuko Kijamii Tanzania (SSRA)	Hati Inayoridhisha
66	Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira wSongea	Hati Inayoridhisha
67	Bodi ya Sukari Tanzania	Hati Inayoridhisha
68	Baraza la walaji la Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi kavu na Majini	Hati Inayoridhisha
69	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga	Hati Inayoridhisha
70	Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi kavu na Majini (SUMATRA)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
71	Mamlaka ya Maji Tabora	Hati Inayoridhisha
72	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga	Hati Inayoridhisha
73	Bodi ya Kahawa Tanzania	Hati Inayoridhisha
74	Tanzania Commission for Science and Technology	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
75	Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA)	Hati Inayoridhisha
76	Tanzania Education Authority	Hati Inayoridhisha
77	Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
78	Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)	Hati Inayoridhisha
79	Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
80	Baraza la Taifa la Biashara	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
81	Benki ya Posta Tanzania	Hati Inayoridhisha
82	Tanzania Revenue Appeals	Hati Inayoridhisha

Na	Shirika la Umma	Hati
	Board	
83	Tanzania Smallholders Tea Development Agency	Hati Inayoridhisha
84	Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
85	Benki ya Wanawake Tanzania	Hati Inayoridhisha
86	Tax Revenue Appeals Tribunal	Hati Inayoridhisha
87	Bodi ya Chai Tanzania	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
88	Benki ya Maendeleo ya TIB	Hati Inayoridhisha
89	Twiga Bancorp	Hati Isiyoridhisha
90	UTT Asset Management and Investor Services	Hati Inayoridhisha
91	UTT-Projects and Infrastructure Development PLC	Hati Inayoridhisha
92	Universal Communication Access Fund (UCSAF)	Hati Inayoridhisha
93	Mamlaka ya Maji ya Lindi	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
94	Mamlaka ya Maji ya Tabora	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
95	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT)	Hati Inayoridhisha
96	Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASCO)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
97	Mamlaka ya Maji Kahama Shinyanga	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
98	Mamlaka ya Maji Mbeya	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
99	Shirika La Maendeleo la Taifa (NDC)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo
100	Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)	Hati Inayoridhisha
101	Kampuni ya Nyumba za Watumishi	Hati Inayoridhisha
102	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa (NIMR)	Hati Inayoridhisha Yenye Suala la Msisitizo

Kiambatanisho Namba II: Orodha ya Mizigo iliyopo kwenye orodha kuu lakini inakosekana kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Forodha

Jina la Meli: Weser wolf								
Makontena Yanayokesakana kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Forodha								
Na	**Utambulisho wa kontena**	**Ukubwa**	**Na**	**Utambulisho wa kontena**	**Ukubwa**	**Na**	**Utambulisho wa kontena**	**Ukubwa**
1	PCIU8608213	40	**29**	TGHU1548790	20	**57**	PCIU462885	40
2	PCIU8662512	40	**30**	PCIU1226559	20	**58**	BMOU4975156	40
3	PCIU8142526	40	**31**	PCIU2082733	20	**59**	FCIU9845841	40
4	PCIU8335799	40	**32**	PCIU2128156	20	**60**	PCIU9371245	40
5	PCIU8168217	40	**33**	PCIU2690902	20	**61**	PCIU9983381	40
6	TGHU6735638	40	**34**	TRHU1332061	20	**62**	PCIU889600	40
7	PCIU8511558	40	**35**	PCIU2847329	20	**63**	TGHU9879733	40
8	GLDU9063361	40	**36**	PCIU3193310	20	**64**	PCIU8304406	40
9	TENU6797520	40	**37**	PCIU3070660	20	**65**	CXOU2053546	40
10	CXDU2124634	40	**38**	PCIU2571251	20	**66**	PCIU8132008	40
11	PCIU8406681	40	**39**	PCIU2723610	20	**67**	PCIU2880421	20
12	TENU4302811	40	**40**	PCIU1802649	20	**68**	PCIU8299946	40
13	PCIU2618240	20	**41**	PCIU1522397	20			
14	PCIU1099808	20	**42**	PCIU8294072	40			
15	GESU2298970	20	**43**	PCIU8518819	40			
16	PCIU2195982	20	**44**	PCIU8091814	40			
17	PCIU1174060	20	**45**	PCIU8317429	40			
18	CRXU3200340	20	**46**	PCIU8245519	40			
19	PCIU2745190	20	**47**	PCIU8210153	40			
20	PCIU1065069	20	**48**	PCIU8206240	40			
21	PCIU1242225	20	**49**	PCIU8172860	40			
22	TEMU4593759	20	**50**	PCIU8866162	40			
23	PCIU2698462	20	**51**	TENU5120323	40			
24	PCIU1623983	20	**52**	PCIU8157660	40			
25	PCIU1893079	20	**53**	BMDU4084660	40			
26	PCIU2644430	20	**54**	PCIU8645632	40			

27	PCIU2173495	20	**55**	PCIU3080948	40			
28	PCIU1629045	20	**56**	PCIU8482296	40			

Kiambatanisho Namba III: Taasisi ambazo Bodi zake Hazijakaa Kupitisha Hesabu zake kwa wakati unaopaswa

Na	Taasisi Za Uma
1	Baraza la Kiswahili Tanzania
2	Centre for Foreign Relations (CFR)
3	Chuo cha Wanyama Pori – Mweka
4	Copyright Society of Tanzania
5	Shirika la Usambazaji wa Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASCO)
6	Bodi ya usajili ya Waandisi ya Taifa
7	Mamlaka ya Ukanda wa Uwekezaji Tanzania (EPZA)
8	Taasisi ya Elimu ya Watu wazima (IAE)
9	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga
10	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya
11	Chuo kikuu Mkwawa
12	Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC)
13	Baraza la Taifa la Mazingira – NEMC
14	National Institute of Medical Research (NIMR)
15	Shirika la Tija la Taifa (NIP)
16	Kampuni ya Ranchi za Taifa
17	Baraza la Michezo la Taifa
18	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT)
19	Bodi ya Manunuzi (PSPTB)
20	Kampuni ya Kusimamia Raslimali za Shirika la Reli Tanzania (RAHCO)
21	Mamlaka ya maendeleo ya Bonde la Rufiji -RUBADA
22	Tume ya Nguvu za Atomiki
23	Shirika la Viwango Tanzania
24	Mamlaka ya Usafiri wa anga (TCAA)

Na	Taasisi Za Uma
25	Bodi ya Maziwa Tanzania
26	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)
27	Kampuni ya Mbolea Tanzania.
28	Mamlaka ya Usajili wa Bima Tanzania
29	Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC)
30	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa (TPRI)
31	Bodi Tumbaku Tanzania
32	Shirika la Magazeti Tanzania
33	Ubungo Plaza
34	Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)
35	Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA)
36	Kampuni ya Nyumba ya Taifa (WHC)

Kiambatanisho Namba IV: Mashirika yasiyo na Bodi za Wakurugenzi au Bodi za Wadhamini

Na	Shirika
1	Hifadhi za Taifa za Tanzania(TANAPA)
2	Shirika la posta Tanzania (TPC)
3	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Makambaku
4	Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea
5	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bariadi
6	Bodi ya PambaTanzania
7	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko
8	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Geita
9	Bodi ya Utalii Tanzania
10	Makumbusho ya Taifa Tanzania
11	Bodi ya Katani Tanzania
12	Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara ((TANTRADE)
13	Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi

Na	Shirika
14	Chuo cha Wanyama Pori – Mweka
15	Centre for Foreign Relations (CFR)
16	Taasisi ya Taifa ya Sukari
17	Taasisi ya Utafiti ya Wanyama Pori (TAWIRI)
18	Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mpanda
19	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

Kiambatanisho V: Kaguzi ambazo hazikufanyika kwa sababu ya uhaba wa Fedha

Na	Jina la Shirika	Hadhi ya Mashirika ambayo hayakugaliwa
1	Shirika la Madini Tanzania (STAMICO)	Shughuli zifuatazo ziliahirishwa kwa sababu ya ufinyu wa bajeti: Ukaguzi wa mikataba ya uchimbaji madini, mapato na ziara kwenye machimbo ya dhahabu ya TANZANITE
2	Shirika la Petroli Tanzania (TPDC)	Kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, hatukuweza kukagua maeneo yafuatayo: bomba la gesi, mikataba na kutembelea bomba la gesi
3	Shirika la Ugavi wa Umeme la Tanzania (TANESCO)	Ukaguzi wa mikataba, kutembelea mabwawa na ukaguzi wa ufanisi
4	Mamlaka ya Anga Tanzania (TCAA)	Ufinyu wa bajeti ulipelekea kuto kukagua ufanisi wa utendaji, mikataba, kazi za udhibiti wa Anga, na kutathmini ukidhi wa vigezo vya usalama
5	Mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira Namtumbo	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
6	Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa vyama vya Ushirika (COASCO)	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
7	Mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira Tukuyu	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti

Na	Jina la Shirika	Hadhi ya Mashirika ambayo hayakugaliwa
8	Mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira Makambako	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
9	Mamlaka ya maendeleo ya Bonde la Rufiji	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
10	Bodi ya utalii Tanzania	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
11	Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA)	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
12	Bodi ya Mkonge Tanzania	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
13	Makumbusho ya Taifa	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
14	Mamlaka ya maji safi na usafi wa Mazingira Bariadi	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
15	Mamlaka ya Udhibi wa Mbolea Tanzania	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
16	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Geita	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
17	Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
18	Shirika la Uhandisi na Ubunifu wa Viwanda Tanzania (TEMDO)	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
19	Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
20	Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
21	Mamlaka ya Maji Korogwe	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
22	Mamlaka ya Maji Kyela	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
23	Mamlaka ya Maji Mpanda	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
24	Mamlaka ya Maji Njombe	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti
25	Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Nzega	Ukaguzi wa kisheria haukufanyika kwa sababu ya ufinyu wa bajeti

Kiambatanisho Namba VI: Kutokufikiwa kwa Viashiria vya Utendaji

Na	Viashiria Muhimu vya Utendaji	Hali ya Utendaji

01	Meli za Panamax zilizohudumiwa kwenye Gati Na. 13 & 14 katika mwaka 2016 Vipengele vidogo vifuatavyo viliongezwa kwenye Mradi wa Mlango Bahari wa Dar es Salaam (DMGP): • Uendelezaji wa Gati Na. 13 -14 • Uhamishaji wa Gati ya Kupakulia Mafuta ya Kurasini (KOJ) • Uboreshaji wa Gati Na. 8 -11	Muda wa utekelezaji wa Viashiria Muhimu vya Utendaji umeongezwa mpaka mwaka 2016.
02	Kujengwa kwa Gati ya Kupakiza na Kushusha katika meli za wazi kwa mwaka 2014.	Hakujakamilika. Manunuzi bado yapo kwenye mchakato wa zabuni ambapo imefikia katika kumalizia hatua ya pili ya tathmini ya pendekezo la kitaalamu.
03	Ujengaji wa gati nne za ziada - Gati mbili za ziada zitajengwa katika Bandari ya Mtwara kwa kipindi kilichoishia Juni 2014.	Mradi haujakamilika. Zabuni imesitishwa kwakuwa muombaji alishindwa kukidhi matakwa katika hatua ya majadiliano. Mpango uliopo sasa ni Mamlaka ya Bandari kujenga Gati moja ya ziada kwa kutumia mapato yake ya ndani kwa mwaka 2016/2017.
04	Mkondo wa kuingilia kwenye sehemu 13 za kuhifadhia makontena kufikia mwaka 2015.	Mradi haujakamilika. Mradi huu kwa sasa upo chini ya Mradi wa Mlango Bahari wa Dar es Salaam kwa udhamini wa Benki ya Dunia. Hata hivyo, kazi ya upanuzi wa mkondo wa kuingilia unatarajiwa kuanza Septemba 2016.
05	Uboreshaji wa Gati Na. 1-7 ili kuweza kuhimili meli kubwa - Gati Na. 1-7 zinatarajiwa kuboreshwa kufikia mwaka 2016	Mradi haujakamilika. Mradi unatarajiwa kumalizika Mei 2016. Kazi za kupanua na kuimarisha zinatarajiwa kuanza Julai 2016.
06	Kufupisha Gati ya Kupakulia Mafuta ya Kurasini (KOJ) ili kuruhusu meli kubwa ziingie	Mradi haujakamilika. Mpango uliopo sasa ni kuhamisha Gati ya Kupakulia Mafuta ya Kurasini

	katika Gati Na. 13 na 14 ifikapo mwaka 2014.	(KOJ). Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kihandisi unatarajiwa kukamilika Juni 2016. Uhamishaji wa Gati ya Kupakulia Mafuta ya Kurasini (KOJ) kwa kujenga Gati mpya ya kupakulia mafuta pamoja na matenki ya kuhifadhia mafuta unatarajia kuanza katika mwaka wa hesabu 2016/2017.
07	Kuongeza uwezo wa mita ya kupimia mafuta ya Gati ya Kupakulia Mafuta ya Kurasini (KOJ) kutoka mita za ujazo 740 kwa saa hadi mita za ujazo 1500 kwa saa kufikia mwaka 2013.	Mradi bado haujakamilika. Mita mpya za kupimia mafuta zimenunuliwa ambazo zitafungwa kufikia Machi 2016.
08	Kuongeza uwezo wa kuhudumia mbolea, nafaka na vimiminika katika kufikia mwaka 2015.	Mradi bado haujakamilika. Utekelezaji wa mradi utaanza baada ya kumalizika kwa upanuzi na uimarishaji wa Gati Na. 1-7 na ujenzi wa Gati ya kupakulia katika meli za wazi.
09	Ujenzi wa barabara nzuri kufikia mwaka 2013.	Mradi bado haujakamilika. Hali ya kukamilika imefikia zaidi ya asilimia na inatarajiwa kukamilika mwaka huu.
10	Kuendeleza matishari katika Bandari ya Dar es Salaam kufikia mwaka 2013.	Mradi bado haujakamilika. Kwa sasa taasisi zinazohusika zimepatiwa ombi la pendekezo ili ziweze kutuma kufikia mwisho wa Machi 2016.
11	Kupitia sera ya uwekezaji kufikia Disemba 2011.	Sera ya kwanza ya uwekezaji ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ilikamilishwa Machi 2011. Mkataba wa maandalizi ya sera ya pili ya uwekezaji imekabidhiwa kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kiweze kuipitia na kuikamilisha ifikapo Aprili 2016.